ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

BARAZA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 15 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe kwanza assalam alaykum, nichukue nafasi hii kuwakaribisha tena katika mkutano wetu wa kumi na nane wa Baraza la Wawakilishi unaoanza leo tarehe 15 Oktoba, 2009. Katika ajenda hii ya taarifa ya Spika kutakuwa na taarifa mbili kama ifuatavyo:-

1. Waheshimiwa Wajumbe katika mkutano wa kumi na saba wa Baraza la saba la Wawakilishi uliofanyika tarehe 17 Juni, 2009 huo ulikuwa ni mkutano wa bajeti, Baraza lilipitisha miswada miwili ya sheria kama ifuatavyo:

i) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi zinazohusiana na udhibiti wa Mapato ya Serikali.

ii) Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha makisio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2009-2010 kama inavyotakiwa na sheria chini ya kifungu cha 90, kifungu kidogo cha 3 cha kifungu hicho cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2007. Naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo miwili imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hiyo ni taarifa ya kwanza.

2. Taarifa nyengine ni katika kifungu cha 38 cha Sheria ya Baraza la Wawakilishi kuhusu kinga, uwezo, fursa, sheria namba 4 ya mwaka 2007 inaeleza kwamba endapo mjumbe yeyote wa Baraza la Wawakilishi atakamatwa kwa ajili ya mashtaka ya kosa la jinai au atahukumiwa kifungo na Mahakama, basi mamlaka inayohusika itamuarifu Spika kwa haraka sana na itaanisha sababu ya kukamatwa huko, sababu ya kuzuiliwa au sababu ya kifungo hicho.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mnasaba wa kifungo hicho naomba kuwaarifu kwamba mnamo siku ya tarehe 8 Oktoba, 2009 tumepokea taarifa kutoka kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar iliyonijuilisha kwamba Mhe. Abdalla Juma Abdalla ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Chonga anatuhumiwa kutenda kosa la shambulio la matusi na alifikishwa Mahakamani tarehe 28 Septemba, 2009.

Waheshimiwa Wajumbe taarifa hiyo ilifafanua kwamba Mhe. Abdalla Juma Abdalla anadaiwa kutenda kosa hilo mnamo siku ya tarehe 18 August, 2009 majira ya saa nne na nusu kwenye Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake ambapo inadaiwa kuwa alimshambulia kwa matusi ndugu Khamis Uledi Kombo Sheha wa Shehia ya Pujini Kunzini.

Waheshimiwa Wajumbe kesi hiyo inatarajiwa kuanza kusilikilizwa Mahakamani leo tarehe 15 Oktoba, 2009 na Mkurugenzi wa Mashtaka amekubaliana na upelekaji wa mashtaka hayo Mahakamani. Waheshimiwa Wajumbe kama sheria inavyohitaji naomba kuwasilisha taarifa hiyo kwenu. Ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kuwasilisha nakala zote za gazeti rasmi la serikali na vijalizo vyake kuanzia tarehe 4 Agosti, 2009.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam.9 ya mwaka 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi juu ya marekebisho ya Mswada wa Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam. 9 ya mwaka 1996 na Kutunga Sheria mpya ya Utalii. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya

upande wa upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam. 9 ya mwaka 1996 na kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar na mambo yanayohusiana nayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Biashara ya Dawa za Kulevya

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kupiga vita uingizwaji na utumiaji wa dawa mbali mbali za kulevya kwa kuwakamata waingizaji na watumiaji wa dawa hizo na kuwafikisha katika vyombo vya sheria, bado kuna wimbi kubwa la uingizwaji na utumiaji wa dawa hizo katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu na kupelekea kuendelea kuathiri nguvu kazi ya Taifa letu.

(a) Mhe. Waziri ni watu wangapi, waliokwishashtakiwa na kuhukumiwa kifungo kuanzia Januari 2009 hadi Septemba 2009?

(b) Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba suala hili, katika nchi yetu, linapungua au kumalizika kabisa ?

(c) Kwa kuwa waathirika wa dawa za kulevya wanaongezeka kila siku. Je Serikali ina mpango wa kuweka kituo cha Tiba kama kile kilichopo nchini Kenya ?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo katika vyombo vya sheria ndani ya kipindi kilichoanzia mwezi wa Januari hadi Septemba, 2009, kesi zilizoendeshwa za madawa ya kulevya ni 132 na kesi 49 zimeshatolewa hukumu na Mahakama Kuu ya Zanzibar ambapo hakuna mtu aliyehukumiwa kifungo.

(b) Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na polisi kuzuia uingizwaji wa madawa hayo kwa kuweka ulinzi madhubuti

katika Viwanja vya Ndege, bandarini na katika bandari bubu, serikali imejipanga vyema kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya ubaya na athari za madawa hayo. Pia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hivi sasa inaandaa mswada wa mabadiliko ya sheria hiyo ili iende na hali halisi ya matukio ya wakati uliopo. Hivi karibuni tutaleta mswada huo katika Baraza lako tukufu.

(c) Serikali inalo lengo kubwa la kuwa na kituo cha tiba kwa ajili ya kushughulikia waathirika wa dawa za kulevya. Mhe. Spika, ili kusaidia kufanikisha lengo hili, juhudi zetu zimeanza kutia sura za matumaini ambapo mfuko wa dharura wa Serikali ya Marekani (*PERPAR*) kupitia *CDC* (*Centre for Disease Control*) umeonesha nia ya kufanikisha ujenzi wa kituo hicho huko Tunguu. Mshauri wa utengenezaji wa michoro kwa ajili ya kituo hicho yumo katika hatua ya mwisho, itakayofuatiwa na hatua ya utengenezaji wa kitaalamu wa viwango vya vifaa vinavyohitajika katika ujenzi huo (*Bill of Quantity*) na hatimaye kutangazwa tenda kwa ajili ya kumpata mkandarasi kwa kazi hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu mama amekiri kwamba kuanzia Januari 2009 hadi Septemba, 2009 kuna kesi 132 ambazo zimepatikana, lakini tayari kesi 49 zimeshatolewa hukumu na hukumu hiyo watu hao wote wameachiwa.

Je, hizo dawa zilipokwishakamatwa na kufanyiwa utafiti zimeonekana sizo au wamesamehewa kwa kuwa bado ni wadogo na ndio kwanza wanaanza biashara?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, hiyo ndio hukumu ya Mahakama na sisi hatuwezi kuingilia.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuanzia Januari hadi Septemba, 2009 kesi 132 ni nyingi mno na ni aibu sana kutopatikana hata moja, hivyo inaelekea katika Tume ya Madawa ya kulevya hakuna uaminifu. Hivyo, Mhe. Spika ingawa tunatengeneza tume nyengine ya kupambana na madawa ya kulevya lakini ikiwa hali ni kama hiyo basi hatufikii lengo, na kama hatufikii lengo basi tume itutengenezee sheria ya usimamizi wa tume hiyo.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, swali la Mhe. Mwakilishi ni gumu kwa sababu ni vigumu sana kulifahamu. Lakini kwa ufupi nilivyofahamu mimi ni kwamba sheria iliyokuwepo kidogo ina mashaka, kwa hivyo tumeifanyia marekebisho ili sheria hii iweze kufanya kazi zake kwa urahisi na kwa wepesi zaidi ukilinganisha na sheria iliyopo hivi sasa ni ngumu kuitekeleza kama walivyosema wenyewe polisi.

Mhe. Spika, kama alivyosema mwakilishi kwamba lengo je litafikiwa ? Ni kwamba matumaini yetu lengo litafikiwa Mhe. Spika, tume itakuwa nzuri, sheria itakuwa nzuri na wote waliohusika watafikishwa katika vyombo vya sheria na hukumu itapatikana bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikauliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali mama ametueleza kwamba kati ya kesi 132 ambazo ziko Mahakamani ni kesi 49 zimetolewa hukumu na watuhumiwa wote wameachiwa.

Kwa kuwa watuhumiwa hawa 49 kuachiwa kwamba wote hawana kesi ya kujibu. Je, serikali imeona kuna kasoro gani za kimashtaka baada ya kuona kuwa kuna kesi nyingi 49 za watuhumiwa wote wameachiliwa wamekuwa hawana hatia. ?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi): Mhe. Spika, katika kesi 132 kesi 49 zimetolewa hukumu na hakuna aliyetiwa hatani hata mmoja. Ni kwamba imeonekana hakuna kasoro yoyote kwani moja ni utekelezaji wa ile sheria iliyokuwepo ni vigumu wakati mwengine kuitekeleza ili kumtia hatiani ndio maana katika kikao hiki tunataka kuleta marekebisho ya sheria hiyo ili iwe rahisi mhusika aweze kutiwa hatiani.

Nam. 18

Uchomaji wa Takataka za Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa taka taka za Hospitali ya Mnazi Mmoja huchomwa karibu na Hospitali hiyo wakati wa usiku na kupelekea harufu ya taka taka hizo kuendelea hadi siku ya pili na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaokwenda hospitalini hapo kupata huduma na kukagua wagonjwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, hali kama hii umewahi kukabiliana nayo.

(b) Huoni kuwa kuna haja ya serikali kuandaa sehemu maalumu iliyokuwa kando na Mji kwa lengo la kuteketeza taka za Hospitali ili kunusuru afya za wananchi kwa kuvuta hewa chafu. ?

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa takataka za Hospitali ya Mnazi Mmoja huchomwa karibu na Hospitali hiyo wakati wa usiku. Hata hivyo, wizara yangu kupitia uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja umechukua hatua mbali mbali za kuwakinga wagonjwa na moshi pamoja na harufu mbaya kama ifuatavyo:-

- Kudhibiti takataka zote zinazotokana na mwili wa binadamu kwa kuzikusanya sehemu maalum bila ya kuzichanganya na takataka nyengine.

- Kutayarisha shimo maalum (*placenta pit*) la kuchomea takataka zinazotokana na mwanadamu ambalo litazuia kusambaza moshi wenye kutoa harufu mbaya.

- Kuhakikisha kuwa takataka zinachomwa kila siku ili kuepusha harufu inayotokana na kukaa kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuandaa sehemu maalum iliyokuwa kando na Mji kwa lengo la kuziteketeza takataka hizo, Wizara yangu imeliona hilo. Hata hivyo, baada ya kuzngumza na wataalamu pamoja na Washirika wetu wa Maendeleo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepewa ushauri ufuatao:-

(i) Mhe. Spika, kwa kuwa hospitali yetu ni ya ngazi ya rufaa ni vigumu kuitenganisha na sehemu ya kuchomea takataka kwani kufanya hivyo itakuwa ni sawa na nyumba iliyojengwa vizuri lakini choo chake kimejengwa mbali na nyumba hiyo. Isipokuwa inatakiwa kuweka tanuri maalum la kisasa ambalo halitaruhusu kutoa harufu wala moshi mkali kutoka nje.

(ii) Mhe. Spika, ili kufanikisha upatikanaji wa tanuri hilo Wizara yangu imeshafanya mazungumzo ya awali na Benki ya Maendeleo ya Afrika na imeonesha nia ya kutupatia mtambo

huo wa kisasa ambao utakuwa hauna matatizo yoyote na tayari maombi yameshapelekwa Makao Makuu ya Benki hiyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu mama amekubali kwamba takataka zinazochomwa hapo wamezitenganisha baina ya taka zinazotokana na binadamu na takataka za matumizi ya vifaa vyao. Ametwambia kwamba katika takataka hizo za binadamu zinatafutiwa sehemu nyengine ambayo ina usalama kuepusha kuenea harufu mbaya katika hospitali hiyo.

Je, pamoja na hayo maandalizi wanayoyaandaa na kwakuwa bado kero hiyo ipo hasa ukilinganisha wagonjwa wetu wa aina mbali mbali wanalala pale hivyo ana mpango gani wa dharura kuhakikisha kwamba panapatikana pahala muafaka kama hawana gari basi watafute gari la kuzolea hizo taka kuzipeleka mbali ili kuinusuru jamii yetu isiumie kutokana na moshi mbaya uliokuwepo pale.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, maombi yake tunayachukua na tutayafanyia kazi, tutalijadili zaidi na kuona kwamba tunalitekeleza vizuri na kuepusha kutupa taka pahala pabaya ili zikaweza kuzagaa. Kwa hivyo, tumelichukua wazo lake hili na tutakaa na wataalamu kulijadili na kumuhakikishia Mheshimiwa kwamba tutafanya kazi nzuri zaidi kuepusha harufu ile.

Nam. 22

Elimu ya Ukimwi Maskulini

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali, na Shirika la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*) imekuwa ikielimisha jamii umuhimu wa Elimu na athari za ngano kwa wanafunzi, ili kuepusha mimba, ndoa za mapema na utoro maskulini. Pia hutoa mafunzo ya stadi za maisha na ukimwi kwa walimu ili kuwakinga na kuwaepusha na maambukizo mapya ya VVU, ikiwa ni pamoja na kuieneza taaluma hiyo kwa wengine.

(a) Je, Mhe. Waziri mafunzo hayo ambayo ni muhimu kwa walimu na wanafunzi yameshatolewa kwa Unguja na Pemba ?

(b) Je, mafunzo hayo kiujumla yameshirikisha walimu wangapi na

wanafunzi wangapi?

(c) Je, ni endelevu au yakupita tu ?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mafunzo haya muhimu kwa wanafunzi na walimu yamekuwa yakitolewa na yanaendelea kutolewa kwa skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

b) Kuanzia Mwaka 2004 hadi hii leo, mafunzo ya stadi za maisha na elimu ya UKIMWI yametolewa kwa jumla ya skuli 120 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, jumla ya skuli 20 za Unguja na Pemba (12 Unguja na 8 Pemba) zimepatiwa mafunzo ya stadi za maisha na UKIMWI kwa walimu na wanafunzi kupitia Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (*ZAC*). Kila skuli ilitoa wanafunzi (50) na walimu (5). Kwa upande wa Unguja skuli zilizopatiwa mafunzo hayo ni Jang'ombe msingi (A), Chumbuni, Bububu Msingi (A) na (B), Kusini, Kiongoni, Kiboje, Ghana, Nungwi, Mkwajuni, Mahonda na Kiwengwa. Skuli za Pemba ni pamoja na Vitongoji, Michakaeni, Kangani Msingi, Mtambile, Ole Msingi, Kangagani Msingi, Finya na Sizini. Wanafunzi waliopatiwa mafunzo haya (waelimishaji rika) wanaendelea kutoa mafunzo hayo kwa wanafunzi wenzao kupitia klabu za afya maskulini.

(c) Mafunzo hayo ni endelevu na siyo ya kupita.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake ya kutafuta wafadhili ili kupunguza mimba za utotoni na UKIMWI.

Mhe. Spika, ni kwamba wanapokuja wafadhili ni sawa kuwapokea na kuifanya hiyo kazi, lakini wao wana lengo kwamba hili tatizo kulipunguza. Hivyo, wizara yake imefanya tasmini kiasi gani wamefanikiwa katika hizo skuli ambazo amezitaja na atatoa mfano wa skuli ngapi zimepunguza mimba za utotoni na pia kuenea kwa taaluma ya UKIMWI.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara yangu imefanya tasmini na kuona kwamba kwa kiasi kikubwa mafunzo haya yamekuwa yakisaidia katika kupunguza wimbi la mimba za utotoni, lakini pia kupunguza wimbi la ongezeko la maradhi ya UKIMWI.

Mhe. Spika, kuhusu skuli ngapi kwa kweli hapa kwa sasa hivi jibu hilo sina lakini akilihitaji nitampatia kwa maandishi.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nawapongeza kwa kutoa taaluma hizi kwa wanafunzi na katika jibu mama ametoa takwimu kwa baadhi ya skuli kwamba tayari zimekwishapata mafunzo hayo.

Kwa kuwa skuli bado ni nyingi je, utaratibu huu utakwenda kwa maskuli yote au zimechaguliwa zile ambazo zimeathirika sana na haya aliyoyazungumza.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu © nimesema kwamba mafunzo haya ni endelevu na sio ya kupitia. Kwa maana hiyo tutaendelea kuifanya kazi hii kadri hali itakavyoruhusu.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi naipongeza serikali kwa kuanzisha masomo haya ya kuzuia maambukizo ya UKIMWI kwani kweli yanafanyika na ushahidi tunauona kwenye baadhi ya maskuli hasa yanayofanya masomo ya ziada pembezoni mle tunakuta mipira ya kondom. Hivyo Mheshimiwa mafunzo haya yana kiwango gani ni hayo hayo matumizi ya kondom au yanaendelea zaidi ya hapo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa ya kusambaa kwa kondom katika maeneo ambayo masomo ya ziada yanafanyika. Mhe. Spika, mafunzo ambayo yanatolewa ni kutoa taaluma jinsi ya kujikinga na siyo tu kutumia kondom lakini kujua kwanza athari ya vitendo viovu ambavyo wanafunzi wanaweza wakajiingiza. Kwa hivyo, wizara yangu haihusishi zaidi matumizi ya kondom lakini wanatoa taaluma ya msingi jinsi gani wanafunzi waweze kujikinga na maradhi, lakini pia vile vile na kuona athari za kupata mimba wakiwa utotoni.

Nam. 1

Kudhibiti Ajali, Barabara ya Mtoni- Kiembe Samaki

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Kwa kuwa skuli nyingi pembezoni mwa barabara ya Mtoni, Daraja Bovu, Amani hadi Kiembe Samaki. Aidha mfano huu huu, Barabara hizi zimezungukwa na masoko mengi ya biashara pamoja na harakati nyingi za watu zinazopelekea kuwepo kwa msongamano mkubwa wa watu hao pamoja na wanafunzi ambao sio tu kwamba mara nyingi huzitumia barabara hizi kwenda na kurudi skuli, lakini pia hukata mara kwa mara katika barabara hizi na hatimaye ajali nyingi huoengezeka.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imeandaa mikakati ipi ya kuwachukulia hatua za kisheria madereva wote wanaokwenda mwendo wa kasi katika barabara hizi.

(b) Kwa kuzingatia ukweli kwamba, ajali nyingi hutokezea katika barabara hizi, je, Mhe. Waziri ni ajali ngapi zinazosababisha vifo hutokezea kwa kila mwaka.

(c) Je, wizara inashirikiana vipi na wizara husika katika kuhakikisha kwamba askari wa usalama barabarani wanatekeleza ipasavyo, majukumu yao ya kusimamia usalama wa watumiaji wa barabara hizi.

(d) Je, Mhe. Waziri kwa kiasi gani wizara yako inafahamu vituo vya Askari wa Usalama barabarani vilivyopo katika bara bara hizi na kwa kiasi gani vinatumika kupunguza wimbi la ajali katika maeneo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake Nambari 1 lenye vifungu a, b, c, na d kama hivi ifuavyo:-

(a) Wizara yangu imeandaa mikakati maalum ya kuwachukulia hatua za kisheria madereva wote wanaokwenda mwendo wa kasi. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kutumia sheria ya usalama barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 inayoliwezesha Jeshi la Polisi kuwa na

uwezo wa kuwakamata na kuwafungulia mashtaka madereva wote wanaokwenda mwendo wa kasi. Aidha, wizara yangu imeunda Bodi ya Usafiri ya Zanzibar ambayo inashughulikia masuala yote ya usafiri barabarani ikiwemo suala la usalama barabarani. Pamoja na mikakati hiyo, wizara yangu pia imeweka alama za usalama barabarani ili kuwaongoza watumiaji wote wa barabara kwa lengo la kupunguza ajali zisizo za lazima.

(b) Kwa mwaka 2008 katika barabara za Mtoni, Daraja Bovu, Amani hadi Kiembesamaki zilitokea ajali tatu zilizosababisha vifo vya watu watatu na kati yao hakukuwa na Mwanafunzi hata mmoja.

(c) Wizara yangu inashirikiana naa Wizara husika kwa mfano, katika Bodi ya Usafiri Barabarani wizara yangu imemteua Kamanda wa Usalama barabarani kuwa ni mjumbe wa Bodi hiyo. Aidha, wizara pia ilishawahi kutoa pikipiki kwa Jeshi la Polisi kwa lengo la kuwafanya askari hao waweze kutekeleza majukumu yao ya kusimamia usalama barabarani vizuri. Mbali na mashirikiano hayo, Idara ya Usafiri na Leseni na Jeshi la Polishi kupitia Askari wa Usalama Barabarani huwa na mpango wa mkakati kupambana na kufanya ukaguzi wa barabarani.

(d) Wizara yangu inavifahamu vituo viwili vya askari wa usalama barabarani viliopo katika barabara ya Mtoni, Daraja Bovu, Amani hadi Kiembesamaki, kimoja kikiwa Mwanakwerekwe na cha pili kikiwa Chumbuni.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Awali ya yote nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa aliyoifanya katika Skuli ya Chumbuni kwa kuweka kipunguza mwendo ambacho kinasababisha kupunguza ajali za wanafunzi na wananchi wanaotumia barabara ile.

Je, swali langu ni kwamba, katika barabara ya Mwanakwerekwe penye Skuli ya Mwanakwerekwe ambayo inatumiwa na wanafunzi pamoja na wananchi wanaotumia barabara ile, ikiwemo pia Skuli ya Muungano na Sebleni kwa barabara inayotokea Amani na barabara ya Uwanja wa Denja. Hii katayarisha marekebisho gani ya kuweka kipunguza mwendo kama kilichoko barabara ya Chumbuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa kutupongeza katika kufanya kazi zetu vizuri, lakini pia ushauri wake tunaupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, na mimi niipongeze serikali yetu kwa juhudi zake nzuri za kuweka miundombinu ya barabara na mambo mengineyo, lakini tunazungumzia barabara katika suala hili. Kwa asilimia kubwa sana Mhe. Spika, wananchi wanazitumia barabara hizi na madereva kwa ufasaha kutokana na mwendo mzuri wanavyotaka bila ya kuzingatia usalama barabarani.

(a) Je, kwa kuwa mwendo wa kasi ni kosa na kwa kuwa katika maeneo yetu mengi alama za barabarani hamna, kwa mfano katika skuli zetu kama ya Muungano, Sebleni na nyenginezo hakuna matuta, lakini pia hakuna alama zinazoonesha kwamba nenda kwa usalama au zebra inayoonesha kukatisha barabara. Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha angalau tunapata alama hizo na zebra ya kuwa ni usalama mmoja wapo wa kuweza kuwanusuru wanafunzi na watu wetu.

(b) kwa kuwa watu wetu hasa siku za sala ya Ijumaa au siku za sala za Iddi, huwa wanakusanyika katika misikiti yetu ya barabarani kwa mfano, Msikiti wa Kwaboko na barabara sasa hivi ni nzuri madereva wanakwenda wanavyotaka, eneo hili pia hakuna alama ya barabarani wala tuta linaloonesha ishara au zebra na madereva kuregeza mwendo ili watu wakatishe barabara, au Msikiti wa Mwembemimba halkadhalika. Mhe. Waziri atachukua hatua gani kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapatiwa vitu hivyo nilivyovieleza ili kunusuru maisha ya wazee wetu wanaokwenda kusali katika misikiti hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ningeliomba pia nisaidie kidogo kuhusu swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na taasisi nyengine kama Manispaa wanajitahidi sana kuweka usalama barabarani, tunajitahidi kuweka alama barabarani, lakini tatizo moja ambalo linatukabili ni kuibiwa kwa alama hizi na watu ambao sijui kwa nia gani lakini wanaziiba. Kwa hivyo, tunatoa wito kwamba wananchi wasiibe vile viashiria vya usalama barabarani.

Kwa upande wa *zebra cross* Manispaa ambao ndio wanahusika nazo wameanza kuweka katikati ya mji, lakini tutawashauri waendelee na maeneo ya ng'ambu ili kuondoa tatizo hili.

Kuhusu matuta Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo lina mjadala mrefu, sisi watu wa Wizara ya Mawasiliano hatupendi sana kila eneo kuweka matuta. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali kama tutaweka huko alikosema Mhe. Ali Denge, Mikunguni, Muungano, Kwaboko inawezekana baadae nchi yetu ikawa imejaa matuta. Inasaidia kupunguza ajali, lakini upande wa pili waweka vitega uchumi na watu wengine wanaumia sana. Kwa sababu kama gari la makontena lenye tani 40 likipanda tuta na kushuka kila eneo, basi kuna hatari mizigo yenyewe kuanguka lakini pia hasara kwa wenye magari.

Tunajaribu sana kuangalia pande zote mbili za shilingi, lakini pale ambapo tunahisi kuna ulazima wa kuweka matuta tutaweka na tutaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi kila ambaye anaona pako sehemu inastahili. Lakini hatupendi kuweka matuta kila sehemu kwa sababu inawezekana madhara yake kwa upande wa pili ikawa makubwa zaidi kuliko vile ambavyo tunayatarajia.

Mhe. Spika, nilitaka kuchangia hayo tu.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano naomba kuuliza swali la nyongeza. kwanza na mimi niungane na yeye kuwashukuru sana Jeshi la Polisi kuhusu kuzuia na kuelekeza namna ya kupunguza mwendo kwa madereva wetu.

Katika suala ambalo nataka kuuliza ni kwamba mwaka juzi Mhe. Waziri alipoulizwa swali kuhusu matuta alisema sheria hairuhusu, lakini leo anasema ni makubaliano. Lakini sheria hiyo hiyo kama utapita barabara ya Kinyasini/Dunga ina matuta mengi tu bila ya kuwafikiria wafanyabiashara na makontena. Hivyo, maeneo ambayo yametajwa yenye harakati nyingi kama skuli na masokoni, wanapoleta mapendekezo wananchi ya kujengewa matuta nini tatizo? Ni gharama ya lami ya kuwekea matuta au tatizo sheria?

Kama tatizo ni lami na mambo mengine, wangeshajiishwa wananchi ili wakaona kwamba wanaweka matuta barabarani. Hivyo Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuweka matuta barabarani hasa kwa madereva wa sasa na gari zilivyokuwa nyingi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, nafikiri nilisema kwamba suala hili linataka mjadala wa kina. Kwa sababu matuta tunaweka barabarani lakini tunaangalia kila aina ya usalama wa barabarani ndio tuweke matuta. Kwa bahati mbaya sana katika maeneo mengine likiwemo la Mhe. Ame Mati wananchi wake wanaweka matuta wenyewe bila ya kuishauri serikali. Hivi juzi mimi mwenyewe niliagiza waende watu wangu wakaliondoe hilo tuta kwa polisi barabara mpya ya Mshelishelini kwenda Pwani Mchangani,

wananchi wameweka tuta bila kuishauri serikali. Lakini sisi tumekwenda kuliondoa kwa sababu sio sheria, walikuwa wao waje serikalini, wizarani halafu tukubaliane kuweka hilo tuta.

Mhe. Spika: Kabla ya kuendelea sijui kama waliona ndio msaada kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi au vipi. (*Kicheko*)

Nam. 25

Uvamizi wa Kiwanja cha Shirika la Bima Pemba

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Katika kujipanga vizuri, Shirika la Bima hivi sasa wanajenga jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Ofisi ya Makao Makuu hapo Maisara kwa Unguja lakini pia kwa Pemba Afisi imejiandaa katika mipango yao ya mwaka huu kujega na wao Afisi yao mpya katika eneo la Tibirinzi ambayo michoro tayari bado kutangaza tenda na kuanza ujenzi.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kama kiwanja kilichokua ijengwe afisi hiyo Tibirinzi Pemba kimevamiwa na Afisi ya Mwanasheria na weshaanza kujenga fensi.

(b) Kama ndio, Je, Wizara imechukua hatua gani ya kusaidia ili Afisi ya Bima, Pemba ipate kiwanja chake.

(c) Je, Mhe. Waziri, inakuwaje Taasisi inayohusika kutoa Hati ya kiwanja kimoja kwa mamlaka mbili tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Shirika la Bima tayari limeshaanza ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu yake hapo Maisara, tafauti na ilivyoelezwa na Mhe. Mwakilishi. Jengo hilo linatarajiwa kuwa na ghorofa nne sio ghorofa moja tu, ni *sky scraper* hiyo inakuja. Ujenzi huo utafanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza itakuwa ni ujenzi wa ghororfa mbili na baadae tutamalizia ghorofa mbili nyengine.

Kwa upande wa Pemba lengo ni kujenga jengo lake la ofisi hapo Chake Chake. Mhe. Spika, si kweli kwamba kiwanja cha Shirika la Bima Chake Chake limevamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ikiwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu itavamia itakuwa hatari tena. Kilichojitokeza ni utata juu ya mmiliki halali wa kiwanja hicho baina ya taasisi hizo za serikali. Haikuwahi kutolewa hati moja kwa mamlaka hizi mbili tofauti.

Mhe. Spika, tatizo hili tayari limeshashughulikiwa ipasavyo kwa kushirikiana na wizara zetu hizi mbili, Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ambayo inashughulikia na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, nathubutu kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba ufumbuzi muafaka tayari umeshapatikana kwa Shirika la Bima kupatiwa kiwanja chengine. Taarifa rasmi niliyoipata siku mbili tatu zilizopita ni kwamba kiwanja kipya kwa Shirika la Bima kimeshapatikana na wanatarajiwa kukabidhiwa hii leo huko Pemba. Ahsante.

Nam. 7

Ujenzi wa Bustani katika Maeneo ya Makaazi ya Wananchi

Mhe. Ali Denge Makame (Kny. Mhe. Ame Ussi Juma) - Aliuliza:

Tunaipongeza Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kuruhusu na hatimae kupatikana Mfadhili wa ukarabati wa Bustani ya Forodhani iliyofunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, Dr. Amani Abeid Karume, August 2009.

(a) Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na bustani katika maeneo ya Ng'ambu, Je, Wizara imeandaa mikakati gani kuhakikisha kwamba Bustani kama ilivyo Forodhani, zinajengwa katika maeneo ya Ng'ambu.

(b) Kwa kuzingatia nchi ya India imeendelea katika ujenzi wa bustani maeneo mengi ya mjini na vijijini. Je, serikali haioni ipo haja ya kuiga mfano huu.

(c) Je, kwa nini serikali haikuandaa ujenzi wa bustani maeneo ya Tunguu na maeneo mengine yanayokatwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makaazi.

(d) Kwa kuwa utamaduni huu wa kuwa na maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya Bustani haujaimarika nchini, Je, Wizara haioni kwamba

kuna haja ya kuanzishwa na hatimae kuimarishwa utaratibu huu kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napeda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu a, b, c na d kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kupokea pongezi za Mhe. Mwakilishi kuhusu ukarabati wa bustani ya Forodhani iliyofunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, Dr. Amani Abeid Karume, Agosti 2009. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba, wizara yangu itaweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa bustani hiyo ili iendelee kuwa na hadhi nzuri iliyopo hivi sasa.

(a) Mhe. Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa bustani pamoja na huduma nyengine za kijamii katika maeneo ya Ng'ambo, wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, pamoja na serikali kwa ujumla, inaandaa mpango maalum wa kuimarisha huduma katika Miji (*Zanzibar Urban Services Programme*). Mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia na miongoni mwa huduma hizo ni uimarishaji wa bustani, viwanja vya michezo, burudani na kadhalika. Hivi sasa Mtaalamu Mshauri wa Mradi huo ameanza kuandaa ripoti ya awali ya mpango huo ambayo itaainisha matatizo mbali mbali yanayohitaji kushughulikiwa katika Mji wa Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu inakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja ya kuiga na kujifunza mfano wa India pamoja na nchi nyengine katika maeneo ya miji na vijiji. Juhudi nilizozieleza hapo juu zina lengo la kuweka bustani kwa mujibu wa mazingira yetu yatakavyoruhusu.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu katika maeneo yote mapya likiwemo eneo la Tunguu ambalo hukatwa viwanja vya makaazi na kugaiwa kwa wananchi, maeneo maalum yamekuwa yakitengwa kwa ajili ya bustani na viwanja vya michezo.

(d) Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba utamaduni wa kuwa na maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya bustani tunao. Tatizo liliopo ni juu ya kuyaendeleza na kuyahifadhi maeneo hayo. Wizara yangu inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa kwamba kuna haja kubwa ya kuimarishwa kwa utaratibu huu kwa maslahi ya taifa. Wizara yangu itashirikiana na taasisi husika

kuhakikisha kwamba maeneo ya bustani yanawekwa na kutunzwa vizuri.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika mandhari ya mji wetu hasa sehemu ya Forodhani harakati ya bustani yetu ya Forodhani imetia sura mpya katika mji wetu na wananchi pamoja na wageni wanafurahika kwenda kuangalia au kutembelea katika mazingira ya kisasa kabisa.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi husema katika juhudi hizo tusielekee mjini bali tuelekee na ng'ambu. Kwa mfano kuna bustani zetu nyingi za ng'ambu zimewekwa bila ya kazi yoyote na baada ya muda mfupi huenda kukawekwa makontena ya biashara na kukosa hadhi ya bustani zenyewe.

Kwa mfano Mhe. Spika, bustani yetu moja ya *Jamhuri Garden* ambapo wanafunzi wengi wanafaidika kupumzika na kufanya tathmini ya masomo yao, lakini hakuna mwelekeo wa bustani hasa ambao unaelekea katika mwelekeo wa kisasa. Bustani ya pili ni ya Michenzani, ambapo pale palikuwa na makontena yakahamishwa ili kutoa nafasi kutengeneza bustani ya kisasa ambapo wananchi wetu watakwenda kupumzika pale bila ya bughudha. Kwa sababu anayekataa kwenda Forodhani atakuwepo pale kati kati ya mji.

Je, Mhe. Waziri pamoja na hizo juhudi za tathmini zinazofanywa, lakini kwa kuwa haya maeneo mawili tunayo mikononi wizara ina harakati gani za kuyafanyia utafiti wa haraka haraka ili yaanze kazi hiyo kwa manufaa ya watu wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli tunayo bustani yetu ya *Jamhuri Garden* ambayo ni nzuri, si nzuri kama ile ya Forodhani, lakini ni kweli bustani ile ikitengenezwa inaweza kuwa nzuri kuliko ya Forodhani, itakosa ile mandhari ya bahari tu. Lakini pia kwa kutumia wataalamu wetu tunaweza tukatengeneza ile mandhari ya bahari mle mle ndani.

Jengine ni kwamba kweli Michenzani tulikuwa na eneo lile ambalo lilikuwa na bustani, lakini sijui kwa nini bustani ile sasa hivi imekufa haipo. Wakati nikijibu swali mama nilisema tayari tunae mtaalamu hapa na karibuni atatoa taarifa yake ikiainisha maeneo mbali mbali ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Naamini kwamba ripoti hiyo itahusisha *Jamhuri Garden*, Michenzani na maeneo mengine.

Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba sio Michenzani tu hata pale *round about* Michenzani, tulikuwa na bwawa la maji linaleta mandhari nzuri ya mji wa

Unguja, lakini nayo haipo. Inasikitisha kwamba tunaanzisha vitu halafu sisi wenyewe tunaviuwa na ndio maana wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ hili tumeliona na kwa mahimizo yenu wawakilishi tutayafanyia kazi ili kuona mji wa Zanzibar kuanzia Mji Mkongwe hadi ng'ambu unapendeza na kuwa na bustani ambazo zitatoa nafasi kwa vijana wetu kwenda kupumzika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. kwanza naipongeza serikali kupitia wizara yake Mhe. Naibu Waziri kwa kutengeneza bustani ile ya Forodhani.

Tunasikia hivi karibuni wamekamatwa watu watatu wanataka kufanya uharibifu katika bustani ile. Je, hili ni kweli.

Katika mji wetu wote ukiegesha gari unalipa sh. 250, lakini Forodhani sh. 1,000. je, ni kwa sababu ya uzuri wa ile bustani au kuna sababu nyengine ya msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, sina taarifa ya kukamatwa kwa watu hao, lakini kama taarifa hiyo ni ya kweli siwezi kujua watu hao walikuwa na dhamira gani. Lakini kama kutakuwa na watu ambao wamekamatwa na walikuwa na dhamira ya kuharibu ile bustani hawa sijui adhabu yao iwe ipi, lakini kwa kweli tuwaachie vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, ni kweli maeneo mengi kuna sehemu ambazo watu wanaegesha gari wanalipa, nadhani sh. 500 lakini Forodhani pale ni sh. 1,000. sina hakika wenzetu wa Manispaa wamechukua kigezo gani, lakini nadhani eneo lile kwa kuweka kiwango hicho itasaidia kupunguza ule msongamano wa magari na hivyo kutoa fursa pia kwa bustani yetu kuwa haipati ule uharibifu ambao usiokuwa na sababu.

Nam. 31

Uharibifu wa Mazingira

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:

Katika Kisiwa cha Unguja kuna uharibifu mkubwa wa mazingira kwa uchimbaji mchanga katika maeneo mbali mbali kwa Wilaya ya Magharibi na Kaskazini B, lakini pia kumezuka wimbi kubwa la uharibifu wa mazingira katika kisiwa cha Pemba kwa uchimbaji wa matofali ya mawe ya jasi hasa katika Mkoa wa Kaskazini na kundi kubwa la watu wamejiajiri katika kazi hiyo ili kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

(a) Je, Mhe. Waziri katika uchimbaji huu wa matofali ya mawe pana kibali chochote kinachotolewa.

(b) Kwa kuwa katika uchimbaji mchango Serikali ya Wilaya na Halmashauri huwa wanakusanya kodi kwa kila gari ya mchanga je na haya matofali ni kwa moja moja au kwa gari/shehena.

(c) Kwa kuwa kazi hiyo inaharibu mazingira Je, kuna Taaluma inayotolewa kwa watu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, uchimbaji wa mchanga unafanyika katika mashamba ya watu binafsi ambapo hupata vibali kutoka Halmashauri ya Wilaya husika. Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu hutoza ada ya ushuru wa usafirishaji.

(b) Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya hukusanya kodi kwa kila tani ya mchanga.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu inafahamu kwamba uchimbaji wa mchanga na matofali ya mawe ya jasi unaharibu mazingira. Hivyo wizara inaendeleza utaratibu wa kutoa elimu ya mazingira kwa wachimbaji na wenye mashamba ili kupunguza uharibifu wa mazingira na kuyaendeleza tena maeneo yaliyoathirika. Mhe. Spika, wizara yangu pia inamuomba Mhe. Mwakilishi kuwa jimbo lake pia linahusika na uharibifu mkubwa, basi aanzishe ile kamati ambayo ya mazingira ili tuweze kushirikiana na Wizara yetu ya Kilimo ili kuliondoa suala hili zaidi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mwenye shamba hutoa shamba lake kwa kupata neema ya kupata fedha kwa ajili ya kujihudumia yeye na familia yake inayomuhusu. Lakini pia azma kubwa ya serikali ni kwamba, huduma ile inayotolewa katika shamba lile kuwasaidia wananchi katika utengenezaji wa nyumba zao na mambo mengineyo yanayohitajika.

Je, kwa kuwa kuna elimu ya taaluma ambapo hutolewa taaluma mbali mbali na Mhe. Naibu Waziri kasema kwamba taaluma hiyo hutolewa kwa madereva na

wenye mashamba hayo. Je, taaluma ya kupanga miti kwa nini hawaelekezi huko ili wananchi wale wanaolimiwa mashamba yao wapande miti halafu ardhi ile iwe nyingi zaidi kama ilivyokuwa zamani yaani ijirudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nataka niwahakikishie waheshimiwa kwamba elimu tunayoitoa kwa wenye mashamba kwanza mashamba yale ambayo yanachimbwa mchanga tunataka kwanza kiende kima cha mita tatu la mwanzo, la pili baadae tunarejesha miti. Lakini moja katika tatizo linalotupata katika mashamba yetu kwanza kuna wizi mkubwa nyakati za usiku, ndipo niliposema pamoja na kumuomba Mhe. Ali Abdalla Ali lakini naliomba Baraza zima tushirikiane katika kuokoa nchi yetu. Kwa sababu suala hili linatuhusu sote.

Si vibaya kwamba tunauliza hapa Barazani, lakini naomba tushirikiane zaidi nje ya Baraza. Kwa sababu uharibifu wa mazingira jambo hili litapotokezea au tukimaliza hiki kisiwa tutaangamia sote sio kama itaangamia Wizara ya Kilimo peke yake.

Mhe. Spika: Kabla ya kuendelea kuna matangazo mawili, nimeombwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwamba mara baada ya masuala haya ambayo tumeshamaliza, kamati itaendelae na shughuli yake ya kupitia ule mswada unaohusu madawa ya kulevya hapa juu kuanzia punde hivi tukiendelea na shughuli nyengine. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati usiwe na wasi wasi Mhe. Abubakar Khamis Bakary amenihakikishia kwamba atahudhuria kamati hapo na atakuja na yeye huko.

Vile vile ikifika saa saba pale tunapoondoka kwenye shughuli zetu, Kamati ya Fedha na Uchumi nayo itakutana kuendelea na Mswada wa Usafishaji wa Fedha Haramu. Kwa hivyo, wajumbe wote wa kamati hizo mbili kwa saa hizo ambazo nimezieleza watakwenda kwa ajili ya kuendelea na shughuli za miswada. Nawashukuru sana.

Shughuli za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam. 9 ya 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar

(Kusomwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na uongozi wa Baraza kwa kuipanga wizara yangu kuwa ya kwanza kuwasilisha Mswada wa Sheria katika Mkutano huu wa 17 na katika Kikao cha Kwanza leo tarehe 15 Oktoba, 2009.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo naomba sasa nichukue nafasi kuwasilisha Mswada wa Sheria kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Zanzibar imo katika mageuzi ya kiuchumi ambayo yanalenga kukuza uchumi wake na kupunguza umaskini. Ili mafanikio yapatikane kwa haraka zinahitajika sekta nyingi zichangie katika ukuaji wa uchumi badala ya kutegemea sekta chache za biashara na kilimo kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Moja kati ya sekta ambayo imeonesha matumaini makubwa katika kuchangia ukuaji wa uchumi kwa miaka ya karibuni kutoa ajira na kuongeza kipato nchini ni hii sekta ya utalii.

Mipango yote ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar imetambua mchango mkubwa wa sekta ya huduma hasa utalii. Aidha, katika mpango mkuu wa muda mrefu ujulikanao kama dira ya 2020 na mipango ya muda wa kati hasa MKUZA na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala imeweka mkazo katika uimarishaji wa sekta hii.

Mhe. Spika, biashara ya utalii kwa hapa Zanzibar inasimamiwa na Sheria Nam. 9 ya mwaka 1996. Baada ya kuitekeleza sheria hiyo kwa muda mrefu kubadilika kwa hali ya utalii na usimamizi wake pamoja na mipango ya kitaifa ya kuondoa umaskini na kukuza uchumi, imeonekana kuwa ipo haja ya kuifanyia mabadiliko kwa kutunga sheria mpya ya utalii ya Zanzibar itakayoendana na mahitaji mapya ya uendeshaji wa biashara hii na usimamizi wake kwa ujumla.

Ili kufikia azma hiyo, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji imeandaa rasimu ya mswada wa sheria hii baada ya kukamilisha taratibu za kutunga sheria tuweze kupata sheria hiyo mpya itakayoweka taratibu bora zaidi za usimamizi wa sekta hii.

Mhe. Spika, kutokana na kukua kwa kasi kwa sekta ya utalii na tegemeo la kuwa iwe sekta kiongozi katika kuinua uchumi wetu, imeonekana wazi kwamba ipo haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria Nam. 9 ya Utalii Zanzibar ya mwaka 1996. Maeneo ambayo yalionekana kuwa na kasoro ni kama yafuatayo.

Muundo wa Uongozi wa Kamisheni

Kamisheni chini ya sheria iliopo sasa uongozi wake upo chini ya Mwenyekiti ambaye hana Bodi ya Wakurugenzi, Katibu Mtendaji akisaidiwa na Wakurugenzi wawili. Hali hii haileti mtiririko mzuri wa usimamizi wa chombo

kikubwa na muhimu kama hiki. Ingawaje Waziri mhusika alipewa uwezo wa kuunda Bodi ya Ushauri, lakini hata kama ingeundwa basi isingekuwa na nguvu kwani ingekuwa ni ya ushauri tu.

Mipango ya Kazi na Ripoti

Sheria haikuweka wazi majukumu ya mabadiliko na utekelezaji wa mipango ya Kamisheni na utoaji wa ripoti za utekelezaji.

Mfumo wa Fedha

Katika mfumo wa sasa Kamisheni inaendesha bajeti yake kama Idara ya Serikali badala ya mfumo wa mamlaka inayojitegemea, hivyo kuathiri kufanya maamuzi ya haraka wakati kunapojitokeza haja ya kufuatilia au kukabili ushindani uliopo duniani sasa katika biashara hii.

Sera ya Utalii

Sera ya Utalii inayotumika sasa ni ya mwaka 2004 wakati sheria yake ni ya mwaka 1996 na ilipaswa kuwa na sheria ya karibuni kuliko sera ili sheria itoe nguvu za kiutekelezaji wa sera hiyo.

Mabadiliko ya Kiwakati

Sekta ya Utalii inakua na kubadilika kwa haraka sana. Aidha, mfumo na uendeshaji, taratibu za kazi, huduma mpya zinazojitokeza katika utalii na ushindani duniani ni miongoni mwa mambo ambayo katika sheria ya sasa yanaanza kupitwa na wakati.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia upungufu uliojitokeza katika sheria ya sasa, haja ya kuifanyia marekebisho ni jambo la busara na la lazima. Kutokana na wingi wa maeneo yanayohitajika kufanyiwa marekebisho tumeona tupendekeze kutungwa kwa sheria mpya hasa kwa vile sekta hii ni muhimu katika mipango ya kukuza uchumi wetu na inamgusa kila mtu awe mwenyeji au mgeni.

Mhe. Spika, sekta ya utalii inawagusa wadau mbali mbali katika ngazi ya taifa, wilaya, halmashauri, shehia na kadhalika, kwa upande mmoja. Wawekezaji katika maeneo ya mahoteli, mikahawa, watembeza wageni, usafirishaji na michezo kwa upande wa pili. Wote hawa wanahitaji sheria na usimamizi ambao utatoa fursa sawa kuweka mazingira mazuri katika kuendeleza biashara hizo.

Pamoja na mambo hayo, Sera ya Utalii ya Mwaka 2004, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Zanzibar na mfumo mzima wa Kiutawala na Usimamizi wa Kamisheni umezingatiwa katika kuandaa rasimu hii ya mswada wa sheria.

Katika maandalizi ya mswada huu kulifanyika kikao cha pamoja cha wadau mbali mbali wa sekta binafsi na umma kwa ajili ya kupata maoni yao. Maoni yaliyotolewa katika kikao hicho yamejumuishwa katika rasimu hii ikiwa ni pamoja na nyongeza ya Majukumu ya Kamisheni, masuala ya Utalii wa Kimazingira na Utalii Endelevu. Pia waraka huu umezingatia mipango ya sera za ndani, taratibu za makubaliano ya kimataifa, kikanda kama vile Sera za Taratibu za Jumuia ya Kimataifa ya Utalii Duniani, Jumuia ya Afrika Mashariki na Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mhe. Spika, madhumuni ya maelezo haya niliyoyatoa ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Utalii itakayosimamia majukumu ya Kamisheni ya Utalii kwa mujibu wa mahitaji ya sasa na uzito wa sekta ya utalii kwa uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria mpya ya Utalii umegawika katika sehemu 6 na una jumla ya vifungu 32. Sehemu ya 1 ya mswada inaeleza mambo ya awali ambayo ni jina, muda wa kuanza kutumika na tafsiri ya maneno mbali mbali kama yalivyotumika katika mswada huu.

Sehemu ya 2 inaweka misingi ya kiutawala ya kamisheni ikijumuisha Muundo wa Bodi ya Wakurugenzi, Miko ya Kazi na Uendeshaji wa Shughuli za Kamisheni na Upangaji wa Mipango kazi. Aidha, sehemu hii pia inaweka viongozi watendaji wakuu na watumishi wengine wa taasisi hiyo.

Sehemu ya 3 ya mswada inazungumzia masuala ya fedha na usimamizi wake, hasa Mfuko wa Kamisheni, Vyanzo vya Fedha za Kamisheni, Utayarishaji wa Makisio na Utoaji wa Ripoti.

Sehemu ya 4 ya mswada huu inaweka taratibu na masharti ya leseni kwa wenye kuendesha biashara zinazohusiana na utalii.

Sehemu ya 5 ya mswada inazungumzia majukumu na wajibu wa waendesha biashara ya utalii ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu za biashara zao zinazohitajika na upatikanaji wake. Aidha, imeweka utaratibu maalum kwa baadhi ya aina za biashara.

Sehemu ya 6 inazungumzia mambo ya jumla na katika usimamizi wa sheria. Maeneo yaliyomo katika sehemu hii ni biashara maalum zilizotengwa kwa

Wazanzibari. Hatua za dharura kwa wasiofuata masharti ya sheria, Uundwaji wa Jumuia ya Waendeshaji biashara za utalii, Majukumu ya Kijamii kwa wenye biashara za utalii, Makosa na Adhabu, Haki ya kukata rufaa, Kumaliza kosa kwa makubaliano, Utungaji wa Kanuni na Kufutwa kwa Sheria inayotumika sasa.

Mhe. Spika, kutokana na mwelekeo na umuhimu wa Sekta ya Utalii kwa uchumi na maendeleo ya Zanzibar kwa ujumla wake, imeonekana kuna haja kubwa ya kubadilisha Sheria ya Kuendeleza Utalii ya mwaka 1996 ili iendane na mipango na sera zilizopo sasa katika kuendeleza Sekta ya Utalii.

Mhe. Spika, kwa misingi hiyo, wizara inaamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wataichangia ipasavyo rasimu ya mswada huu wa Sheria ya Utalii na kufanya marekebisho pale inapojitokeza na baadaye kuupitisha na kuupeleka katika ngazi za juu kwa kutiwa saini na kuwa sheria ili iweze kutumika kwa manufaa na maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti ya Kamati ya Fedha Uchumi): Mhe. Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kuendelea kuwa hai na tukiwa wazima wa afya. Pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kwanza ili kutoa maoni ya Kamati yangu ya Fedha na Uchumi juu ya Marekebisho ya Mswada wa Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam. 9 ya Mwaka 1996 na Kutunga Sheria Mpya ya Utalii Zanzibar.

Mhe. Spika, niruhusu nimpongeze na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa uwasilishaji wake mzuri mbele ya Kamati lakini hata leo mbele ya Baraza lako Tukufu. Ameonesha ni kwa kiasi gani amekuwa makini na bidii katika kazi zake. Pia niwapongeze watumishi wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa jinsi wanavyompa mashirikiano ya dhati na kumuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, mbali na pongezi hizo, lakini pia tunampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuwashirikisha wadau wa utalii (sekta binafsi) tangu katika hatua za awali za matayarisho ya Mswada huu hadi leo hii tunaujadili katika Baraza lako tukufu.

Kwa kweli Mhe. Spika huu ni mfano mzuri wa kuigwa katika ile dhana ya utekelezaji wa sera ya Serikali ya kuishirikisha sekta binafsi katika mipango

yake ya maendeleo *(Public Private Partnership - P.P.P)*

Mhe. Spika, tunazitaka Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii ya Fedha na Uchumi kuiga mfano kama huu wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji wakati wanapoandaa miswada mbali mbali ya sheria, kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia sana katika utekelezaji wa sheria husika kwa vile wadau hao (sekta binafsi) watakuwa ni sehemu ya sheria iliyotungwa.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii uliyonipa niwashukuru Wajumbe wenzangu niliokuwa nao kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Assaa Othman Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ashura Abeid Faraji	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	-	Mjumbe
7.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
8.	Mhe. Said Khelef Ali	-	Mjumbe
9.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	Mjumbe
10.	Ndg. Amour Moh'd Amour	-	Katibu

Mhe. Spika, kila mmoja wetu anafahamu namna Sekta ya Utalii inavyokuwa kwa kasi kubwa duniani na Zanzibar ikiwa ni sehemu mojawapo. Aidha, katika kuinua maisha ya wananchi wetu kiuchumi muelekeo wetu tunaiangalia sekta hii ya utalii kama mkombozi wetu.

Ni dhahiri kama miundo mbinu ya kuusimamisha utalii itasimama kisawasawa basi biashara itakua kwa kiasi kikubwa, kilimo nacho kitakuwa na nafasi yake kutokana na kuwepo kwa soko la bidhaa.

Halikadhalika miundo mbinu mingine ya usafiri na usafirishaji nayo itaimarika.

Mhe. Spika, ili tufikie huko tunakolenga, suala la mabadilko katika mipango ya sheria zetu ni muhimu ili ziendane na mazingira halisi yaliyopo. Hatuwezi kubaki na sheria na taratibu hizi hizi tulizonazo wakati mazingira yenyewe yanabadilika. Mabadiliko haya Mhe. Spika, yahusishe maeneo yote na kwa maana hiyo miongozo ya Sheria, Kanuni na Utawala ilenge katika kuwagusa kila mdau kwa nafasi yake.

Mhe. Spika, tunaelewa fika kwamba wahusika wa kuimarisha utalii si Kamisheni ya Utalii peke yake au Wizara inayohusika na Utalii tu, bali ni mtiririko unaowashirikisha wananchi katika sekta tofauti. Hii ni sekta mtambuka. Utalii hauwi tu kwa sababu ya maeneo na uzuri wa fukwe zetu au magofu na mambo ya kale ya kihistoria tuliyonayo au kuwepo kwa mji mkongwe, kimapunju au mashamba ya viungo na viungo vyenyewe bali unahitaji kwanza watu wa kuyaratibu na taratibu ndizo zitakazoongozwa na sheria zetu.

Mhe. Spika, tusipokuwa na miongozo madhubuti basi ile dhana tuliyonayo ya kwamba utalii unaweza ukamkomboa mwananchi wetu inaweza ikageuka vyenginevyo na badala yake watu wachache tu ndio watakaofaidika.

Mhe. Spika, ni faraja kubwa kwamba Serikali imeweza kugundua mapungufu yaliyomo katika Sheria Nam. 9 ya Utalii Zanzibar ya mwaka 1996 ambapo muundo wa Uongozi wa Kamisheni, masuala ya mfumo wa fedha, sera yenyewe ya Utalii, mipango ya kazi na ripoti pamoja na mabadiliko ya kiwakati ni mambo ambayo kwenye sheria hii yalikuwa hayakukaa sawa sawa.

Mhe. Spika, kumekuwa na manung'uniko mengi kutoka kwa wananchi wetu juu ya kazi ambazo zinafanywa na watu ambao si raia wa Tanzania au si Wazanzibari. Kazi ambazo watu wetu wanaweza kuzifanya na ni haki yao kuzifanya, vyenginevyo watakuwa wanakosa kufaidika na ile azma ya Serikali juu ya kuwepo kwa sera hii ya Utalii.

Kwa mfano biashara ya kutembeza watalii, chini ya sheria hii inayopendekezwa. Kazi hii imetajwa wazi wazi kwamba ifanywe na Wazanzibari. Hii pia tumependekeza wahusishe waongozaji watalii. Maamuzi haya ni ya busara kwa sababu mbili kubwa. Kwanza ni lengo la kuwapatia ajira vijana wetu, lakini la pili ni kuhakikisha kwamba historia yetu haipotoshwi kwani vijana hao watakuwa wanatoa maelezo katika kile wanachokielewa. Lakini pia watakuwa walimu wazuri wanaoweza kuulinda utamaduni na silka zetu za Kizanzibari.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii ina wajibu mkubwa wa kuwatambua na kuwaelimisha wale wote ambao itawapa leseni za biashara hizi za utalii. Lakini kuwa makini huko kuende sambamba na kuondoa urasimu wa upatikanaji wa leseni hizo.

Mhe. Spika, lengo la kuwa na utalii wenye kuendana na wakati pamoja na mambo mengine ni jambo muhimu sana. Nchi yetu hutegemea sana mapato yanayotokana na utalii kwa ajili ya maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na huduma za kijamii.

Ni kweli kuna baadhi ya wafanyabiashara wa utalii hukosa uaminifu na kuangalia zaidi faida kuliko kuangalia mambo mengine na hivyo huwa na ujanja ujanja wa kukwepa kulipa kodi. Uwekezaji wa kumbukumbu za wageni wanaoingia nchini usio sahihi unaofanywa na wamiliki wa mahoteli na nyumba za kulala wageni huchangia kwa kiasi kikubwa kuikosesha serikali mapato mengi.

Aidha, kwa yale mahoteli yanayowalipisha wageni wao moja kwa moja nje ya nchi *(Package Tours)* yaangaliwe kwa makini kwani huitumia fursa hii vibaya.

Mhe. Spika, ni lazima tuwe makini katika kusimamia upatikanaji huu wa taarifa muhimu tena ziwe zimekamilika. Si vibaya hata kidogo kwa taarifa ya mgeni kuhusisha hata chombo alichosafiria ili kuwe na uwiano ulio sahihi juu ya wasafiri wa siku hiyo na kwa chombo kilichoainishwa.

Mhe. Spika, **s**heria imetenga biashara ambazo zitafanywa na wazalendo, kusimamia jambo hili ni muhimu sana. Tusichukulie tu kwamba hili wananchi wetu hawaliwezi, kila jambo linawezekana tujaribu kuwawezesha wananchi wetu wataweza tu.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii imeenea sana vijijini mwetu. Maeneo ambayo wanajamii wanaishi kwa karibu na wanayatumia, haitakuwa busara endapo wananchi hao ama hawatafaidika au watadhalilika kwa kuwepo kwa uwekezaji wa utalii kwenye maeneo yao. Kuwe na utaratibu mzuri wenye kuwashajiisha wawekezaji hao kuchangia kwa hiari maendeleo ya huduma za jamii Kwa vijiji vyetu uchangiaji huu usisababishe uhasama miongoni mwa walengwa bali uwe ni kichocheo cha maendeleo na maelewano yenye mahusiano mazuri baina ya wanajamii na wawekezaji.

Mhe. Spika, **s**heria hii kama zilivyo sheria nyengine imeweka utaratibu wa utungwaji wa kanuni ili kuweka mazingira bora ya utekelezaji wa sheria, jambo ambalo kamati yetu inaliomba lifanyike mara tu sheria hii itakapoanza kutumika kwani wakati mwengine kanuni hizo huwa zinachelewa kutungwa.

Mhe. Spika, niwaombe wajumbe wenzangu, waujadili mswaada huu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na hatimaye waupitishe kwa kauli moja.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha na Uchumi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono hoja hii.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin (Waziri Kivuli wa Utalii, Biashara na Uwekezaji): Mhe. Spika, kabla sijatoa maelezo ya upande wa upinzani yanayohusiana na mswada huu naomba niombe radhi kwamba mchapaji wa hotuba yangu amechelewa na haijakamilika. Kwa hivyo, baada ya kukamilika nitaiwasilisha kwa sehemu zote zinazohusika.

Mhe. Spika, mwanzo kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwenye rehema na mwingi wa hekima na uadilifu, kwa kutubarikia uzima na afya njema tukaweza leo hii kukutana katika Baraza lako tukufu baada ya mapumziko yaliyofuatia kumalizika kikao cha Bajeti ya Serikali.
Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Mswada ulioko mbele yetu. Vile vile Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapa mkono wa pole wote ambao wamenyimwa haki yao ya Kikatiba ya kujiandikisha kama wapiga kura kutokana na sheria kandamizi iliyotawaliwa na ukiritimba wa mfumo wa ubaguzi wa Chama kimoja ndani ya Eti mfumo wa vyama vingi. Pole hizi pia ziwaendee wale ambao wataendelea kunyimwa haki hiyo kwa kutumia sheria hiyo pamoja na nguvu za dola kwa kuwa tayari kujeruhi na hata kuua.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo fupi naomba sasa nizungumzie Mswada kwa maelezo machache ambayo nadhani yanaweza kusaidia katika kuufanya bora zaidi au kwa lugha ya watawala wetu kuuboresha, kwani mtawaliwa huona kila kinachotoka kwa mkoloni wake ni kizuri.

Mhe. Spika, katika kifungu nambari 2 ambacho kinatoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mswada huu, katika tafsiri ya neno mtalii naomba Mhe. Waziri anifafanulie. Je, Waheshimiwa Wawakilishi wanaotoka Pemba kuja Unguja kwa shughuli za Baraza na baadaye Waheshimiwa Wawakilishi kutoka Unguja watakapokwenda Pemba kwa ajili ya Semina mwezi ujao watakuwa ni watalii?

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mwaka uliopita kwamba tunakabiliwa na changamoto kubwa ya mfumko wa bei na baya zaidi kwamba mnamo kati ya mwaka 2008 dunia imekumbwa na mtikisiko wa uchumi, jambo ambalo kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya dunia tena tegemezi haiwachi kuathirika.
Sasa katika kukabiliana na hilo, nadhani ndio Zanzibar ikaamua kuendesha biashara hii ya utalii na kutunga sheria mpya ili kusimamia vyema kazi hiyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 cha mswada kuna kijifungu nambari moja ambacho kina sehemu (a) mpaka (t). Je, kijifungu cha pili cha kifungu hiki kiko wapi na kinaeleza nini ?

Mhe. Spika, katika kifungu hicho cha 4, kijifungu cha kwanza kinaelezea juu ya kazi za Kamisheni katika sehemu ya (h) kumetajwa juu ya usajili, kutoa leseni na kusimamia biashara ya utalii. Naomba nimuulize Mhe. Waziri je, Kamisheni itahusika na utoaji wa leseni za mahoteli, mikahawa, nyumba za kulala wageni na maduka ya utalii. Nini itakuwa taathira juu ya taasisi nyengine zinazotoa leseni?

Mhe. Spika, kamisheni itatoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa utalii. Lakini sehemu ambayo utalii unaendeshwa kunapatikana athari mbali mbali. Je, manufaa ambayo yanatokana na utalii jamii itanufaika vipi na biashara hiyo na nani atasimamia juu ya upatikanaji wa manufaa hayo ? Nadhani ingekuwa vyema hayo yakaelezwa katika sheria.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 7 (1) bodi inapewa uwezo wa kuunda kamati na kijifungu 2 (a) bodi inatakiwa kuweka hadidu rejea za kamati iliyoundwa na kamati baada ya kumaliza kazi zake, inaweza kubaki au kuendelea kuwepo. Je, kuna maana gani ya kamati kubakia wakati imemaliza kazi zake. Huku si kuongeza gharama za bure.

Mhe. Spika, kifungu cha 11 kinaelezea kuwepo kwa Mkurugenzi Mkuu ambaye ni mteuliwa wa Rais, na kijifungu 2 (a) kinataja sifa za mtu ambaye atafaa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ambapo pametajwa awe na shahada ya kwanza, ningeshauri shahada hiyo iwe inahusiana na taaluma ya Utalii kuliko kutajwa taaluma tu.

Mhe. Spika, katika kijifungu cha 3 cha kifungu hicho cha 11 ambacho mimi nina mashaka nacho kuwa ni cha 3 kutokana na mtiririko wa vijifungu kumetajwa kuweko kwa Wakurugenzi wa Idara Kuu. Je, kuna idara ngapi kuu mbona hazijatajwa katika sheria ?

Mhe. Spika, kijifungu cha 5 cha kifungu hicho kimetaja kuanzishwa kwa kitengo maalum cha ulinzi, ni jambo zuri. Lakini kitengo hicho kitashirikiana vipi na vyombo vyengine vya ulinzi na kwa masharti yepi wakati wa kutekeleza majukumu yake ya ulinzi, ni vyema yatajwe kuepusha mgongano na vyombo vyengine.

Mhe. Spika, kifungu cha 15 kijifungu kidogo cha 2 kinaelezea juu ya mwendesha biashara ya utalii kuwa na leseni. Kabla ya kupitishwa sheria hii kuna utitiri wa vyombo vinavyotoa leseni za shughuli za utalii. Je, chini ya sheria hii utaratibu huo umezingatiwa vipi.

Mhe. Spika, kifungu cha 16 kijifungu kidogo (1) (a) kumetajwa mtaka leseni alipe mchango kwanza ndio apewe leseni. Mchango huo ni mchango gani

mbona haujaelezwa katika sheria kwamba kutakuwa na michango aina kadhaa. Hivyo kuweka utitiri wa michango na ada ……

UTARATIBU

Mhe. Haji Omar Kheir: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Kanuni kinataka hati yoyote inayowasilishwa mezani iwe imefika kwa wahusika, ili mhusika anapoisoma wale watakaokuwa wamepewa wawe wana uwezo wa kuinukuu. Sasa Mheshimiwa naona ametuomba radhi kwamba hati hizo kutokana na makosa ya uchapaji hazijawasilishwa. Mhe. Spika, naomba utaratibu na mwongozo wako.

Mhe. Spika: Labda pengine tusiende mbali sana. Mheshimiwa aliomba radhi na kwa bahati sasa hiyo hati iko tayari nimeshawasilishiwa hapa na waziri sijui kama ameshapewa.

Aliomba radhi na nilimruhusu nikielewa kwamba anafanya haraka sana ili aje aiwasilishe na tayari imeshafika mbele yetu.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin (Waziri Kivuli wa Utalii, Biashara na Uwekezaji): Mhe. Spika, kifungu cha 16 kijifungu kidogo (1) (a) kumetajwa mtaka leseni alipe mchango kwanza ndio apewe leseni.

Mchango huo ni mchango gani, haujaelezwa katika sheria kwamba kutakuwa na michango aina fulani. Hivyo kuweka utitiri wa michango na ada Waziri haoni kwamba kutapelekea utalii wetu kuwa ghali na kupelekea kupungua kasi ya kuja kwa watalii.

Mhe, Spika, Kifungu cha 18 (1) kinaelezea juu ya muendesha hoteli au nyumba ya kulala wageni kuweka kumbukumbu na kuzitoa kwa mamlaka husika zinapohitajika. Jee kama muendesha hoteli au nyumba ya kulala wageni akishindwa kutekeleza hayo atapewa adhabu gani kwa kosa kama hilo. Mbona kwenye orodha ya makosa yaliyotajwa katika kifungu cha 28 haikutajwa pamoja na adhabu yake ikithibiti kuwa ametenda kosa. Ni vizuri itajwe ndani ya sheria.

Mhe, Spika, Kifungu cha 27 (4) kinaelezea kwamba biashara ya utalii ichangie shughuli za maendeleo pahali ilipo. Jee ni nani atakaesimamia hilo kwani suala hilo ni muhimu. Nadhani kungekuwa na kipengele kinachotoa dhamana ya usimamizi na pia pakaekwa kiwango maalum na kusiwachwe mwanya wa mfanyabiashara kuweza kukwepa jukumu hilo.

Mhe, Spika, Kifungu 28 cha Mswada kimetaja orodha ya makosa ambayo

yanaweza kutendwa na waendesha biashara ya utalii pamoja na adhabu pindi kosa likithibiti. Ni vyema orodha ikaongezwa kwa kuzingatia tatizo la uchafuzi wa mazingira. Pamoja na wale wanaokaidi ujenzi wa mahoteli yao karibu na fukwe.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelezo ya kifungu hichi na uelewa wangu, inamaanisha kwamba mkosaji na Mkurugenzi Mkuu wa Kamisheni wanaweza kulimaliza shauri bila kupelekwa mahakamani. Jee hali hii italeta ufanisi zaidi na haitaashiria rushwa ndani yake?

HITIMISHO

Mhe. Spika, Utalii kwa Zanzibar umefanywa kuwa sekta kiongozi katika kukuza uchumi. Madhumuni na sababu za Mswada yanaashiria hilo. Ni muhimu tusisahau kwamba ili kuweza kuendesha biashara hiyo kwa ufanisi ni muhimu kuwa na mazingira shawishi juu ya uendeshaji wa biashara hiyo, la muhimu na la msingi zaidi ni kuwepo hali ya utulivu katika nchi. Lakini kutokana na hali ya mambo yanavyoendeshwa kiutashi na si kwa kufuata maelekezo ya sheria mama hali hiyo inahatarishwa.

Mhe. Spika, katika sheria inayofutwa kumekuweko na udhaifu mkubwa wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na biashara ya utalii. Wasi wasi wangu ni kwamba hilo litaendelea hata sheria hii ikipita, kwani sikuona kipengele kinachozungumzia udhibiti huo na hatua zitazochukuliwa dhidi ya mkorofi atakapojitokeza. Sehemu nyengine ambayo inanipa mashaka ni sehemu ya mazingira na udhibiti wa taka taka zinazotoka mahotelini pamoja na maji machafu. Hali hii inahitaji kutazamwa upya.

Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri Kivuli. Mhe. Waziri Kivuli amegusia jambo ambalo pengine ni muhimu, inawezekana ikawa humu iko kama suala la kukumbushana, lakini amezungumzia Waheshimiwa Wawakilishi wanapokuja kutoka Pemba kuingia hapa na sisi tunapokwenda kule Pemba. Hiyo ni aina fulani, ingawa amegusia kwa Wawakilishi, lakini ni aina fulani ya utalii wa ndani.

Waziri atakuja kutoa majibu. Hata wananchi wanaweza wakatoka hapa wakenda Pemba na wakatembea kwenye maeneo ya mahoteli. Huo ni utalii wa ndani ambao Mauritious wanaufanya sana.

Tunakushukuru sana kwa kutukumbusha hilo. Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na mjadala. Nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na

Uchukuzi, Mhe. Mzee Ali Ussi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kukushukuru wewe Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo baada ya Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti na Mhe. Waziri Kivuli.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kuipongeza wizara, kupitia Mhe.Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake kwa kuona umuhimu wa kuleta sheria hii mbele ya Baraza lako tukufu na kuweza kuchangia mswada huu ambao ni muhimu kwa maendelea ya taifa letu, hasa tukizingatia kwamba nchi yetu inategemea kwa kiasi kikubwa mapato ya utalii kwa maendeleo yake ya kila siku katika nchi yetu pamoja na kukuza uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba niseme kwamba kwanza mimi mwenyewe binafsi, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaukubali mswada huu na kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, jambo la kwanza ambalo mimi ningetaka nifahamu katika mchango wangu ni kuhusu hawa askari wa utalii ambao watakuwepo katika taasisi hii. Askari hawa watakuwa ni askari wa polisi ama ni askari ambao wameajiriwa kwa ajili ya kitengo maalum kama walivyo katika maeneo mengine na kazi zao zitakuwa hasa zinahusiana na maeneo yepi.

Jengine Mhe. Spika, ningeomba serikali kwa kupitia wizara husika ikazingatia zaidi suala zima la utalii na hasa matumizi ya fedha za kigeni katika suala zima la utalii. Mhe. Spika, nafikiri utakuwa ni shahidi mzuri tulipokuwa katika safari ile ya kule Afrika ya Kusini. Kwa wastani tulipofika pale tulijaribu kwenda madukani kwa ajili ya kujinunulia mambo mbali mbali, lakini kilichoonekana pale ni kwamba wenzetu wamejidhatiti zaidi, jambo ambalo mimi ninalipendekeza kwa upande wa serikali yetu litumike ni kwamba huwezi kutumia fedha zile za kigeni dukani kwa kununua chochote kile, isipokuwa ni lazima uende katika maduka ambayo yamewekwa maalum ubadilishe fedha zile na kuweza kupata fedha zao, yaani zile *rand* za Afrika ya Kusini ndio unaweza kutumia katika maeneo yote yaliyobakia.

Sasa kwa hapa kwetu naona bado hili suala halijadhibitiwa vizuri. Mtu anaweza akatumia dola pahala popote hata kama ni mgeni katika mazingira ambayo pengine zile fedha ambazo zilihitajika kwenda serikalini moja kwa moja zikawafikia pengine labda watu ambao hawahusiki na pengine kupunguza mapato ya fedha za kigeni kwa upande wa serikali.

Mhe. Spika, hili nafikiria ni jambo muhimu na ni la kulizingatia, kwa sababu serikali wakati mwengine inapata tatizo kubwa la kutafuta hizi fedha, hasa pale inapotaka pengine kuwapeleka nje raia wake ikiwa ni viongozi ama jamii tu pengine mtu anataka kusafirishwa kwa ajili ya matibabu, hutakiwa apate fedha za kigeni kwa ajili ya kule anakokwenda. Sasa kama hatukuweza kudhibiti vizuri haya mapato maana yake ni kusema kwamba tutakuwa na mapungufu hayo na uwezekano wa kuwa tusiwe na mapungufu hayo upo.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba hivi sasa katika suala zima la utalii, tunasheria ile ambayo tumewafanya wenzetu wale ambao wanauza vinyago ambayo humu imetajwa katika sheria hii. Vinyago kwa kweli ni biashara moja ambayo inapendwa sana na wenzetu wageni na ingehitaji kuwa na mahala ambapo ni karibu zaidi na wale watalii wenyewe.

Kwa mfano, tulitoa hili soko la vinyago kutoka Kiwengwa chini na tukalipeleka pale Mchikeni kwa upande wa Kiwengwa. Lakini hata hivyo pale ambapo tumefanya hiyo kazi ya kulipeleka hilo soko hakuna kitu ambacho kimeendelea hadi hivi sasa, ukenda utakuta magofu na hakuoneshi dalili ya kwamba kuna maendeleo yoyote ambayo yanaweza kupatikana kwa ajili ya kukuza utalii na pengine biashara hiyo kwenda vizuri.

Mhe. Spika, ingekuwa vyema basi tuweze kuwa na maeneo yale ya karibu kwa kujenga haya maduka pamoja na masoko haya ya utalii ili mtalii asipate tabu anapotoka katika nchi yake anayoishi basi aweze kupata kile anachokihitaji.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu hii nchi yetu kwa kweli inasifika sana kwa usalama wetu sisi wenyewe, lakini pia na kwa wageni. Lakini bado kuna haja ya kuzingatia suala zima ambalo hivi sasa linajitokeza ili tuweze kutambulika vizuri huko nje na tuweze kukubalika, basi tuone kwamba haya matatizo madogo madogo yanayotokea tunayawekea taratibu na sheria kali ili kuona kwamba hakuna mtu ambaye atasumbuliwa hasa wageni pale wanapotembea.

Jengine Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana katika sheria hii basi tukaweka kifungu ambacho kinamfanya vile vile mgeni yeyote yule asitembee katika maeneo ambayo ni nje ya mji kwa nyakati za usiku.

Mhe. Spika, hivi sasa ni kawaida kuwaona wageni hawa wanatembea hata wakati wa usiku katika maeneo ambayo pengine si salama sana. Kwa hivyo, na hiyo nayo inachangia pengine kupatikana kwa uhalifu kwao kwa sababu tu ya tamaa za wale watu ambao wanatamaa.

Mhe. Spika, jengine ambalo Mhe. Mhe. Waziri Kivuli alilizungumza, naomba ninukuu hapa katika hii sheria ambayo imesema hapa maana ya yule mtalii. Inasema kwamba;

> "Mtalii ni yule mtu ambaye ameondoka katika eneo lake analoishi kwa kipindi kinachozidi masaa 24".

Maana yake ukiondoka katika eneo lako unaloishi kwa kipindi hicho basi utakuwa tayari umekuwa ni mtalii. Hiyo ndio tunayoizungumza ambayo Mhe. Spika, umenisaidia kwamba ni mtalii wa ndani. Lakini sasa utalii huu wa ndani vile vile unachangia pato, haidhuri ni kwa fedha zetu za ndani, kwa sababu kama tulivyosema hapa ni kwamba tunapokwenda Pemba sisi Waheshimiwa Wajumbe wako, kule tunakuwa tunaishi kwenye mahoteli, kwa hivyo kama tunaishi kwenye mahoteli maana yake tunachangia mapato kwa njia moja ama nyengine kukuza mapato yale kwa njia ya kuwafanya wenzetu ambao wamewekeza katika sekta hiyo ya majumba ya wageni waweze kuingiza fedha ambazo zinatoka ndani.

Pia Mhe. Spika, mimi ningeiomba wizara ikaangalia suala la kukuza maeneo haya ya misitu yetu. Kwa mfano, msitu wa Ngezi na msitu wa Jozani pamoja na wale wanyama wanaoishi humo.

Mhe. Spika, hivi sasa katika misitu yetu hii wanyama wengi wamepungua na wanapungua kwa sababu tunakosa kuwahifadhi kwa mujibu wa taratibu ama sheria ziliopo. Kwa mfano, Paa. Paa ni wanyama ambao wapo kwetu kwa muda mrefu sana hapa Zanzibar, lakini kwa hivi sasa Paa wanaonekana zaidi katika eneo la Tumbatu na kwa sababu Tumbatu kule wenyewe wanafuata zile sheria kikamilifu kwamba huwezi kuwasaka wale isipokuwa kwa kipindi maalum.

Mhe. Spika, nataka niwapongeze sana wananchi wa Tumbatu pamoja na Mhe. Mwakilishi wa Tumbatu, Mhe. Haji Omar Kheir kwa kusimamia hilo na kuona kwamba kule hakuna watu wanaowawinda wale wanyama katika kipindi ambacho kimekatazwa, kwa hivyo inasaidia.

Mhe. Spika, kwa upande wa Jozani na maeneo mengine misitu yetu ipo ya asili, lakini pia tuna misitu ambayo sisi tunaipanda kwa ajili ya kuongeza haiba kwa upande wa watalii, lakini kumekuwa na tatizo. Kwa hivyo, kuna haja ya kuona kwamba miti ambayo imewekwa kwa ajili ya hifadhi haikatwi ovyo, hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la ukataji wa miti ambayo haingefaa kukatwa hasa ukizingatia suala zima la kukuza utalii katika maeneo hayo.

Jengine ambalo ningependa kulizungumza Mhe. Spika, ni kuhusu wale watembeza wageni ambao kwa kiasi fulani wanasaidia kukuza ile sekta ya utalii, lakini nao wanahitaji kupata mafunzo kwa ajili ya kazi hii. Kwa sababu wengine pengine wanafanya kazi hii kwa hamu zao tu na pengine hata hawana mafunzo ambayo yataweza kuwafanya wafanyekazi hii kwa vizuri zaidi. Kwa hivyo, ningeomba kile chuo chetu kiliopo hapa Zanzibar cha Utalii basi kikachukua nafasi hiyo ya kuwafunza wenzetu hawa mafunzo haya vizuri, ili wakafanyakazi zao kwa utaalamu zaidi na kujiwezesha kufanya vizuri.

Mhe. Spika, jengine ningependa niipongeze wizara hii, hasa nilikuwa nikifuatilia kwa makini katika magazeti mbali mbali yanayohusiana na sekta hii ya utalii na jinsi tunavyoweza kushughulikia suala zima la utalii. Hata juzi tuliona meli moja imekuja hapa Zanzibar ambayo ina watalii kutoka Urusi, hii inatokana na juhudi zilizofanywa na mwenzetu huyu ndugu Merda, sijui kama nimelitamka sawa sawa jina lake hilo. Alikwenda kule Urusi na kufanya kazi nzuri ya kuwashawishi wenzetu wale na wamekuja na tumewaona. Kwa hivyo, kuja kwao kutasaidia.

Pia Mhe. Spika, tunao wataalamu wengi katika eneo letu hili hasa Mhe. Mahmoud Thabit ni mtu mmoja ambaye ni mtaalamu sana wa mambo mengi yanayohusiana na mambo ya sekta hizi za utalii, basi ni vizuri pengine na yeye Mhe. Mahmoud tukamshirikisha na hasa kwa sababu anaiwakilisha Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na yeye tukampa nafasi ya kwenda nje ili kuitangaza sekta hii ya utalii. Nafikiri ana uwezo mkubwa Mhe. Mahmoud, kwa hivyo atatusaidia sana katika suala zima la kwenda kuitangaza sekta yetu ya utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa niendelee kulipongeza na kulitaka liendelee ni uhusiano uliopo katika nchi zetu za Afrika ya Mashariki kwa watalii ambao wanakuja katika nchi za Afrika za Mashariki, kwa makusudi kuamua kwamba pengine mtalii aliyekuja na kufikia Kenya, basi haamui kuondoka na kwenda zake nje kurudi kwao basi mpaka afike Tanzania kwa ujumla Arusha na hatimaye Zanzibar. Kwa hivyo, ningependa na wenzetu hawa tukashirikiana katika jambo hili ili kuona hiyo sekta ya utalii inakwenda katika hali hiyo.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa na hata Mhe. Waziri Kivuli ni kuhusu udhibiti wa mapato yanayotokana na sekta ya utalii. Mhe. Spika, udhibiti wa mapato ni jambo muhimu. Napenda nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake za makusudi za kuona kwamba mapato yanayotokana na utalii yanaingia mikononi mwa serikali, ndio sasa tukawa tunaweza kufanya shughuli zetu nyingi.

Mhe. Spika, kama tutakumbuka hapo nyuma kabla ya kuingia sekta ya utalii kuifanyia kazi vizuri tulikuwa na matatizo mengi, hasa mishahara pia ilikuwa ikichelewa kutolewa kutokana na ukosefu wa fedha. Lakini sasa hivi sekta hii ya utalii inasaidia sana kuweza kupata mishahara kwa wakati kutokana na usimamizi mzuri. Nakubaliana na wale wanaosema kwamba bado kuna mianya midogo ipo, lakini kwa sababu wizara husika ipo na kwa kupitia Wizara ya Fedha basi nafikiri watalizingatia hilo, ili kuona kwamba maeneo hayo hayaachiwi mianya.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka tulitilie mkazo ni kwamba pamoja na watu wengine, lakini watu ambao tunatakiwa tushajihishe huu utalii basi ni pamoja na sisi wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, ningeomba sana kwamba kwa wale ambao watakuwa na uwezo basi wakaanzishe hizo kazi za kujenga hayo majumba aidha ya kuweka wageni ama mahoteli. Haidhuru madogo madogo, kwa sababu uwezo wetu utakuwa sio mkubwa sana, lakini tukiweza kufanya hivyo maana yake tutaweza na sisi kuchangia au kutoa mchango kwa serikali, ili kuona kwamba tunaweza kuiendeleza sekta hii ya utalii.

Mhe. Spika, nilikuwa na mchango huo hasa katika hilo. Vile vile ningetaka nimalizie kwa kuomba sana wenzetu wa vyombo vya ulinzi na usalama hasa maskari, kwa kushirikiana na hao maaskari ambao wametajwa humu nafikiri tunawaona katika vituo vya polisi pale inaposimama gari ya utalii, basi polisi ambaye yupo pale na yule mtu wa utalii anakuja pale ili kutaka kujua pengine ile gari inayopitisha wale watalii ina kibali na imelipa vizuri, kwa hivyo kuna mashirikiano mazuri. Vile vile kuondosha usumbufu kwa wageni mara tu baada ya kazi zao zile basi wasichukuwe muda mrefu wawe wanawaruhusu, hasa wakati mwengine wageni wanakuwa wanaondoka kwa muda maalum. Kwa hivyo, ningeomba ifanyike hiyo kazi vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nafikiria niseme tu kama nilivyosema mapema kwamba mimi mwenyewe binafsi naunga mkono huu mswada, kwa sababu ni mswada mmoja muhimu ambao utasaidia sana mchango wa taifa letu kwa hapa tulipo na huko tunakokwenda. Mhe. Spika, mimi mwenyewe pamoja na wananchi wa Jimbo la Chaani tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniona haraka na kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. Mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tumeupokea mswada huu na natanguliza kusema kwamba tunaunga mkono.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kufikiria kwamba hivi sasa

umefika wakati kwamba ile sheria tuliyokuwanayo tuifanyie matengenezo ili iweze kukidhi shughuli za kiutalii ipasavyo, lakini wakati huo huo shughuli hizo zitupatie tija kwa sababu imeonesha ina mategemeo ya kutupatia fedha. Kwa hivyo, kwa hilo nashukuru.

Pia isingefikia hivyo, isipokuwa ni kutokana na jitihada ya wenzetu tuliowapa dhamana hizi za kuishughulikia ipasavyo sekta hii, kwanza kwa utaalamu. Naipongeza serikali kwa kuwasomesha wataalamu wa sekta hii na sasa wanatufikisha pahala sekta hii na sisi kuwemo katika midani za nchi zenye kuendesha shughuli za utalii kwa njia kama za viwanda, serikali yetu kufikia katika hatua hiyo ni jambo la kujipongeza. Mafanikio yake tumeyaona kwenye bajeti nini mchango wa sekta ya utalii umechangia katika bajeti ya serikali.
Kwa hivyo, Mhe. Spika, juhudi zote zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuihuisha sekta hii katika kupata mapato zaidi kwa serikali, mheshimiwa tunawashukuru viongozi wetu wa serikali katika kufikia haya.

Mhe. Spika, sasa nije katika mchango wangu unaohusiana na mswada huu, na mimi katika sehemu ya ufafanuzi pale, hasa pale panapo askari wanaohusiana na mambo ya utalii. Ningeomba Mhe. Spika, na mimi nichangie kidogo kuhusiana na sehemu hiyo. Katika ukurasa wa 37 kwenye kifungu ambacho kinasema askari wa utalii maana yake ni afisa wa kitengo maalum kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 114 cha sheria hii ili kuhakikisha usalama wa watalii na mali zao.

Mhe. Spika, mambo ya uaskari kwanza ni mambo ambayo yanajumuisha mambo katika Jamhuri ya Muungano, lakini hata hivyo katiba imetukasimu kuunda vitengo maalum. Kwa maoni yangu Mhe. Spika, vitengo maalum tulivyoanzisha nafikiri vinakidhi. Tunacho kitengo maalum cha KMKM, Valantia, Kikosi cha Zimamoto hao cha Valanatia, Jeshi la Kujenga Uchumi na vyenginevyo ambavyo sivikumbuki kwa ghafla.

Mhe. Spika, imani yangu ni kwamba vyombo hivi ndio vya ulinzi kwa serikali pamoja na sehemu zake zote za kiuchumi. Sasa tukianza utaratibu huu wa kamisheni hii iwe na askari, Baraza la Mji pale tumeshakuwa na askari. Sasa tutakuja kutunzwa na majukumu haya ya kiulinzi.

Mhe. Spika, ni vyema basi vikosi tulivyonavyo tuviimarishe ili viweze, kwa sababu nchi yetu ni ndogo. Nchi yote itakuwa wahudumu ni askari tu, itakuwa kama ni nchi ya Kichina. Kwa hivyo, mimi nashauri juu ya suala hili kwamba ni askari ni gharama. Kile kivazi tu cha askari Mhe. Spika, kama haijatimia 700,000/- basi hujamvisha askari akatimia, kiatu chake, masoksi yale, makaptura, magwanda, ukanda, kofia na flana yake ya ndani na humpi sare moja. Askari uchache wake awe na sare angalau nne, moja iko kwa dobi, moja

kavaa, nyengine ziko kwenye pasi na nyengine ameweka akiba ikimuharibikia.

Kwa hivyo, wakati nchi yetu pato lake ni ndogo kuongeza askari, mheshimiwa suala hili mimi kwa maoni yangu naona tulitizame kwa mapana. Labda maafisa tu ambao baadae watakuwa wanashirikiana na wenzetu. Mimi nasema bado hatua hiyo itakuwa inatupa ugumu na gharama katika mzunguko mzima wa serikali yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningeishauri serikali kwamba Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji bado iendelee na mashirikiano kama yaliopo sasa hivi na vyombo vyetu vya ulinzi katika kuweka ulinzi kwa watalii wetu pamoja na biashara nzima ya sekta hii.
Mhe. Spika, eneo jengine katika huu ufafanuzi kwenye ukurasa huo huo wa 37 katika neno "Mtanzania". Mhe. Waziri anatuambia maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria ya uraia wa Tanzania au kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya kampuni ya sura ya 212 ya sheria ya Tanzania.

Sawa. Lakini Mhe. Spika, hapa tunashughulika na sheria yetu ya Zanzibar, hivi bado sisi katika sheria yetu ya makampuni inasemaje juu ya hili. Kwa sababu kwenye mambo haya ya kimahakama kila mmoja na madaraka yake, je sisi kwenye sura ya makampuni inasemaje juu ya suala hili la Mtanzania, hatuna sheria kama hii hata tukawa tunaweza kunukuu sheria ya Tanzania nzima.

Mhe. Spika, suala jengine ni katika kifungu cha 3(3) kinachohusiana na kamisheni pamoja na muundo wake. Kwa hivyo, hivi sasa imeonekana kufanyike marekebisho kwa kamisheni hii.

Je, katika utayarishaji au kwenye muundo huu mpya unafafana na kamisheni ya aina nyengine katika nchi yetu ya Tanzania au kikanda kama vile *SADC* pamoja na maeneo mengine. Kwa sababu hivi sasa shughuli zetu tumeingia kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na masuala ya utalii tunalo soko letu la kanda la nchi za Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

Mhe. Spika, katika muundo huu ambao tunarekebisha sheria hii kweli utakidhi matakwa ya kushirikiana na wenzetu kikamilifu au itakuwa nusu na mengine tunaungane na wenzetu wa Bara, ili tuweze kufikia lengo. Mhe. Spika, hapa namuomba Mhe. Waziri anihakikishie sheria hii katika muundo huu basi Zanzibar bila ya kutegemea sheria ya Tanzania Bara tutaweza kuendesha shughuli zetu sawa kimataifa bila ya kukopia.

Suala jengine ambalo naomba kuchangia ni kuhusu kazi za bodi na hapa zimetajwa nyingi. Lakini naomba kwenye mengineo katika kazi za bodi kuongeza mashirikiano hasa na wadau wa Sekta Binafsi za Wazalendo.

Mhe. Spika, uchumi wowote kwa kutegemea wageni tu, basi unaweza kupanda haraka na kushuka mara moja. Kwa hivyo, mategemeo yangu ni kuwa bodi hii mpya itakuwa karibu sana na wawekezaji wa Sekta Binafsi Wazalendo, ambao hao wakati wote tutahakikisha kwa mujibu wa uzalendo wao watakuwa na uchungu wa nchi yao, kama kwa hasara pamoja na faida ndogo basi shughuli hii itakuwa inaendelea.

Pamoja na kwamba watu watapata faida japo ndogo, lakini angalau wananchi wetu watafaidika na ajira. Kwa kweli mgeni anakuja hapa kwa lengo la kuhakikisha kuwa anapata faida tu, habari ya wananchi wamepata kazi au hawakupa wala hashughuliki.
Mhe. Spika, ndivyo tunavyoona hivi sasa hata wafanyakazi wanaweza kuchukua popote licha ya sheria tulizonazo, kwamba wachukuliwe Tanzania Bara pamoja na Zanzibar, lakini wao wanaweza kuchukua Kenya na hata Mauritius na wala hawajali hata tukiwaambia kama tumekuwa tukiwapigia zumari mbuzi kwa wawekezaji wetu tulionao.

Kwa hivyo, nadhani tukaweka mikazo pamoja na motisha kwa wazalendo wetu bodi hii itaweza kupanua wigo mkubwa kukakikisha biashara hii inakamatwa na wazalendo na kuleta tija mara mbili, kwanza wenyewe watakuwa wamefaidika, yaani fedha watakazopata wazalendo zitakuwepo hapa na kusaidia sekta nyengine ambazo zitakwenda kwenye mabenki yetu na serikali itaweza kuzitumia pamoja na wafanyabiashara wengine.

Lakini tutahakikisha wazalendo wanachukua jamaa zao na kupata ajira, ambalo hivi sasa hilo limekuwa kero na kitu ambacho ni maudhi kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, katika hizo kazi za bodi ningeomba waelekeze eneo hilo.

Mhe. Spika, jambo la tano ambalo nataka kuchangia ni namna ya kugaiwa maeneo ya utalii. Najua serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipodhamiria kwamba sasa inajikita kwenye masuala ya utalii, basi visiwa vyetu vyote vya Unguja na Pemba viliainisha maeneo ya shughuli za utalii. Kwa bahati mbaya sana maeneo mengine yameshughulikiwa na wawekezaji wameelekezwa huko, lakini wengine wamechagua wanamotaka wao hasa katika vijiji vya pwani.

Kwa kweli naamini baada ya miaka 5 mpaka 10 vijiji vya Paje na Bwejuu ule uasili utatoweka kabisa na ukitoweka kabisa bado nchi yetu itarudi kule kwenye uasili, yaani watu watarudi maweni ambamo wasimoweza kulima na wala kufanya shughuli zozote pamoja na kwenye ukame.

Mhe. Spika, maeneo haya yameuzwa kwa sababu ya umasikini, kutokana na ujinga au kutofahamu wananchi wa humu wamejiuzia kwa fedha chache na hivi sasa wamerudi kwenye maeneo kame ambayo kazi zao hazifanyiki vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri kwa sababu yapo maeneo maalum ambayo yamewekwa kwa ajili ya utalii, ruhusa ya sehemu nyengine zozote zisizokuwa mule basi serikali izuie. Kwa sababu mbali ya athari nilizoeleza pia zinaathiri mila pamoja na silka za nchi yetu.

Kwa mfano, watalii wanaonekana wamevaa nguo zao za ndani tu na wamekaa ufukweni, basi watoto wanaiga pamoja na watu wazima, yaani wanaona mambo ambayo si mila wala silka zetu. Kwa kweli na hizo ni athari ambazo ni miongoni mwa matatizo.

Mhe. Spika, maeneo ambayo yameainishwa na serikali yapo zamani tokea zilipoanza shughuli hizi, kipindi kile alipotuletea taarifa za mafuta Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tulipewa ramani ambazo zinazoonesha sehemu zote za utalii.

Eneo jengine kwa hawa wawekezaji hasa wa shughuli za utalii, yaani mahoteli wanapewa maeneo makubwa sana bila ya kuitumia na ardhi yetu ni ndogo, yaani ni kisiwa. Kwa kweli ardhi ni kubwa sana kuliko maeneo wanayotumia na hii ni athari baadaye sisi wananchi tunaongezeka, lakini bado eneo la shughuli zetu za maendeleo hatutaweza kuzifanya hasa za kilimo.

Kwa kweli utalii bado haujaweza kutosheleza ajira hata robo tatu ya Wazanzibari, lakini eneo lote likachukuliwa na hivi sasa wengine wanaishi kwa kilimo. Kwa hivyo, maeneo makubwa yote tukaweka kwa ajili ya utalii wakati bado pato la taifa kutokana na utalii halijaweza kutosheleza angalau kuwapa fidia mwananchi ambaye hana kazi liweze kumlisha halijaweza kufikia kiwango kikubwa cha kutosha.

Kutokana na hali hiyo bado tutaendelea kutegemea ardhi yetu kwa ajili ya shughuli nyengine kama vile ufugaji, kilimo pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, Mhe. Spika suala la utoaji wa ardhi kwa wawekezaji hasa wa shughuli za utalii ipunguzwe. Hilo ni la kwanza.

Jambo la pili mikataba wanayopewa wawekezaji inakuwa ni mikubwa, yaani inaanzia miaka 30 na kuendelea. Kwa hivyo, maeneo haya kudhibitiwa kwa muda mrefu nalo ni tatizo, basi ni vyema yakafikiriwa. Ingawa wanasema kwamba biashara haitabiriki, lakini si kweli. Kwa sababu yule aliyepewa kutokana na kumbukumbu hafiki hata miaka 10 hisa yake anauza na kumuuzia mwengine, kwa nini auze na wala hajapata faida.

Kwa mfano, wawekezaji wengi ambao waliopewa tokea mwaka 2000, basi mpaka mwaka 2006 wengine hawapo kabisa kwenye kampuni ile, yaani amemuuzia mwengine na ameuza kwa sababu yeye tayari ameshafaidia kwa hiyo anauza na kwenda kutafuta sehemu nyengine.

Mhe. Spika, ninahakika kwa wawekezaji wa Zanzibar hakuna hata mmoja aliyepata hasara isipokuwa wanafaidika, lakini sisi faida yetu bado imekuwa ndogo na sisi ndio tunategemea ardhi yetu.

Kwa kweli, Mhe. Spika semina moja ya Baraza hili ilifanywa Holeli ya KEMPINSKI na tuliona hata ule ujenzi wenyewe, yaani imewekwa nyumba moja hapa na nyengine kule. Kwa mfano, Mhe. Spika chumba ulichopangiwa ilibidi uletewe kigari na kuweza kuelekea sehemu ya kupata chakula, yaani jinsi walivyopewa nafasi baada ya kuweka chumba na chumba kiasi ya mita 50 na kuelekea *dinning hall*, lakini unakwenda kwa kigari na eneo jengine zaidi ya kilomita mbili au tatu hawajalifanyia chochote na ile ni hasara kwa nchi.

Mhe. Spika, eneo lile linaweza kukimu wakulima angalau 150 kupata mtama, viazi vikuu na vyenginevyo kwa ajili ya kujilisha wao wenyewe. Kwa hivyo, natilia nguvu mtazamo wangu kwa nini watu wasipewe maeneo makubwa, kwa sababu maeneo mengine hawayatumii ipasavyo na pia yanaacha umasikini kwa wananchi hasa wazalendo.

Suala jengine kuhusu sheria hii mpya imuangalie na mwananchi kwa maeneo ambayo pengine yameonekana ni ya utalii, lakini anayamiliki Haji Mkema au Mhe. Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi na hata mwengine kwa kumpa fidia ya dola mia moja bado hujamsaidia kitu.

Kwa sababu kile ni kijungumeko, atajengea nyumba na kuezekwa bati na aoe mke kama hana mke, lakini kusomeshea watoto wake skuli basi hawezi hata kidatu cha nne (*Form IV*) fedha zimekishwa, lakini ardhi yake ile aliyokuwa akilima muhogo, kufugia mbuzi na maisha yake ya kawaida yalikuwa yakiendelea.

Mhe. Spika, naona kuwe na mtazamo mzima kwa wale ambao maeneo yao yamechukuliwa na serikali, bado kuwe na fedha endelevu zinazoweza kumsaidia yule ambaye aliyetoa eneo lake kwa kuuza, utaratibu huu waelimishwe wananchi wetu wasiwe wanatoa maeneo ovyo, waripoti serikali katika mauzaji yake, ili aweze kujengewa haki.

Kwa kuwa Mhe. Waziri ni jamaa yangu kwa Kizimkazi. Mhe. Spika, tunacho kilio kwa Mchangamle, kwa sababu tulipewa eka pale na imechukuliwa, lakini

baada ya fidia tuliyopewa na hivi sasa tumeacha kazi basi hatuna kitu na yeye ameathirika kidogo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa hali ile ambayo tuliyonayo mimi na yeye, basi tukajijengea sisi wenyewe maana yake tuko kwenye madaraka hivi sasa na tukajenga uwezo na yule mjomba yetu ambaye alikuwa na eka yake pale basi angalau yule mwekezaji awe anatoa na chengine chochote japo mwisho wa mwezi, ili kiweze kusaidia katika maisha.

Kutokana na hali kama hii kweli tutaona faida ya utalii, lakini kwa kumwachia mtu au kusema eneo hili tumeshampa mwekezaji na wenzetu wa *ZIPA* wamekazana juu ya hili na wala sijui wanapata nini katika hili. Kwa sababu wanaweza kumtisha mshamba, kwa kweli tunatishwa sana Mhe. Spika, yaani tunaambiwa kama hapakutolewa basi patatolewa kwa nguvu, kwa hivyo suala la kututiza watu wa *ZIPA* Mhe. Spika liachwe, kwa sababu ardhi tunatoa kihalali kama eka tatu ni sheria iliyowekwa tokea wakati wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Kwa mfano, masuala ya kutishwa na kuambiwa hapa patachukuliwa na serikali kama hutaki tayari ameshaletwa mzungu na hivyo ndivyo tunavyoambiwa shamba. Kwa hivyo, tusitizwe kwa sababu ile ni haki yetu ya kutumia kwa ajili ya kutusaidia na tunataka kutoa vyema na kama hatutaki basi tusilazimishwe kwani ile ni ridhaa yetu na wala mtu chake hawezi kulazimishwa.

Mhe. Spika, zinatumika nguvu za hadaa kwa wale wanyonge kama vile masikini hawakusoma ambao ni washamba wanahadaliwa, kwa nini wanahadaliwa na ile ni dhulma, basi ananyang'wa na kuachwa mikono mitupa na kufa na umasikini wake.

Kwa hivyo, kweli tunawekeza hasa kwenye masuala ya utalii, lakini wananchi watizamwe hatima yao. Mhe. Spika, bado serikali yetu hata ikipata vipi haijakuwa na mtazamo wa kumtizama masikini, hivi sasa zinashinda zile fedha kidogo za kupewa wale wazee wetu kila mwisho wa mwezi.

Tokea wakati wa marehemu Mzee Abeid Amani Karume alipoanza miaka 45, basi kiwango kingeweza kuinuka kwa wale kidogo lakini hivi sasa wameongezeka na kipato chetu kidogo bado maisha ya wananchi wetu yatazidi kudidimia na rasilimali yetu ni ardhi nayo inakwenda kwa wawekezaji bila ya mafanikio.

Mhe. Spika, utalii tumeukubali lakini uje kwa misingi ya kumhakikishia mwananchi anafaidika vilivyo kwa maisha ya hivi sasa na vizazi vya baadaye.
Mhe. Spika, utalii katika eneo jengine kwamba kutakuwa na uwakala wa

mambo ya watalii kwa usafirishaji pamoja na kuwatembeza. Kwa kweli suala hili ni jambo zuri, kwa sababu lazima kuwe na chombo cha kuwashughulikia.

Lakini katika mifumo ya kisasa na wenzetu katika kushughulikia watalii wako watu binafsi, yaani mmoja mmoja nadhani humu ndimo mnamotokea mambo yanayotutia kasoro katika shughuli zetu za utalii kama vile kuna mapapasi, gari za daladala.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nadhani angefanya utaratibu wa kuwaelekeza wenzetu hasa wasafirishaji, kama vile bodi au wa gari wakafanya umoja wao na kuweka chombo mwenye gari mbili au moja japo ataendesha mwenyewe ni vyema kuwa kwenye kampuni moja na kuweza kusajiliwa na kujulikana na hivyo ndivyo wanavyofanya wenzetu.

Isipokuwa kipato chake atapewa kwa mujibu wa hisa aliyoweka, lakini kila mmoja gari yake anachukua huyu na yule, wakati mwengine huwa wanakuwa na tabia mbaya kwa kushirikiana na wenzao huwaambia tayari wameshawapeleka watalii mahala kadhaa na jioni wanawavamia na kuwaibia camera pamoja na vitu vyengine.

Mhe. Spika, kama kutakuwa na kampuni basi mtalii yule ameibiwa kwenye gari kampuni ile ya usafiri ndiyo itakayokuwa na dhima, kwa sababu hiyo ndiyo dhamana na hata Wizara au Shirika la Utalii ama Kamisheni inajua kwamba kampuni hii ndiyo tuliyowapa watalii wa Kifaransa au Wataliana na dhima yote watakuwa wamebeba wao.

Lakini utaratibu wa hivi sasa ameweka *Tax Stand* yake anakuja mtalii na kwenda kumkamata shati. Kwa kweli ule utaratibu ambao upo pale pwani unatia unyonge na tena ni aibu hasa kwa wale watalii wanaokuja kwa bodi, yaani mtalii anakamatwa mkono mtalii kama mtoto anayepelekwa kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja siku za sikukuu. Kwa kweli wananyang'anyiana na wanatuona watu wa ajabu na kusema njoo huku na wengine lugha ya kiswahili hawajui na wala si utaratibu mzuri.

Mhe. Spika, nadhani kama kungekuwa na kampuni basi zinakuwepo gari tu na inapojaa basi inaletwa nyengine, kwa sababu kipato wanachopata kitakuwa kimoja, lakini kila mmoja na kipato chake basi ndivyo vile mtalii anakamatwa mkono kama anapelekwa sikukuuni katika viwanja vya Mnazi Mmoja na wala ule si utalii Mhe. Spika isipokuwa ni uhuni.

Kwa hivyo, katika masuala ya utalii tusifanye uhuni na wajue kwamba sisi ni watu wastaarabu ambao tunaendesha shughuli zetu kistaarabu, kwa sababu wao wamekuja kustarehe hapa. Kwa mfano, tokea anapofika bandarini anapokelewa

anatembea pamoja na kulala katika hali nzuri.

Kwa kweli, ile tabia inayofanyika pale ni ya kihuni ambayo inashusha hadhi katika mambo yetu ya huduma, kama kuna masuala yale ya kutathmini basi pale kwenye huduma anaweka *fair* baada ya kutia *excellent* au *good*. Kwa mfano, mtalii anapoulizwa wakati ulipokwenda Zanzibar mambo ya huduma za usafiri yako vipi basi anaweza kutia *fair* kutokana na utaratibu uliopo pale, kama vile mtalii anaweza kuingia kwenye gari wakati mzigo wake umepakiwa kwenye gari nyengine.

Mhe. Spika, napenda kama sheria ilivyozungumza kama kuwe na wakala, kwa hiyo hawa watu mmoja mmoja wajiunge na wafanye wakala na kampuni yao basi. Kwa mfano, gari ya mizigo hii pamoja na watalii na wanawachukua pamoja katika hali ya usalama tena kwa ustaarabu.

Shughuli hizi za utalii hivi sasa ndio miongoni mwa mambo nchi inategemea. Kwa hivyo, suala la mafunzo, yaani utaalam bado kuna haja ya kupeleka wimbi la wananchi wetu kwa ajili ya kujifunza fani hii ya utalii.

Kwa sababu fani hii inahitaji huduma nyingi kwanza nyumba, chakula, vinywaji, usafiri sasa mambo yetu yakifanyika kitaalam ndipo yanapokuwa mazuri. Kwa mfano, mapishi ya kuweka mafuta kikaangoni na kukoroga bado hayajatosheleza, kwa hiyo ni lazima wapelekwe wenzetu kujifunza utaalam huu vizuri.

Pamoja na hilo naomba kusisitiza hali ambayo tunaizungumza kila siku ya kuimarisha Chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii. Kwa kweli kuna haja ya kukiimarisha chuo chetu, kwa sababu mbali ya jitihada bado hakijaweza kukidhi kutoa wataalamu wa kutosha. Kwa mfano, fani ndogo ndogo za wahudumu wa kutandika vitanda, kupeleka vinywaji, lakini fani nyengine bado hatujakuwa na wataalamu katika kiwango cha juu.

Mhe. Spika, mbali ya hawa kutumia chuo chetu cha hapa, lakini serikali kwa makusudi kipeleke vijana wetu nchi za nje kwa ajili ya kujifunza pamoja na kuona mitindo kwa sababu kila siku fani hizi zinabadilika sawa na mishono ya nguo, yaani mipango ya huduma imekaa kama mishono ya nguo. Kwa mfano, gilasi mwaka huu hoteli hii inaweza kukamatwa kwa namna ya aina yake na nyengine pia katika hali ya kumhudumia mgeni.

Kwa hivyo, tusione kama kawada anapohitaji mtalii maji na kupelekewa kama kawaida, isipokuwa kuna namna ya kupeleka gilasi ya maji. Mhe. Spika, lengo langu ni kuhakikisha huduma zetu lazima tuweze kuziboresha katika njia ya kitaalamu.

Lakini kwa sababu tunao watu wengi na hivi sasa milango ya afisini hatuna. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa ikichukua kundi la walimu na hivi sasa walimu wamejaa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nako tayari kumejaa, kwenye vikosi ndio hao tunasema vipunguzwe, kwa sababu hata ile *ratio* ya kimataifa ya askari, wananchi 1500 kwa askari mmoja na sisi hapa tupo 540 kwa askari mmoja.

Kwa hiyo, kiwango chetu tulichokipata kwa wenzetu wa jeshi wanatuambia usalama wetu uko zaidi, kwa sababu askari mmoja anahudumia watu 500 wakati kimataifa imeweka 1500, kwa maana hiyo hili ni jambo la kujivunia nayo imeshajaa. Kutokana na hali hiyo hivi sasa tunategemea hii sekta yetu ya utalii.

Mhe. Spika, nadhani wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali washushe somo hili katika *syllabus* zao, ili wanafunzi wimbi hili kubwa waweze kujikita huko na baadaye waweze kuchukuliwa. Kwa maana hiyo, elimu yetu ilingane na yale mazingira ambayo tunayohitajia, yaani elimu ya hivi sasa ilenge katika malengo ya mahitaji ya taifa.

Kwa hivyo, nadhani shughuli za utalii na Rais Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Abuod Jumbe Mwinyi aliingiza siku ya kilimo mpaka Skuli ya Sekondari ya Lumumba ikawa ya kilimo, kwa sababu tulikuwa tukihitaji wataalamu wa kilimo na Skuli ya Fidel Castro ikawa ya Uvuvi japo hatukufikia, lakini alifikiria dhana kwamba hivi sasa nchi yetu tunategemea kilimo na uvuvi.

Kutokana na hali hiyo, elimu ianzie huko kwa sababu wanapomaliza hawawezi kuajiriwa, basi wataweza kuvua pamoja na kulima. Lakini hivi sasa kwa kuwa ni tegemeo hilo ni la taifa tunaambiwa ni sekta tegemezi. Mhe. Spika, *syllabus* yetu ya skuli hivi sasa somo la kuhudumia au shughuli za utalii liwemo na wanafunzi wetu wanapomaliza basi waweze kujikita kwenye eneo hilo.

Kwa sababu kweli hivi sasa vijana wengine wanaweza kuzungumza Kitaliana. Kwa mfano, jimboni kwa Mhe. Ame Mati Wadi watoto wanazungumza Kitaliana utafikiri wako Milani, yaani wale wamejifundisha wenyewe na masomo yale yakiwemo mle angalau ya lugha basi yanaweza kuwasaidia sana katika kupata ajira kwenye sekta ya utalii.

Mhe. Spika, kama si hivyo tutasema tu aa! Bwana hawatuajiri na kweli hawatoweza kutuajiri, kwa sababu hatuna utaalamu ule. Kwa mfano, mtu amewekwa *Desk Officer* na anafika mgeni wa Kirusi hajui Kiingereza wala Kifaransa isipokuwa Kirusi atamhudumia vipi.

Kwa hivyo, nadhani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hasa kwa upande wa lugha basi ijitahidi katika masuala ya *communication*, ili wanafunzi wanapotoka, basi angalau kila mwanafunzi awe anajua lugha tatu mpaka nne na inapotokezea haja ya kuajiriwa kwenye sekta hii ya utalii basi Mhe. Waziri asipate tabu ya kuweza kuwasisimia na kuwapatia ajira kwenye eneo hilo.

Mhe. Spika, nafikiri nimezungumza vya kutosha, lakini hii yote ni kutilia mkazo kwamba mswada huu ninaukubali wa Mhe. Waziri na ninategemea tutapata michango mingine, haya niliyoyazungumza ndio yanayotokana na matatizo ya wananchi.

Kwa hivyo, imekuja sheria hii na kwa bahati nzuri imeweza kuyazungumza na wakayasikia na Mhe. Waziri amesikia mategemeo yao, ili sekta hii iwe kweli ni sehemu ya pili ya mafanikio ya vijana wetu katika kujipatia ajira kwa wakati huu ambao tunashida kubwa ya ajira.

Mhe. Spika, nakushukuru sana pamoja na Mhe. Waziri nampongeza sana na narejea tena kusema kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika mswada huu uliowasilishwa hivi asubuhi na Mhe. Waziri. Kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta mswada huu wenye madhumuni mazuri.

Vile vile sababu na madhumuni ya mswada huu imeweka wazi malengo ya mswada huu pamoja na hayo kabla sijachangia naomba kuunga mkono mswada huu mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa jimbo langu la Mfenesini kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sikuwa na nia ya kuchangia mwanzo kwa sababu ni mjumbe wa kamati na tayari mswada huu tumeshaukalia kwa siku nzima kuujadili. Kutokana na hali ya mazingira ilivyo, basi nimeona bora na mimi niuchangie muda huu.

Kwa hivyo, kwenye mchango wangu nitakwenda katika sababu na madhumuni ya mswada huu. Mhe. Spika, siku zote kwenye miswada huwa tunalalamika sana kwamba sababu na madhumuni huwa haziko wazi, lakini kwa mswada huu tunampongeza yeye mwenyewe Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake, kwamba ukisoma tu sababu na madhumuni basi unapata kufahamu malengo ya mswada huu kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba ninukuu sehemu tatu kwenye sababu na madhumuni, ili kudhihirisha yale ninayoyazungumza. Kwa hivyo, naomba unistahamilie Mhe. Spika.

Sababu na Madhumuni

> "Mswada huu wa Sheria unalenga kuweka mfumo bora wa kisheria, ili kujenga mazingira mazuri na kukuza biashara ya utalii …"

Kwa hivyo, hilo ni lengo zuri kwa sababu kwanza katika uchumi wetu hivi sasa Sekta Kiongozi ni Utalii. Kwa kweli tumeona huko nyuma pamoja na kwamba tulifanya jitihada kubwa, lakini sheria yetu ilionekana ina vikwazo vidogo vidogo. Kwa maana hiyo, marekebisho haya yataupa nguvu utalii wetu, ili tufikie kwenye malengo.

Vile vile *paragraph* ya pili amezungumza kwamba mpango utawezesha wazalendo walio wengi katika ngazi zote hasa vijijini kushiriki na kuchangia moja kwa moja katika ukuzaji uchumi. Hili ni suala zuri kwa sababu huko vijijini hasa ndio kwenye dhamira na malengo ya kusaidia hasa hao wazalendo waweze na wao kukidhi mahitaji yao pamoja na kuendeleza maisha yao. Pia katika ukurasa wa mwisho amezungumza kwamba watatengeneza soko kwa bidhaa zinazotengenezwa hapa Zanzibar ili hao watalii wakija wapate kununua nao wapate kunufaika. Mhe. Spika, mambo yote ya msingi na ndio yanayoendeleza utalii wetu. Kwa hivyo, tunamshukuru mheshimiwa pamoja na wataalamu wake na sheria ikipita nadhani mambo yetu yatakwenda vizuri.

Mhe. Spika, pia katika ukurasa huo huo kuna sehemu imezungumzia kanuni, ni kwamba sheria imemtaka Mheshimiwa Waziri baada ya mswada huu kukamilika atengeneze kanuni ambazo zitasaidia baadhi ya vipengele vya sheria vitaongozwa na kanuni hizo. Hapa nilikuwa nataka nimuombe mheshimiwa pamoja na wataalamu wake kwamba miswada mingi inayokuja hapa inachukua muda mwingi kutengenezewa kanuni, lakini namuomba kwa umuhimu wa mswada huu basi hizo kanuni nadhani sisi tukishaupitisha tu zitengenezwe ili ziende sambamba na sheria hizo. Kwa sababu kanuni zikichelewa zitakuwa zinaleta matatizo kwa hivyo namuomba hilo sana yeye na wataalamu wake wakae watengeneze hizo kanuni ili tuweze kuupeleka mswada wetu katika hali nzuri.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye ukurasa wa 39 kuhusu muundo wa Bodi ya Wakurugenzi. Ameelezea mwenyewe kwenye sheria mwanzo haikuwepo lakini sasa hivi tayari bodi ipo na kuna watu wametajwa ambao wanaunda bodi hiyo. Mimi nilikuwa na mawazo katika hao wajumbe wa kwenye bodi.

Kwanza amezungumza kwamba kutakuwa na mwenyekiti ambaye mara nyingi huwa anateuliwa na Rais. Yeye mwenyewe mheshimiwa huwa anapeleka majina matano ambao katika hao mmoja wapo akiteuliwa anaweza akaifanya kazi hiyo bila ya wasi wasi wowote. Lakini baadhi ya miswada huwa naona mwenyekiti anapotajwa humu kwenye sheria huwa anaekewa na sifa, lakini huu sifa sikuziona. Mimi nilitaka maelezo kidogo kwamba pengine atakapokuja kutufanyia majumuisho anambie pengine angeliweka sifa kungekuwa na kasoro moja, mbili, tatu ndio anaona bora aache hivi hivi wazi ili kila mwenye sifa anayoitambua yeye anahitajika kwa kazi hii aweze kumpendekeza na Mhe. Rais aweze kumteua.

Mhe. Spika, kama kuna lolote la ziada ningeomba anieleze kwa nini sifa zisiweko. Pia kuna wajumbe wengine ambao wameanishwa kwenye sheria kwamba atawateua yeye ni wajumbe sio chini ya wanne na hao wawili watatoka katika taasisi mbali mbali zinazojitegemea. Lakini kuna wengine tayari wamekwisha kutamkwa kwamba huyu atatoka kama sehemu ya daktari ataingia kwenye bodi hii. Mimi ningelishauri bora kungefanywa mfumo wa kama hao wawili kwamba watoke sekta binafsi lakini baadae wakifika huko yeye mwenyewe ndiye anayeteuwa katika hao kuliko kutaja kabisa nataka daftari, nataka *engineer* naona sio utaratibu mzuri.

Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba ataje tu watu wanne watakaotoka taasisi fulani ikishafika kule yeye mwenyewe ataweza kuwateua.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa 44 kifungu cha 15 kinazungumzia leseni. Tunashukuru kwamba hivi sasa sheria imeweka wazi kuwa nani atatoa leseni ya utalii. Hapo nyuma kulikuwa na vurugu mechi kubwa kila taasisi ukenda ukitaka leseni unapata, lakini hivi sasa sheria hii imeweka ni nani anaweza kutoa leseni hiyo. Pia imepunguza usumbufu wa kuweza kuzunguka taasisi nyingi kwa kutaka leseni moja, nadhani sasa hivi sheria imeweka wazi kama utalipa ada na ukifuata masharti yaliyokubalika basi unaweza ukapata leseni hiyo bila ya matatizo.

Kwa hivyo, napongeza kwamba na hili Mhe. Waziri na watendaji wake wameliona ndio maana wakalipendekeza hivyo. Hili likishakaa sawa basi watu wengi wataweza kuekeza ikiwa ni wazalendo ama watu kutoka nje.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchngia kuna kifungu kimezugumza juu ya hawa wawekezaji kuchangia shughuli za maendeleo katika vijiji ni jambo zuri na wapo wengi wanachangia, lakini ninachoshauri mimi sio vibaya sasa hivi tukaainisha katika sheria ili tukaweza kupata tija zaidi. Kwa sababu kwanza kuchangia mtu ni hiari yake inawezekana mtu akaweka mradi wa mamilioni, lakini utakuta kwa mfano kuchangia madawati mawili katika kijiji yeye huwa

anapata tija kubwa kuliko lile alilolichangia.

Mimi nilikuwa nashauri labda hapa tungetumia asilimia kama mtu ataweka mradi wa milioni mia moja basi asilimia tano achangie kwenye kijiji ama asilimia kumi achangie kwenye kijiji. Hapa kwanza wana kijiji watapata kunufaika zaidi lakini naye atajua jukumu lake kuliko kukaa akawa anatumegea mwenyewe leo kidogo na kesho kidogo. Nadhani tukiweka kwenye sheria kwamba mradi unaoanzia shilingi milioni mia moja ama mia mbili basi asilimia kumi itakuwa ni mchango wa wana kijiji katika maendeleo mbali mbali. Tena wana kijiji wakipata fedha zile watatizama kipi cha msingi maji, skuli, zahanati hilo watapendekeza wenyewe. Hii itakuwa nzuri kwanza na yule muwekezaji mwenyewe atapata kujiandaa kwa kutoa mchango wake, lakini tukikaa mtu ukawekeza mamilioni yaliyokuwepo halafu anasaidia watu bati 12.

Mhe. Spika, pia itakuwa yale malengo ya kuchangia maendeleo ndio yamekuwa lakini hayakufikia kule yanakohitajika. Sasa ushauri wangu mimi kama itawezekana kisheria basi tungetizama kwenye asilimia kama kuna mradi unaoanzia kiasi fulani cha fedha basi aambiwe yule muekezaji achangie kiasi fulani cha asilimia ili wananchi waweze kunufaika. Huu ndio mchango wangu katika sehemu hiyo ya maendeleo katika kijiji.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kuchangia nije kwenye tafsiri ukurasa wa 38, hapa nilikuwa nataka ufafanuzi katika mambo mawili. Jambo la kwanza muongoza utalii.

Mhe. Spika, muongoza utalii naomba ninukuu halafu baadae nitoe wasi wasi wangu. “Muongoza watalii nasema kwamba maana yake ni mtu anayetoa taarifa kufahamisha, kuelekeza watalii kwa malipo kuhusu maeneo, uoto, utamaduni, uasili, jiografia, historia na mambo yanayofanana na hayo”.

Mhe. Spika, mimi sina tatizo lakini sasa katika kutembeza watalii huyu aliyetafsiriwa hapa nilikuwa nataka nitoe maelezo halafu labda Mheshimiwa Waziri atakujanambia ni sawa sawa nilivyofahamu ama sivyo.

Mhe. Spika, watalii wanaokuja hapa wanakuja kwa fani mbali mbali, wengine wanakuja wanasikia mji wetu ni wa urithi wa kimataifa. Kwa hivyo, wanakuja wauone mji wa Zanzibar uko vipi. Ndani ya huo mji wenyewe ndio una mambo mbali mbali mna masoko ya kuuzwa watumwa. Ukenda katika masoko ya kuuzwa watumwa kuna mtu rasmi yuko pale anatoa taaluma ile kwa mgeni, lakini hapa nilivyofahamu mimi huyu anatoka nae mgeni pengine hoteli ama popote alipompata anakwenda nae sehemu ile. Sasa je yule mtu ninayemkuta pale akatoa maelezo anaitajwe yeye ni jina hili hili ama lina tofauti.

Mhe. Spika, la pili ni kwamba wageni hao hao wanakwenda katika maeneo mbali mbali ya kihistoria. Kwa mfano anaweza kwenda Kizimkazi huko kuna msikiti wa mwanzo kabisa pamoja na pango la Mwanamize. Hao wanaokwenda kule wanakuwa wameshajua kuyaeleza yote yale huwa wanapata taaluma ama wale waliokuweko kule ndio wanaoeleza haya.

Pia na hilo nilitaka nilitambue kwa sababu nimepata utata kidogo. Mimi nimeshakwenda Jozani nilipofika nimepokewa pale nikakuta wataalamu wakanitembeza lakini sikutoka na mtu yeyote mjini, kwani watalii wengi sasa hivi hutoka na watu huku huku mjini wanakwenda kuwatembeza katika maeneo tofauti. Wasi wasi ilikuwa ni je hawa wanaokwenda kuwapeleka huwa wanasomeshwa historia ya nchi yetu yote ili wanapokwenda kule watoe maelekezo yanayofaa ama wakimfikisha kituoni anakuwa yupo mtu anayeweza kuwapa taaluma hiyo. Nilikuwa nataka nielezwe kwamba huyu ni sawa sawa na huyu aliyetangazwa hapa kwenye sheria au pana tofauti. Kama pana tofauti nitaelezwa kama ndiye huyo huyo pia nitaelezwa.

Mhe. Spika, suala jengine kwenye tafsiri ni kwamba kuna chombo cha baharini pale kimeelezwa kwenye tafsiri naomba ninukuu. “Maana yake ni chombo kinachosafirisha baharini kilichoundwa kukidhi viwango vilivyokubaliwa na kamisheni kwa ajili ya huduma za kulala na chakula kwa watalii wa kiwango ambacho kinategemea muda na kuwepo katika chombo hicho”.

Mhe. Spika, mimi sina mashaka lakini sasa utaratibu wa vyombo viko vingi. Kwa mfano, ukenda hapa Forodha mchanga au sayansi ya baharini utakuta pana vyombo pale wanapanda watalii wanaokwenda Ng’ambu kwenda kuangalia makobe na vitu vyengine. Lakini mle huwa hawalali wala mle hawali labda kunywa maji tu, huwa wanakwenda halafu wanarudi. Pia hivi sasa ukenda Kiwengwa utakuta watu wanatembezwa kwa ngarawa hutumia tanga huwa wanakwenda huko halafu wanarudi pia mle hawali wala hawalali. Vile vile wengine huwa wanapenda kuvua wanaweza wakapanda boti wakafunga mitego yao kila wakenda kasi wanarambaza na wanapata samaki.

Je, katika tafsiri hii na hilo limeingia ama liko fungu gani? Pia nimepata utata kidogo katika tafsiri lakini na mambo yanavyokwenda. Ningemuomba mheshimiwa akija hapa anifahamishe na hata ile ngarawa wanaopanda kutembezwa kule Kiwengwa iko katika fungu hili au hawa forodha mchanga kutoka pale kwenda kutizama makobe wako kwenye tafsiri ile.

Mhe. Spika, mwisho kabisa katika mchango wangu kwa sababu tayari nilikuwa nataka nitie barka tu. Nije katika mawazo kijumla katika suala zima la utalii.

Mhe. Spika, kwa kuwa utalii hapa petu sasa hivi ndio sekta kiongozi, naomba na mimi nitoe michango miwili ili wizara kama inahisi itasaidia basi waweze kuuchukua na kuweza kusaidia kupata mafanikio haya.

Mhe. Spika, wataalamu wanasema mtalii wa daraja la kwanza ana kazi kubwa mpaka akapatikana, na mtalii wa daraja la kwanza si hoteli tu Kempiski ama Lagema. Lakini nasikia mtalii wa daraja la kwanza anahitaji kujua kila kitu tangu anapoanzia *airport* kujua uwanja wetu uko vipi au kama atakuja kwa kutumia bandari anataka kujua bandari yetu iko vipi, miundombinu yetu iko vipi mpaka anafika kwenye hoteli yenyewe.

Mimi ningelishauri kwa kuwa mtalii wa daraja la kwanza ndiye anayetia kipato kikubwa katika nchi, ningeliomba na hayo serikali ingeliangalia kuanzia uwanja wetu wa ndege pia zinaweza kuja ndege zikatosheleza kwa muda ule unaotakiwa. Kwa sababu nasikia zikija ndege tatu tu kwa uwanja wetu basi itabidi kwanza tufunge isije ndege nyengine kubwa mpaka zile ziondoke kwani hata hiyo *parking* yenyewe ni ndogo. Naomba na hili kwa kuwa tunahitaji kipato na kipato kikubwa kinatokana na utalii baada ya zao letu la karafuu kuja hali ya chini. Hili serikali ingelilichukulia jitihada ili kama watalii wanataka ndege sita basi zote zikae pale watembee halafu warudi. Kuliko kupangiwa zamu leo njooni tatu, keshokutwa tatu inakuwa biashara imechanganya lakini wenyewe tunaizuia. Naomba na hili serikali yetu ilitizame pamoja na hiyo miundombinu ya barabara na hayo mahoteli yenyewe. Mhe. Spika, hayo yote yakiangaliwa basi tutafikia kwenye yale malengo.

Mhe. Spika, suala la pili ambalo pia wenzetu wawekezaji wanalitumia nahisi nalo linapunguza mapato ni kwamba utakuta leo hoteli itaitwa *MANTARIF* mnaekeana mikataba, mnampa msamaha pengine wa mwaka inategemea na sheria inavyosema. Akimaliza muda wake wa majaribio anamwita mwenzake anaibadilisha jina inaitwa *MANTARIF LODGE* nae anapata mwaka, akimaliza na yeye pia anaitwa mwengine anaita jina lake *MANTARIF* sasa itakuwa kile kipato cha serikali kinapungua. Naomba na hili litizamwe kwa sababu wenzetu wafanyabiashara sio wote lakini wengine huwa ni wajanja. Jambo hilo huwa wanalitumia nimetoa mfano kwa hoteli hiyo lakini ziko hoteli nyingi akimaliza muda tu anampa mwenzake anabadilisha jina halafu anafanya biashara.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa katika yote ni kwamba watalii wa ma-group ambao pengine wanatoka Italy wanakuja hapa inakuwa mambo yao yote yanafanywa kule kule huku wanakuja kutembea. Pia na hili lingefuatiliwa ili tukaweza kupata takwimu nzuri tukapata fedha ambazo ni sawa sawa na wale watalii waliokuwepo. Hapa pia nahisi pana ujanja unakuwa unatumika. Ningeliomba yote hayo niliyoyabaini na kuyapendekeza kwa wizara wangeliyafanyia kazi kwa lengo kukuza utalii wetu na kuongeza kipato chetu.

Mhe. Spika, narejea tena kuunga mkono mswada huu kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini kwa asilimia mia moja. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ingawa sina mchango mkubwa, lakini nimeamua na mimi nitoe maelezo mafupi kuchangia mswada huu. Nadhani sheria ya kwanza ambayo tunaifuta kwa mswada huu tuliipitisha katika Baraza hili na kwa sababu inaonekana kwamba sheria ile sasa imepitwa na wakati na kwamba kuna haja ya kuunda sheria ambayo itatilia nguvu zaidi kazi za utalii nimeona na mimi nitoe maoni kidogo katika sheria hii.

Mhe. Spika, kwanza nikija kwenye sehemu ya kwanza ya utangulizi kwenye tafsiri ya biashara ya utalii ambayo hii ni sehemu ya pili tu kwenye tafsiri hizi. Mstari wa tatu kutoka chini kwenye kifungu hiki maana yake ni biashara ya utalii inayotoa huduma kwa watalii na mambo mengi lakini hapa chini kuna wakodishaji baskeli, kuna vyombo vya moto, vyombo vya baharini, vyombo vya michezo vya baharini kwa watalii. Mimi nilitaka nitoe ushauri tu kwamba wakodishaji baskeli hapa inaonekana kwamba ni maneno yanayojitegemea wenyewe. Lakini vyombo vya moto, vyombo vya baharini hayo vile vile ni maneno yanayojitegemea wenyewe.

Kwa hivyo, kama tunataka tuiweke kwamba ni wakodishaji wa baskeli, wakodishaji wa vyombo vya moto basi hii sentensi tungeitengeneza ikasomeka hivyo. Vyenginevyo tukichukulia vyombo vya moto vyote nayo ni sehemu ya biashara ya utalii, nadhani itakuwa kidogo tumekwenda nje ya matakwa ya mswada huu. Hilo lilikuwa ni la kwanza.

Mhe. Spika, jambo la pili nililoliona ni kwenye kifungu cha 5 ambacho kinazungumzia Bodi ya Wakurugenzi. Kwenye Bodi ya Wakurugenzi kwenye kifungu cha 5(2d) wajumbe wengine wasiozidi wanne watakaoteuliwa na waziri na kati yao wajumbe wasiozidi wawili kutoka sekta binafsi zinazohusiana na mambo ya utalii. Mimi wasi wasi wangu katika kifungu hiki ni kwamba tumekiweka kuwa hakiko wazi sana, maana yake Baraza hili kutunga sheria ya kujua kwamba kwenye Bodi ya Utalii hatujui idadi ya wajumbe, lakini ni waziri tu ambaye ndiye atakuwa anajua kwa sababu ni mamlaka ya kuteua. Sisi wajumbe ikawa kila mara tuulize bodi ina wajumbe wangapi, hili naona ni tatizo. Nadhani tungelikuwa *specific* tukajua bodi yetu itakuwa na wajumbe wangapi, na kati ya hao kama wanatoka sekta binafsi wajulikane inatoa watu wangapi.

Katika kifungu hicho hicho 2(c) mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambaye ni daktari anayetambulika. Inawezekana iko mantiki kwa waziri kupendekeza hivyo kwamba mjumbe mmoja awe ni daktari kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Lakini sisi tulikuwa tunaomba sana tuangalie kwamba kazi kubwa ambazo zimetajwa za biashara hii ya utalii ni pamoja na kuendeleza utalii wa kimazingira. Utalii wa kimazingira ni ushauri mzuri wa kuendeleza sekta hii lazima utatokana na watu wa fani za kimazingira.

Nilitaka waziri atufahamishe huyu daktari kakusudiwa kwamba ata-*play role* katika kutoa ushauri kwenye nyanja hii au anateuliwa kwa sababu ya shughuli nyengine zaidi za kitalii. Kama daktari huyu hakusudiwi huko mimi nilikuwa nikifikiria kwamba kwa madhumuni ya kutekeleza utalii wa kimazingira ambao kwa kweli ndio wenye umuhimu katika uchumi wetu, basi mtu mwenye sifa ya utaalamu wa mazingira ndio watu wa kupendekezwa katika bodi hii.

Mhe. Spika, nilipokuwa nasema kwamba wajumbe wa bodi hapa bado hawajakuwa *specific* na hatujawafahamu kwa sababu sentensi inasema wajumbe wengine wasiozidi wanne. Kwa maana hiyo waziri anaweza akateua kuanzia mtu mmoja mpaka wanne, ni matakwa ya waziri anaweza akasema kuna mtu mmoja, anaweza akasema kuna wawili hatuna uhakika kwamba kweli atakwenda kwenye watu wanne. Basi kama inasema wasiozidi wanne angalau basi tungeweka maneno wasiopungua kadhaa tukajua kwamba angalau waziri ana-*range* na hiyo *range* isiwe kubwa kiasi ambacho ya kumpa usumbufu waziri ateue wangapi ama azidishe, mimi nadhani tungelikuwa *specific* katika hilo.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 5(7) ni kwamba mjumbe yeyote wa bodi atapoteza sifa za kuwa mjumbe iwapo hatohudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya idhini ya mwenyekiti au makamo mwenyekiti. Mimi nadhani hili neno au hapa likitumika kama lilivyo basi maana yake watu wote wawili hawa mwenyekiti au makamo mwenyekiti wamepewa *role* ya wajumbe wale kuwaandikia maana yake nikitaka mimi naweza nikamuandikia mwenyekiti au nikitaka naweza nikaomba ruhusa kwa makamo mwenyekiti kwa hili neno au ninavyoliona hapa.

Nadhani kwa utaratibu mzuri wa kiongozi bora kazi hii angelipewa mwenyekiti. Kama mwenyekiti atakuwa hayupo basi itakuwa makamo mwenyekiti ndiye aliyekuwa na *role* itajulikana, lakini hapa mimi nadhani au inaweza ikatuletea matatizo. Kwa sababu hapa inaleta *choice* ama idhini ya mwenyekiti au makamo mwenyekiti. Naweza nikamtumia makamo mwenyekiti na hii haitokuwa sifa nzuri ikawa wote wawili wapo lakini nikaomba ruhusa kwa makamo mwenyekiti na isiwe mwenyekiti.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha (b) mstari mwengine unaofuata iwapo ataonekana na kuthibitishwa kuwa na matatizo ya akili. Hii nakubaliana nayo lakini ugonjwa wa akili sio matatizo tu ya kiafya, nadhani ionekane kama tumekusudia ugonjwa ambao hawezi kufanya kazi au awe na matatizo ya kiakili. Leo hatunaye hapa Mwanasheria Mkuu lakini akili yake iko timamu, lakini hatunaye kwa muda mkubwa tu je mjumbe wa aina hiyo katika bodi yuko nyumbani kwake amelala akili yake iko timamu lakini hawezi kufanya kazi bado aendelee kuwa ni mjumbe wa bodi hiyo. Mimi nadhani hapa ingeonekana kwamba kweli ni matatizo ya kiafya pamoja na akili.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 6(c) kwenye kazi za bodi hii nilitaka kuitilia nguvu tu kwamba imesisitizwa utalii wa kimazingira, kwa hivyo, mimi sina tatizo.

Mhe. Spika, lakini ukija kwenye kifungu cha 9 ambacho kinaelezea mikutano ya bodi. Mikutano ya bodi hii kwenye kifungu cha 9(4) akidi ya kikao ni nusu ya wajumbe ambao walioteuliwa kwa wakati huo. Mimi ndio ilikuwa ikinipa shida hapa itakapokuwa imeruhusiwa ile wasiozidi wanne lakini waziri akateua mtu mmoja, lakini mwengine akawa ni mkurugenzi mkuu anaingia kwa wadhifa wake, mjumbe mwengine ni kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na huyu mwenyekiti ambaye ameteuliwa na Rais kwa hivyo kutakuwa na watu watatu wanaoingia *portfolio* zao lakini pengine kutakuwa na wajumbe wawili tu ambao amewateuwa waziri kama itabakia kama hivi ilivyo. Kwa hivyo, akidi hapo nusu yake wanaweza wakawa ni hao watu wenye *portfolio* tu wakawa wapo pale, wakaja watu kwa *portfolio* zao ndio wana-*compose* bodi kwa sababu ni watatu. Waziri ameambiwa kwamba hawatozidi wanne atakaowateua akiteuwa tuseme watatu awe kasoro mmoja tu basi *still* watatu hawa watakaokuwa na *portfolio* zao ikawa ndio wana-*compose* bodi. Mimi naiona hiyo bodi haitokuwa na nguvu hasa za kufanya kazi. Itakuwa ni watu wenye *portfolio* wamekuja kwa kazi zao.

Pia tusisahau watu wenye *portfolio* hawana mchango mkubwa sana kwa bodi zaidi ya mambo ya ushauri kuliko wale wajumbe ambao wanateuliwa ambao kazi yao kubwa itakuwa ni kushughulikia mambo yale ya bodi. Kwa hivyo, ni la akidi vile vile ilikuwa ni sababu ambayo inatilia nguvu ya kwamba huku wajumbe wajulikane kwamba *specific* ni wajumbe wangapi ambao watateuliwa.

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa nikikisoma hicho hicho cha 9(6) kwenye ukurasa wa 42 bila ya kujali masharti ya kijifungu cha 4 cha kifungu hiki iwapo kikao hakitofanyika kutokana na kutopatikana akidi, bodi itafanya kikao katika tarehe inayofuata na wajumbe waliohudhuria itakuwa ndio akidi ya kikao na

watakuwa na uwezo wa kuendesha shughuli za kikao hicho.

Vile vile *statement* hii mimi niliona ina matatizo kwa sababu kama leo watakuwa hawakutimia hiyo *quorum*. Halafu msingi wa kutimia *quorum* ni kwamba hao waliopo hawana maamuzi ndio msingi wake. Lakini siku ya pili watu hao wakikaa sasa watakuwa wana maamuzi kwa kweli mimi inanipa mashaka. Kwa hivyo, inakuwa ule msingi hasa wa *quorum* hapa hatukuutimiza. Kwa hivyo, bado na kama kesho itakuwa hawapo maana yake mimi sioni ule umuhimu wa kwamba ikiwa leo hawakutimia wasubiri kesho wale wale waliokuwa hawakutimia wakifanya itakuwa wana maamuzi. Mimi nasema twende katika misingi ya kidemokrasia hasa ya vikao, na misingi ya kidemokrasia ya vikao ni kupata *quorum* kwa ajili ya kupata maamuzi.

Sasa kama kutakuwa na wajumbe hawatimii hawa wa bodi, hawaji katika kikao *quorum* yao haitimii, mimi nadhani itakuwa ni watu ambao wanasema hawawezi kufanya kazi basi wawekwe watu ambao watakuwa wapo wa kufanya kazi, lakini tukifanya hivi kwamba leo hawakutimia kesho walale wafanye kazi itakuwa tumeuvuka msingi mkubwa wa *quorum* za vikao ambao ni msingi mkubwa wa *participation* ya vikao ambalo ni suala la mijadala ya kidemokrasia.

Kifungu cha nane kidogo kwenye hiyo hiyo Bodi, kwa mujibu wa sheria hiyo bodi itajiwekea utaratibu wa kuendesha vikao vyake kwa kadiri itakavyoona inafaa. Sijui kama huu ni utaratibu wa kawaida wa bodi zetu, kwamba sisi tutunge sheria lakini bodi nyengine inaweza ikapanga pengine vikao vine kwa mwaka, lakini bodi nyengine tukaiwacha kuwa *flexible* iende ikakae ipange hata vikao 20 kwa mwaka. Kama huu utakuwa ni utaratibu wa msingi wa bodi zetu, basi mimi sina matatizo, lakini kama huu sio msingi wa uendeshaji wa bodi zetu mimi nafikiri bado bodi ingekuwa *controlled* kwa sababu vikao si vikao kwa maana ya kujadili maneno tu, lakini ni vikao kwa ajili ya kutumia fedha ambazo ndio msingi wa Baraza hili kujadili zinakwenda vipi.

Kwa hivyo, ingekuwa ni busara sana kama tulivyoweka *limit* katika mambo mengine na vikao hivi vikawa na *limit* zake. Mimi sipendi kupendekeza kwamba viwe ni vikao vingapi kwa sababu shughuli za bodi itakuwa wanazijua wao wenyewe ikiwa ni pamoja na wizara, lakini tusiiwache bodi ikawa kesho ikikohowa inataka kikao, keshokutwa inataka kikao, keshokutwa tena ajenda haikutimia inataka kikao.

Vikao vya bodi vitakapokuwa vingi kamisheni haina kazi, itakuwa kamisheni shughuli zake za utendaji wa kila siku zote zimehamia kwenye bodi, na hii nayo ina matatizo. Kwa sababu bodi ina misingi yake ya kufanya kazi na kufanya kazi kujua sera zinakwenda vipi, kuna mambo ya kupokea ripoti za

fedha na hivi ni vikao ambavyo vinakuwa vina utaratibu wake. Kwa hivyo, tusije tukaipa bodi nafasi kubwa ya kufanya vikao mpaka ikatawala shughuli za kila siku mpaka ikaonekana kwamba hakuna haja hata ya kuwa na kamisheni. Mhe. Waziri nadhani hapa angelijaribu kui-*frame* vyengine ili ikatutoa wasi wasi huu.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 11, Mkurugenzi Mkuu na Wafanyakazi, kifungu 11 (3) kutakuwa na Wakurugenzi wa Idara Kuu za Kamisheni ambao watateuliwa na bodi. Hapa mimi nakubali, lakini tulipokuwa tunazungumzia uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu halafu ikazungumziwa uteuzi wa Katibu wa Bodi humu tumeweka sifa humu. Kwa hivyo, suala la sifa lisije kwa wale maafisa wawili tu, lakini suala hili lije vile vile kwa wakurugenzi wa vitengo. Kwa hivyo, maelezo haya yakibakia kama yalivyo kutakuwa na wakurugenzi wa idara ambao watateuliwa na bodi, basi bila ya kui-*qualify* ya kwamba huo uteuzi utakaofanywa na bodi utazingatia nini naona nalo hili ni tatizo.

Kwa hivyo, mimi ningependekeza hapa sentensi hiyo iendelee na uteuzi huo utazingatia sifa za kielimu za kitaaluma na uzoefu wa kazi katika shughuli hizo, nadhani ikiwa hivyo angalau sisi tunapata ile *hope* kwamba bodi itakapokuwa inakaa nayo itafuata misingi ya uteuzi kwa mujibu wa masharti maalum ambayo ni muhimu sio tu kwa mkurugenzi, sio tu kwa katibu, lakini vile vile kwa wakurugenzi wa sekta mbali mbali, vyenginevyo bodi inaweza ikakaa wakamteuwa mtu rafiki yake kutoka wapi anakuja lakini kuna mzoefu wa mambo ya utalii, mwenye sifa za utalii, mwenye elimu kabisa keshafanya kazi, lakini mkurugenzi wa bodi akasema kuna mmoja huko anafaa zaidi kuliko huyu. Mimi nadhani haya mambo lazima tuyaweke vizuri.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 12 hapa sina tatizo kubwa isipokuwa ni tatizo la uandishi. Kifungu cha 12 Mfuko wa Fedha za Kamisheni, 12(2)(d) fedha nyengine zitakazokusanywa kwa njia ya misaa, labda hapo limesahaulika neno da, kwa hivyo likiongezwa itakuwa ni miaada.

Kifungu cha 17 kutoa upya leseni. Kuna maelezo hapa yanasema ‘baada ya kamisheni kupokea maombi ya utoaji upya wa leseni, mimi nilikuwa napendekeza kwamba baada ya kamisheni kupokea maombi ya utoaji wa leseni mpya kuliko utoaji upya wa leseni. Inaweza kuidhinisha leseni na hili neno ‘inaweza’ hili, hili ni neno moja ambalo sisi huwa hatulipendi, kwa matatizo gani? Tumekuwa tukizungumzia sana mambo haya ya leseni namna yanavyopoteza muda, masharti umeshatimiza, malipo ushatoa, lakini mtu kupata leseni azungushwe nenda huku kuna bwana mmoja hajatia saini, leo mkurugenzi kenda wapi hajapatikana, afisa huyu hajapatikana, sasa hii inaweza ikiwekwa hapa ndio inayopalilia mambo haya.

Mimi nasema kama masharti yametimia tuwaambie tena kwa muda kwamba leseni itatolewa si zaidi ya wiki moja na kama kuna matatizo kama mtu hajapata leseni asema kuwa sijapata leseni lakini masharti yametimia. Nadhani tukiweza kuiunda sheria ya aina hii itakuwa inaweka *control* ya maafisa nao kutumia vizuri yale maraca yao hasa kwa kuzingatia masuala ya *time*, kwa sababu mara nyengine unakamilisha masharti lakini bado unazungushwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 19 kwenye kutembeza watalii.

Kifungu 19(b) kinasema:

"Biashara ya kutembeza wageni imetengwa kwa Wazanzibari'.

Sasa ni Wazanzibari wote, Wazanzibari wakaazi au Wazanzibari gani hapa? Lakini hapa tumesema kuwa ni Wazanzibari ukija ukifungua kwenye kifungu cha 24, kinasema biashara zifuatazo zimetengwa kwa ajili ya Watanzania, kule kuna Wazanzibari hapa kwa ajili ya Watanzania. Kwenye kifungu hicho hicho cha 24(1)(g) waongoza utalii wenye sifa ya chini ya kifungu cha 11(b) ya sheria, hapa biashara zifuatazo zimetengwa kwa ajili ya Watanzania, kule kwa ajili ya Wazanzibari. Mimi nafikiri tungeiweka hii kuwa *specific* ijulikane ni vipi.

Wazanzibari ni Watanzania, lakini kama hivyo ndivyo, kwa nini huku mwanzo imewekwa *specific* kwamba biashara hii ni kwa ajili ya Wazanzibari ni kwa sababu tumewa *qualify* ni Watanzania wepi ambao tunataka wa-*participate* na kilio cha Baraza hili Mhe. Spika, tusisahau tunazungumzia namna ambavyo vijana wetu wa Kizanzibari waliomaliza skuli hatuna pahala pa kuwapatia kazi. Sasa leo uwanja huu ukiukunjua ni uwanja mdogo sana huu, ukiukunjua kwa Watanzania kilio hiki cha Wazanzibari kwamba hata shughuli ndogo ndogo za kutembeza wageni kwa hivyo, tumeziondosha mikononi mwa vijana wetu na hii itakuwa ngumu baadae, itakuwa tunapiga kelele lakini haina faida.

Mimi nasema ziko kazi ambazo tunawahitaji ndugu zetu wa Tanzania, watu wenye ujuzi wao, wenye sifa zao za kielimu, yawezekana zilizo tofauti na walizonazo vijana wetu hatuwakatai, lakini kwenye kazi hizi ndogo ndogo ambazo nahisi *taxi driver* sijui nani ukazifanya kwamba hizi nazo ni kazi za kila mtu zinaweza zikaleta mashaka yake hasa kwa nchi ndogo kama hii na moja ni hili suala la kutembeza wageni.

Mhe. Spika, nimeona katika kifungu hiki kuna maneno matatu yametumika yakionekana kama yana maana moja. kwa mfano, hapo kifungu (b) kuna kutembeza wageni, lakini ukija kifungu 20(1) kuna kuongoza watalii na kuna pahala nimeona vile vile kutembeza watalii, kutembeza wageni, kuongoza

watalii na kutembeza watalii. Mimi nasema haya matatu yote tutafute mooja tu liwe linafanya kazi kuliko yote. Kwa sababu mimi nikiwa na wageni wangu ukanikuta huko Kiwengwa je, mimi utaniita kuwa natembeza watalii au wageni? Kwa hivyo, suala la wageni na watalii ni lazima tulipe tafsiri.

Huku kwenye tafsiri kuna tafsiri ya watalii hakuna tafsiri ya wageni. Kwa hivyo, ni lazima maneno haya matatu yaunganishwe litumike moja badala ya kuyatumia kuongoza watalii, kutembeza watalii au kutembeza wageni, ili lisije likatupa shida wakati kukitokea matatizo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa mimi nimeusoma mswada huu na ni kwa sababu ni mswada unaorekebisha sheria kwa ajili ya kuunda sheria mpya ambayo inasimamia shughuli iliyo muhimu katika uchumi wetu, naona ni mswada ambao umekuja kwa wakati unaohitajika sana. Mimi natapa nimpongeze Mhe. Waziri kwa ku- *respond* haraka sana kwa sheria ambayo tumeitunga lakini ikawa inalega lega katika kuongoza shughuli zetu za kiutalii. Jambo hili nadhani lingekuwa ni la kuigwa kwa wizara zote, tusiwe tuna sheria kila siku ambazo zinaleta *complication* katika utendaji wetu.

Na mwisho kabisa nilitaka nizungumze suala pengine halimo katika mswada huu lakini linahusiana na mambo haya ya utalii. Katika fukwe zetu hizi tumekuwa tukipiga kelele sana juu ya namna ambavyo tunatoa vibali vya ujenzi wa hoteli za kitalii lakini halafu kukawa kuna migongano baina ya shughuli za kiutalii na shughuli za wananchi. Nadhani haya ni mambo yanayoendelea bado. *Concern* yangu kubwa sana ni ufukwe huu mkubwa, kwa Zanzibar nasema huu ndio ufukwe mkubwa. Hoteli tayari zinaanza kujengwa jengwa, ukipita chini huku unaona hoteli zinajengwa nyengine ni nzito, kama palikuwa hapana hoteli pale panaanza kuporomoka mmong'onyoko ule unavyoonekana namna ambavyo ardhi inavyoliwa, leo pakiongezewa uzito wa majengo kama yale najuwa mporomoko utakuwa ni mkubwa zaidi. Kwa hivyo, pamoja na kuongeza shughuli zile za ujenzi wa mahoteli pale, lakini ni vyema watu wa mazingira wakatanguliza fikra hizi za namna ambavyo wanaweza wakaepuka ile *soil erosion* ambayo sasa itakuwa inakwenda kwa nguvu sana.

Lakini suala jengine ni kwamba zile zimejengewa kwa ajili ya watalii na watalii wengi hapa pamoja na utalii wa ndani lakini ni wenzetu wanaotoka nje. Wakianza shughuli za pale za kiutalii na wananchi ambao ufukwe ule wanautumia kuliko popote kwa shughuli zao za kiafya, Mhe. Waziri yazingatiwe mapema sana, isije mwishowe kwa sababu ya kujengwa hoteli ikajakuwa sasa sehemu hii hapa inafungwa hakuna tena shughuli za watu kupita na kufanya shughuli zao za afya, tunataka utalii uimarike lakini tunataka na afya za watu ziimarike. Watu wengi sana katika maeneo ya mjini hapa hata wanaotoka Pemba wengine Dar es Salaam wakifika hapa wanautumia ufukwe

huu kwa ajili ya shughuli zao za kuimarisha afya zao. Kwa hivyo, pasije pakawa na maingiliano katika mambo haya.

Jambo la kuzingatia lililo zuri sana ni kwamba kama utungwe utaratibu hoteli zile zinazojengwa na majumba yale yatafika mpaka wapi kutoka sehemu ya bahari. Hilo lina umuhimu sana Mhe. Spika, kwa sababu yapo majengo siku nyingi yalikuwa yamejengwa pale, lakini hayana kero kwa sababu masafa kutoka kwenye bahari mpaka yaliko majengo yanakuwa hayaharibu yale mazingira wala hayawakeri watu wengine kufanya kazi, lakini pakiingia mambo ya biashara atakuja mzungu kaka hoteli aseme nataka kwenda chini kupumzika sasa, basi ataambiwa mfanyabiashara yule kaleta kitega uchumi kwa hivyo tunampa ruhusa ya kwenda kukaa pale akapumzishe watalii.

Mhe. Spika, hili litatuletea matatizo na nasema nilitangulize kwa sababu leo tunazungumzia mswada ambao unahusiana na shughuli hizi ili kuitanabahisha serikali iwe na mazingatio ya mapema sana kabla mambo hayajaharibika katika sehemu zile.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mswada huu mimi nauunga mkono moja kwa moja kwa sababu sioni tatizo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Nashukuru Mhe. Spika, nami kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu mdogo tu katika mswada huu. Lakini kabla sijatoa mchango wangu niseme kwamba mswada huu nauunga mkono mia kwa mia nikiwa na imani kwamba yale nitakayoyazungumza basi Mhe. Waziri atayafanyia kazi.

Mhe. Spika, lakini pia nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri. Nakumbuka katika kitabu chake cha bajeti kama sikosei kifungu cha 4(1) au 4(2) alisema kwamba, mswada huu uko katika hatua za kwa Makatibu Wakuu, utakwenda Baraza la Mapinduzi na baadae atauleta na kweli ahadi ile ametimiza leo tumeuona mswada huu.

Katika mswada huu wasi wasi wangu Mhe. Spika, utoaji wa leseni kwa maduka ya utalii, baa na upigaji wa disko. Naona sheria hii tayari inafanana na sheria ya taasisi nyengine. Nakumbuka kulikuwa na mvutano baina ya Kamisheni ya Utalii na Idara ya Sanaa kuhusu utoaji wa vibali vya kupiga disko pamoja na ngoma za kienyeji. Utalii wanasema sisi tunayo sheria ya kutoa, lakini Idara ya Sanaa nao wanasema na sisi tunayo sheria ya kutoa. Mvutano ukawa mkubwa mpaka ikafika pahali tukafanya kikao cha pamoja nakumbuka kikao kilifanyika Bwawani kwenda kuzungumzia jambo hili.

Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa marehemu Omar anasema mimi ninatakiwa nichangie shilingi milioni nne kwa mwaka sasa kama sikutoa vibali hivi pesa hizi tutazipata wapi. Kamisheni ya Utalii inasema nyinyi natoa kibali cha kupigwa madisko watalii wanahamaki wanakwenda zao tunapoteza milioni 60 kwa mwezi, sasa milioni zako nne kwa mwaka na zetu 60 kwa mwezi zipi nyingi? Lakini ukitizama sheria zote zinafanana. Sasa ili tusilete mgongano baina ya taasisi mbili za serikali nafikiri ni vizuri Mhe. Waziri atapokuja kutengeneza kanuni basi afafanue ni maeneo gani ambayo Kamisheni ya Utalii itatoa leseni ili na hawa Idara ya Sanaa na wao wajue maeneo gani watatoa vibali.

Nakumbuka katika kikao kile tulifikia pahali tukasema basi maeneo ya hoteli yote yanayolaza watalii ndio Kamisheni ya Utalii itoe vibali, na maeneo mengine ya harusi au madisko yanayopigwa nje ndio Idara ya Sanaa itoe kibali, lakini pia haikutusaidia kitu. Sasa ni vizuri Mhe. Waziri akaangalia, kwa sababu utoaji wa leseni za maduka ya utalii tayari Halmashauri za Wilaya na Manispaa tumeshawanyang'anya mapato, upigaji wa disko na ngoma za kienyeji tayari Idara ya Sanaa tushawanyang'anya mapato, sasa ni vizuri atapotengeneza kanuni aliangalie hili ili taasisi zetu hizi zisiwe zinagongana gongana katika utoaji wa leseni hizi.

Mhe. Spika, kwa sababu ukiuchukulia utalii hata ukienda Bawe Araju hapo kwa kuwa napiga kidumbaki basi watalii wengi wanakwenda kufuata kidumbaki. Sasa hali kama ile ndio kutakuwa na mvutano sasa Manispaa itoe kibali au Kamisheni ya Utalii. Kwa sababu watalii wanakwenda pale ndio nasema ni vyema katika kutunga kanuni tuliangalie hili vizuri.

La pili Mhe. Spika, kama sikosei katika cha waziri alisema Kamisheni ya Utalii kwa mwaka itakusanya karibu shilingi milioni 813.8 katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Lakini nimetizama mswada huu sijakuta pahali katika pesa hizi kama kuna *retention* wameiomba. Sasa naona hapa Mhe. Spika, huyu ng'ombe kama hakupewa chakula atatoaje maziwa? Biashara unayotangaza ndio inayotoka, Kenya baada ya uchaguzi utalii wao uliharibika lakini walitenga karibu dola milioni 80 kuutangaza utalii tu, sisi tumeanza kupata misukosuko hapa Balozi wa Marekani anasema Zanzibar kuna fujo wasende watalii, sasa kama hatukuutangaza vizuri huu utalii kweli hawa watalii tutawapata?

Sasa ningeliomba Mhe. Waziri anambie sijui kama haina haja kutia katika mswada atatia kwenye kanuni lakini kuwe na *retention* angalau ya kuweza kuutangaza huu utalii. Kuna vipeperushi wanataka kufanya, kuna mikutano wanataka kwenda, kuna majarida wanataka kuyatayarisha, sasa kama hawakupata pesa za kufanyia hayo sijui tutautangaza vipi utalii au ndio tutakuwa kila siku tukamwite mtu bwana wala hakuelekea akaombe wizarani.

Sasa nafikiri hili la *retention* tungeliangalia. Kwa sababu sisi lilitupa shida.

Mkoa wa Kusini tulipoamua tuulinde utalii tulikusanya askari polisi, askari wa kamisheni, tukachukau mpaka JKU, Valantia watusaidia katika ulinzi wa utalii, tulikuwa na askari karibu 35. Sasa tumeweka kambi pale askari wanataka kula, Kamisheni ya Utalii haina pesa ikabidi tuzungumze na wenye mahoteli watusaidia angalau kuendesha zile kambi, tumeiendesha kambi ile kama mwaka mmoja tu na wale wameshindwa basi kambi tumevunja, wakati tulipoweka kambi tulipata mafanikio makubwa sana ya kulinda utalii wetu. Sasa nafikiri ni vyema serikali ingefikiria kutoa *retention* katika hizo shilingi milioni 813 ambazo watakusanya kuwapa kidogo za kuweza kuulinda na kuutangaza utalii.

Jengine Mhe. Spika, kuna sehemu inazungumzia kwamba kuna kazi Wazanzibari watafanya, hili kwa kweli ni zuri. Kwa sababu hivi sasa hawa wenye mahoteli wana magari yao wanachukua watalii ambapo kazi ile ilikuwa ni ya wazalendo, lakini hao wenye mahoteli wameanzisha bendi zao, madisko yao wakati hizo ni kazi za wazalendo, sasa sijui sheria hii ndio itaanza kuwabana kuwaambia sasa nyinyi hamtoweza kufanya haya isipokuwa kazi hizi wafanye wazalendo, hapo nasema wamefanya vizuri sana.

Kama nilivyosema Mhe. Spika, kwamba sina mchango mkubwa isipokuwa niolitaka kusema yale ambayo nimeona niyaseme. La mwisho halimo katika mswada huu lakini naomba Mhe. Waziri anisaidie.

Jana nimepigiwa simu kutoka Jambiani Kibigija, wanasema kuna mwekezaji ameamua kujenga ukuta kutoka fukweni kwenye hoteli yake kwenda baharini mita 70, na anajenga ili kuwazuia wananchi wasiingie katika eneo analosema lake kwenye *beach*. Sasa limeleta utata wananchi wamekuja juu sijui kama ana kibali au anajenga tu, leo ilikuwa niende lakini kwa sababu ya kikao hiki ndio sikupata kwenda. Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri atume watu wake wende wakatusaidie. Kwa sababu kama huyu mzungu keshaamua kua mpa *beach* kuwa ni yake ajenge kuta azuie mpaka mita 70 baharini ndani itakuwa hatari. Wananchi wanaweza wakachukua sheria wakenda kuvunja yakaja yakatokea mengine. Basi nimuombe sana Mhe. Waziri alifuatilie kupitia *ZIPA* ama Kamisheni ya Utalii ili tuzuie hilo lisitokee.

Baada ya hayo nilisema sina mchango mkubwa Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia ahsante.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, nami kupata nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa utalii. Kwanza niwapongeze watendaji wote wa wizara hii kwa kuleta mswada huu na sisi kupata kuuchangia.

Mhe. Spika, mimi naomba kuanzia suala la biashara ya utalii. Kama ilivyozungumzwa katika ukurasa wa 37 na kuidhinishwa baadhi ya vitu vingi ambavyo vinahitajika kulipiwa kodi na biashara hii ya utalii. Mimi ningependekeza kwa maoni yangu kwanza wakae na baadhi ya wafanyabiashara ili kuwapa taaluma zaidi vitu gani vinavyohusiana na biashara ya utalii na biashara hizi tulizokuwanazo. Kwa sababu baadhi ya wafanyabiashara utakuta mara nyingi vitu vyao vinakuwa mchanganyiko, mtu anauza mashine za boti au boti na ndani ya duka lake anauza nguo vile vile ambapo ni tofauti na biashara zile za kitalii zinakuwa ni biashara mchanganyiko. Kwa hivyo, ningependa wapewe taaluma wafanyabiashara hawa ili wasije kupambana na yale masuala ya kuwa biashara yake ya utalii imechanganyika na biashara nyengine.

Kwa hivyo, kama tutafanikisha hayo naamini tutakwenda vizuri. Kama inavyoeleweka biashara ya utalii ni nyingi sana na ipo nyingi ambapo kama itasimamiwa na kuangaliwa zaidi itaingiza mapato mazuri ndani ya sekta hii ya utalii.

Mhe. Spika, ukurasa wa 39 kuitangaza Zanzibar kuwa ni kituo cha utalii. Kwa kuwa sasa hivi sehemu ya utalii imekuwa ni mpango mkubwa ambao unataka kutayarishwa na serikali yetu ili kuleta mapato na kufanya vijana wetu kupata ajira kwa hivyo kuna mbinu nyingi za kuutangaza utalii. Kuna mbinu za kutumia ngoma zetu za asili, kuna mbinu za kutumia michezo ya aina mbali mbali ambayo inafanywa na wananchi wetu hapa, na ikiangaliwa vizuri itakuwa ni kivutio kikubwa kwa sekta hii ya utalii. Kuna maeneo mengi ambayo tukiyatumia yataleta kivutio kwa sekta hii ya utalii.

Mhe. Spika, kwa mfano, kipindi cha nyuma nilitembelea baadhi ya mikoa Bara, ukipita sehemu zile za *roundabout* huwa wanaweka kama TV fulani na ile huwa wanaonesha sana mambo ya utamaduni wao au mazingira ya nchi yao. Kwa wenzetu Bara huwa wanatumia sana kuonesha wanyama, kwa hivyo na hapa petu tuna nafasi ya kuonesha mambo ya utamaduni au wanyama tuliokuwanao katika zile sehemu muhimu zinazotembelewa sana kama *roundabout* zetu hizi zilizokuwepo Malindi, *Ng'ambo Station*, pia tuna *roundabout* nzuri tu iko Mombasa. Pindipo tukiweka vivutio hivi pia vitashawishi kwa wageni wetu kutembelea maeneo yale na kuona mambo tuliyokuwanayo ya utamaduni na wanyama mbali mbali katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile kama tulivyokuwa tunaona hapa maeneo yetu ya Forodhani mara nyingi vivutio vingi huwa vinafanyika pale na kunakuwa na wageni mbali mbali na viburudisho vingi, ngoma mbali mbali, kwa hivyo

baadhi ya wageni wetu wengi wakitembelea maeneo yale wanavutika. Ningeiomba wizara ikaangalia zaidi maeneo ya baadhi ya vijiji vilivyokuwa tayari sasa hivi vimeshawekezwa mambo ya utalii vikafanya mikusanyiko kama ile iliyokuwa inafanyika Forodhani na kule wakaweka masuala kama yale ili kupata kivutio zaidi kwa wageni wetu kutembelea maeneo kama haya.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa 42 kifungu cha 5 naomba kunukuu.

Kifungu cha 5:

> "Kutaanzishwa kitengo maalum cha ulinzi wa utalii chini ya Kamisheni ambacho kitakuwa kikifanya ulinzi katika maeneo ya utalii kwa watalii na mali zao".

Mhe. Spika, hii ni muhimu sana. Kwa kuwa tunaanzisha masuala ya utalii kwa hivyo kuwa na ulinzi katika maeneo ya utalii ni kitu muhimu sana. Lakini mpaka sasa hivi kuna matatizo katika haya maeneo ya kitalii ni maeneo ambayo yameingiwa na wageni wengi na watu mbali mbali huwa wanashiriki katika kufanikisha masuala yao mbali mbali ya kimaisha. Pindipo kama kutakuwa na ulinzi uliokuwa mwepesi tu ambao utakuwa hauna silaha nzito, hii itahatarisha maisha ya wageni wetu na watalii wetu wanaotoka sehemu mbali mbali.

Kwa sababu kama inavyoeleweka sasa hivi baadhi ya sehemu nyingi za kitalii wale wahalifu wakiingia katika maeneo yale huwa wameingia na silaha nzito ya kivita. Kwa hivyo, kama tutaanzisha ulinzi wa silaha nyepesi kama rungu au silaha ndogo ndogo tutakuwa tunawapa mwanya wale wahalifu wanaotoka sehemu mbali mbali.

Kama inavyoeleweka sasa hivi tuna wageni kutoka nchi mbali mbali, wengine wanakuja kwa nia nzuri na wengine wanakuja kwa nia mbaya. Sasa pindipo ukianzishwa ulinzi huu ningependekeza uangaliwe vizuri na uwe ulinzi wa uhakika kwa sababu maeneo yetu yamekuwa kivutio kikubwa kwa wageni mbali mbali wakija wanapendelea kutembelea katika mahoteli yetu haya.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa 45 kifungu cha 20 "Waongoza watalii". Mhe. Spika, kuna haja sana ya waongoza watalii wakawa ni watu ambao kuna kitengo maalum cha kuangalia afya zao na utendaji wa shughuli zao za kimaisha na vipi wataziweza shughuli zile za uongozaji watalii au kufanya kazi katika mahoteli ya kitalii.

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tunapata habari kwa waongoza watalii kuwa baadhi yao wengine huwa sijui tuseme wanafyetuka au wanakuwa na akili pungufu, mtu akikasirishwa kidogo tu katika hoteli huwa wanachukua hatua

mikononi mwao kufanya hujuma au kuharibu vifaa mbali mbali vilivyokuwemo katika mahoteli ya kitalii. Au kati ya hao wengine wanaotembeza wageni wa kitalii, huwa ukakamavu wao hauridhishi kulingana na kuwatembeza watalii. Kwa hivyo, ningeomba wizara hii ikawa na kitengo maalum kuwapima afya zao, ili tunaowaajiri pale kwa shughuli ile ya kuwatembeza watalii ambao ni tegemeo la taifa wakawa ni watu wa uhakika angalau kila miezi mitatu au sita wakawa wanapimwa afya zao.

Mhe. Spika, kwa sababu kama tutakuwa hatuna watu wa uhakika kama nilivyoeleza, ikiwa yanatokea matukio mbali mbali tu ya hujuma katika mahoteli kwa hivyo hii itasababisha kuwakimbiza watalii. Ni vyema kuwepo kituo hicho cha watendaji katika sekta kama hizo wakawa wanapimwa. Kwa mfano leo utamchukua mtu kumpima kabadilika akili na wakati wageni wapo kibao kwa kipindi kifupi tu utakuta hii inawakimbiza.

Kwa mfano, mtu anafanya hujuma ya kuharibu vitu au kutia moto kwa hivyo hili litakuwa sio jambo zuri. Au kwa mfano mmoja mdogo tu, leo unamuajiri mtu hasira ndogo tu anakwenda kujitia kitanzi maana yake nini, kafanya kosa gain? Mhe. Spika, ningeomba sana katika kitengo hiki cha kitalii hawa wafanyakazi wakawa wanapimwa afya zao, wasikabidhiwe tu moja kwa moja bila ya kuchunguzwa.

Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu mia juu ya mia kuletwa hapa ili kuuchangia kwa maslahi ya taifa letu mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati, Ardhi na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza naunga mkono mswada huu lakini hata hivyo mchango wangu sio mkubwa.

Mhe. Spika, ningependa nianze na ukurasa wa 37 sehemu hii ya "Askari wa Utalii". Mhe. Spika, sote tunakubali kwamba watalii kuishi kwa amani wanapofika katika nchi yoyote wanayokwenda ni jambo la lazima. Kwa hivyo, kuwepo na kitu kama hiki ni jambo muhimu. Lakini nimejenga wasi wasi hasa kufuatia mchango wa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini ambapo kidogo amelielezea namna gani walivyoanzisha suala zima la ulinzi kwa watalii na hatimaye kati kati ikashindikana.

Kwa sababu hapa inaonekana zilikuwa ni juhudi zake mwenyewe Mkuu wa Mkoa na watendaji wake. Sasa hapa imeonekana tu kuanzishwa kwa askari hawa wa utalii, hatujui askari hawa Mhe. Waziri aje kutwambia watatokana miongoni mwa askari wastaafu, vijana wadogo ambao watapewa trained maalum kwa suala hili. Lakini nani atawalipa? Hili ndio la muhimu.

Mhe. Spika, Mkuu wa Mkoa alishindwa kwa sababu wenye mahoteli walisaidia lakini hatimaye baadae nao wakashindwa na kule hili suala likafa. Kwa hivyo, hapa ni vizuri tukalielewa nani atasimamia suala hili, nani atawalipa vijana hawa, nao watapatikana wapi. Ni vizuri tukawa na vijana shababi wenye uwezo, sio tunakwenda kuweka askari ambao tayari wameshafikia miaka 60 ndio anakwenda kuwa mlinzi kwenye taasisi hizi. Lakini ulinzi wenyewe nadhani vile vile hawa askari wasiwe askari marungu, wanatakiwa wawe na nyenzo, wawe na usafiri, wawe na silaha.

Mhe. Spika, jambo jengine ukurasa huu huu ni suala la "Biashara ya Utalii", hapa kuna maeneo ya kufugwa wanyama, mafugio ya viumbe wa baharini na kadhalika. Hili la viumbe wa baharini sina tatizo nalo, lakini hili la kufugwa wanyama. Mhe. Spika, mtalii anapokuja hapa Zanzibar maana yake anakuja Zanzibar. Kwa mfano, Zanzibar hatuna asili ya ngamia, Zanzibar hatuna asili ya simba, Zanzibar hatuna asili hata ya farasi. Lakini unapoweka ngamia, unapoweka simba katika maeneo ambayo labda tuseme ni ***zoo*** ile, mtalii anapokuja kuangalia ngamia si kitu cha Zanzibar, akiangalia simba kama utaweza kumuweka sio kitu cha Zanzibar. Kwa hivyo, sawa kuwepo kwake kwangu mimi sioni kama kutakuwa na umuhimu.

Kwa yale maeneo ambayo wamesema mafugio ya viumbe wa baharini hili ni sawa. Kwa mfano, ukienda Nungwi kule kuna sehemu pale wapo kasa watalii wanakwenda wanaingia mle wanapiga nao picha, hili linakubalika kwa sababu ni la Kizanzibari, kasa wapo hapa Zanzibar mtalii anapata fursa na ile kumbukumbu ya kwamba alifika Zanzibar, Zanzibar kuna kasa amepiga nao picha, amecheza nao, kama kuna samaki pale. Sasa hili sina tatizo nalo, hili ni zuri na ni vyema likaendelea.

Mhe. Spika, jengine ukurasa huu huu kuna "Duka la Kitalii". Kwa mfano, kuna vitu kama vinyago, zawadi za ukumbusho, vitu vya zamani, kumbukumbu za safari za kutembea Zanzibar. Mhe. Spika, hivyo kinyago kile cha Kimasai kinampa kumbukumbu gani mtalii kwa Zanzibar? Mhe. Spika, mkoba kama huu mzuri kama wangu umeshanifahamu. Huu imetokea tu leo kuja nao, Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame ndio briefcase yake. Lakini mkoba kama huu mtalii akinunua unambakishia kumbukumbu. Mhe. Samia Suluhu Hassan anautazama eeh! Unampa kumbukumbu kwamba kweli hii ni sanaa ya Zanzibar.

Lakini kinyago kile cha Kimasai kachukua na mkuki haimpi kumbukumbu yoyote kwamba alikuja Zanzibar, inampa kumbukumbu kwamba alikwenda Umasaini Arusha sio Zanzibar. Kwa hivyo, nadhani na hili tuliangalie tuone kama kweli linaleta maana yoyote.

Mhe. Spika, hili bahati nzuri uliliona na ulilizungumza kidogo hapo kwa utani pale waziri kivuli alipokuwa akisema kama wawakilishi wa Unguja wakienda Pemba au wa Pemba kuja hapa, lakini ulilitolea ufafanuzi kwamba kuna ule utalii wa ndani. Kwa hivyo, haya maelezo yanatakiwa yarekebishwe. Kwa mfano, kipindi kinachozidi masaa 24 lakini pungufu ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, sasa hivi tumekuwa tuki-*encourage* utalii wa ndani. Sasa utalii wa ndani leo ukitoka hapa ukenda Jozani pale pengine utatumia masaa matano unarudi hufiki yale masaa 24. Kwa sababu utalii tunajua ni neno lenye asili ya Kiarabu, ni kujifunza kwa kuona, kujifunza kwa vitendo. Sasa hebu hii tafsiri ningemuomba Mhe. waziri aiangalie upya na baadae aone tunarekebisha nini hapa hasa tukizingatia utalii huu wa ndani.

Si hapa tu Mhe. Spika, utalii wa ndani. Hata wenzetu pale Bara sasa hivi ndio wanazungumzia zaidi utalii wa ndani. Hivyo hivyo hapa sisi kwetu kuna haja hiyo. Kwa hivyo, nadhani tuangalie lugha gani ya kutumika zaidi hapa.

Mhe. Spika, jambo jengine kwenye ukurasa wa 38 unasema "Taarifa kwa |Watalii" maana yake ni eneo ambalo limetayarishwa kwa ajili ya kutoa taarifa kwa watalii. Mhe. Spika, bahati mbaya mimi sijakuwa miongoni mwa watalii, lakini kwa kuzingatia utalii wa ndani mwaka jana na wewe mwenyewe ulikuwa ni shahidi nadhani. Tukiwa Arusha na timu yako ya Baraza tulipata fursa ya kwenda pale Manyara, lakini kabla ya kwenda kwenye zile mbuga tukafika pale kuna eneo kuna vituo vyao pale, pale unapewa maelezo ya kutosha juu ya mbuga ile iko vipi, wanyama gani waliokuwemo.

Hivyo hivyo, nakumbuka mwaka juzi tulikaribia kupanda mlima Kilimanjaro lakini tulirudi. Tulikwenda tukafika mpaka kituoni pale mwanzo, pale tulipewa maelezo juu ya namna mlima ule na taratibu zake za kupanda na kadhalika. Sasa, kwa hapa Zanzibar tunapokuwa na jambo kama hili ambalo tumeliandika hapa sijui ni eneo gani?

Kwa mfano, unawapeleka watalii Jozani watu watapata maelezo ya msingi, pale Jozani kwenyewe au kabla ya pale. Unawapeleka watalii kwenye spice tour kwa mfano, hapa ni eneo kubwa sana, ni wapi watapata yale maelezo ya msingi kwanza. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa pengine sikufahamu vizuri tu, lakini pia ningependa Mhe. Waziri aje anifahamishe zaidi juu ya vituo vya kuogelea, maana yake ni eneo la kujifunza kuogelea, sehemu za kuogelea na maeneo mengine yanayotoa huduma za kuogelea na kuzamia kwa watalii. Sasa mimi sijalielewa vizuri, sijafahamu hasa nini wamekusudia.

Mhe. Spika, jengine kwenye hili la waongozaji watalii. Mhe. Spika, waongozaji watalii ni watu muhimu sana. Nadhani waongozaji watalii wapo wazuri tu wenye kujua lugha vizuri, wanaeleza ile *history* au jambo lolote vizuri. Sasa ni vizuri hawa watalii wakapewa nafasi kubwa lakini pia wanatakiwa wawe wenyewe wale waongozaji watalii hata *dressing* zao ziwe nzuri. Ingawa watalii wako wa aina nyingi, kuna watalii wengine wanakuja wahuni wahuni na wao hapa, siajabu na wao wakipata wale waongozaji wahuni ndio wanakubaliana. Lakini waongozaji wengine ni wazuri na lazima waendelee kuwa hivyo na hata *dressing* zao ziwe zenye kupendeza.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa huu wa 39 kifungu (m) naomba kunukuu.

Kifungu (m) kinasema kwamba:

> "Kuitangaza Zanzibar kuwa ni Kituo cha Utalii".

Mhe. Spika, hili ni jambo muhimu tena ni muhimu kupita yote. Hivi sasa na mara nyingi hasa uchaguzi unapokaribia kumekuwa na wenzetu sijui nani, ama ndani ya nchi au nje ya nchi, wamekuwa wakifanya kazi hiyo, sio ya kuitangaza Zanzibar kiutalii lakini kuitangaza Zanzibar kwamba ni eneo hatari halifai kwenda kwa watalii. Hata hivi sasa kazi hiyo inafanyika na ndio maana sasa hivi utakuta watalii wengi wame-*cancel* kuja Zanzibar kwa sababu inaonekana kwamba Zanzibar ni eneo hatari, haliendeki, halikaliki kitu ambacho sio cha kweli.

Sasa hii kazi ya kuitangaza Zanzibar sio tu tusubiri wakati ule lakini tuone ile *counter check.* Sasa hivi lazima tutoe taaluma hii kwamba jamani Zanzibar haiko hivyo inakwendeka, inakalika, inapumzikika, kila aina ya starehe unaipata hapa hakuna wasi wasi huo. Siajabu kwenye viwanja vya ndege vyengine nje ya nchi, unakuta Zanzibar ni hatari hakwendeki. Sasa katika suala zima la kuitangaza Zanzibar kiutalii tufanye na *counter check* kwa wale wenzetu ambao wanaitangaza Zanzibar kuwa si sehemu salama.

Mhe. Spika, jengine labda ningependa kujua tu, nadhani mwaka jana kulikuwa na maonesho pale Afrika Kusini yanayohusiana na *Zanzibar Shell*, sijui yale yakoje na Zanzibar ama imeshirikishwa vipi au inashiriki vipi katika maonesho yale ya *Zanzibar Shell.* Kama wenzetu pale Afrika Kusini wamekuwa na kitu kama hicho lakini sisi wenyewe hapa Zanzibar tunalielewa vipi na tunashirikiana nao vipi wale wenzetu pale.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mchango wangu mimi si mkubwa lakini kwenye ukurasa huu wa 40 kifungu (2) (d) naomba kunukuu:

Kifungu (2) (d):

> "Mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Afya ambaye ni daktari anayetambulika".

Mhe. Spika, daktari anayetambulika tukisema hivyo mimi sifahamu ni daktari wa aina gani, ni *dentist*, ni *gynaecologist* au wa fani nyengine. Sasa sijui kwa sababu daktari anayetambulika awe na sifa gani ndio awe daktari anayetambulika. Sasa hebu tungepata ufafanuzi.

Lakini vile vile katika sehemu hii ya Bodi ya Wakurugenzi ni vizuri miongoni mwa wajumbe wa bodi hii ya wakurugenzi mmoja wa wajumbe wake akawa ametoka miongoni mwa hawa wenye mahoteli, awe anawakilisha kundi la hawa wenye mahoteli.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo pia Waziri Kivuli pale alilizungumza kwenye ukurasa huu wa 42 kifungu cha 11 (2) kinasema:

Kifungu cha 11 (2):

> "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu mpaka awe na sifa zifuatazo:
>
> (a) awe ni mwenye taaluma angalau ya Shahada ya Kwanza au inayolingana nayo na uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka mitano."

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri alizungumza kwamba haikusema hapa ni elimu ya aina gani, ingawa kwenye namba 2 (b) imezungumza kidogo awe na uzoefu wa mambo haya ya utalii. Lakini ni vizuri ikawa *specific* basi huyu Mkurugenzi awe ni mtu ambaye ana taaluma ya kiwango hicho cha elimu katika fani ya utalii. Nadhani ingekuwa ni vizuri zaidi kwa sababu atakuwa anafanya mambo, anazungumza mambo, anakosoa mambo katika fani ambayo ameijua juu chini.

Mhe. Spika, la mwisho labda si pahala pake hapa au sikuona. Kwa sababu tumezungumzia utalii sijaona kama kuna sehemu ambayo imezungumzia wafanyakazi katika sekta ya utalii, vipi wafanyakazi watalindwa na sekta hii ya utalii?Kwa sababu sasa hivi wafanyakazi wote katika sekta ya utalii wako *fifty fifty* hajui saa ngapi atafukuzwa, anaweza akaamka leo asubuhi akenda kazini na akafika kule kazi basi. Kwa hivyo, hili sijaliona humu, nadhani Mhe. Waziri kwa ninavyomjua kwa busara zake na hawa wafanyakazi ni shemeji zetu, watoto wetu, wake zetu, waume zetu, sasa lazima tuwajengee mazingira mazuri ili wawe na uhakika mtu anapokwenda kazini basi awe na ile imani ya kazi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nadhani ingawa hili pengine hata wizara yangu inahusika, tumekuwa mara nyingi tumeweka ile mimi si mtaalam wa mazingira, lakini tusema majengo haya ya utalii yawe karibu mita 30 kutoka ufukwe wa bahari. Lakini nadhani tufike pahala tuliangalie upya jambo hili. Sasa hivi bahari inakula ardhi lakini maeneo yote ambayo yamejengwa karibu na bahari imekuwa yamepata stara.

Kwa mfano, Mambo Msiige pale jengo lile liko mita chache sana, bora niseme liko baharini kwa sababu hata maji yanapiga pale, lakini kwa sababu ukuta wake umejengwa madhubuti limeweza kuzuia maji kuja juu. Kimsingi ukiangalia kutoka hapa hospitali ya Mnazi Mmoja, Ikulu pale mpaka unafikia Taasisi ya Baharini kule ujenzi wake uko baharini kabisa na umesaidia bahari kutokuja huku. Lakini yale maeneo ambayo ukiangalia yamefuata hizo taratibu bahari imepata fursa ya kuja huku.

Kwa mfano, hoteli ya Maruhubi kwenye Chuo cha Utalii pale huko nyuma minazi ilikuwa mbali kule. Lakini kwa sababu hakuna kizuizi pale maji ya bahari yameweza kuja huku. Kwa hivyo, nadhani hili hebu tuliangalie upya, Mhe. Waziri hebu ungekaa na wataalam wetu wa ardhi tulipatie maelekezo ya kutosha.

Hata juzi tulipokuwa kwenye semina huku na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kule Bwejuu nilikuwa na Profesa Ali Denge Makame asubuhi tukifanya mazoezi pale nikawa naangalia. Kuna majengo mengine ambayo yamekiuka taratibu hizo yakawa karibu kabisa yakajengwa sijui pengine mita 10. Bado yamesaidia kupunguza bahari kuja juu. Sasa nasema hili Mhe. Waziri hebu tungekaa tukashauriana tuone, vyenginevyo bahari itaendelea kuja huku juu.

Mhe. Spika, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono mswada huu mia juu ya mia.

Mhe. Spika: Nakumbusha tu ile Kamati ya Fedha na Uchumi watakutana mara baada ya kutoka humu ndani. Lakini pili sina jina la muombaji yeyote kuchangia hapo jioni. Kwa ujumla na nikisisitiza hasa wale wenye nia ya kuja kuchangia tufike mapema kama inavyowezekana ili tuendelee na shughuli hii ya mswada huu. Baada ya hayo, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11: 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuipata nafasi hii muhimu ya kuchangia Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar nambari 9 ya mwaka 1999 na kutunga Sheria ya Utalii ya Zanzibar na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, maafisa mbali mbali wa Kamisheni ya Utalii, kwa kuhakikisha kwamba hivi sasa umefika wakati ambao unastahiki kwamba Kamisheni yetu ya Utalii iwe na uwezo na iwezeshwe ili iendelee na iweze kujitegemea katika fani zake za kukuza utalii hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, hapa kwetu Zanzibar tunaamini kwamba kwa asilimia kubwa sana tunategemea utalii na serikali kwa upande mzima inategemea pato lake litokane na utalii na kuweza kufanya mambo yake mbali mbali ya kuharakisha maendeleo katika nchi yetu. Pamoja na hayo Mhe. Spika, wadau wakubwa wa sekta hii au Kamisheni hii ya Utalii ni wananchi pamoja na wafanyabiashara wa nje na ndani na wataalamu wetu mbali mbali tuliokuwanao, ili kuhakikisha kwamba utalii unaimarishwa nchini kwetu na serikali ihakikishe inatafuta masoko katika nchi mbali mbali kutoka nje ili ongezeko la watalii liongezeke katika nchi yetu.

Mhe. Spika, bila ya taaluma nzuri na bila ya mipango mizuri zaidi, basi nasema kwamba kitu chochote kinachopangwa kinaweza kisiende. Naamini taalum ikiwa nzuri ya watendaji wetu na ikienda vizuri kwa wananchi wetu na kuelekezwa katika nchi za nje basi utalii wetu utakua kwa kasi na ongezeko lake litapatikana na tija itapatikana. Kwa sababu tija yetu kubwa tunayoizungumza hapa Mhe. Spika, ni kuhakikisha kwamba watalii wanaotoka nje wanakuja kwetu kwa wingi na kile sehemu ambayo inawezekana kupatikana watalii, basi wapatikane na waje kwetu kwa manufaa ya kusaidia nchi yetu hii ya Zanzibar na kwa ujumla kuwasaidia wananchi wetu ambao kwa asilimia kubwa ajira yao iko katika sekta hii ya utalii.

Mhe. Spika, Zanzibar ni sehemu ya visiwa Mwenyezi Mungu alivyotujaalia, lakini kwa bahati mbaya huko tunakotoka tulikuwa tunajiona kama tumo katika msitu ambao hatujui faida yake. Kwa mfano Mhe. Spika, kama tukielekea ukanda wa pwani, sehemu za Kaskazini Mashariki na Kusini Mashariki basi asilimia kubwa ya mwitu wetu ulikuwa unalimwa mtama au mahindi, viazi vikuu, muhogo, pilipili hoho au pilipili kichaa. Mimi nilikuwa mdogo lakini

Mhe. Spika nilishuhudia. Wakati huo tulikuwa hatujui kuna nini, kumbe Zanzibar ni sehemu yenye utajiri mkubwa, lakini tulikuwa hatuna taaluma wala hatujafumbua macho wakati huo tulikuwa bado tumelala usingizi.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri baada ya miaka ya 1980 hivi serikali kwa makusudi ilipoanza kusema tu kwamba iingie katika sehemu ya utalii, lakini naamini wakati ule ilikuwa mwanzo mgumu, tulikuwa tumeingia vizuri lakini hatukujua faida yake kwa baadhi ya wengine, ikatokea fursa kwa wageni kuja katika maeneo mbali mbali na kuanza kusema tunataka maeneo haya na serikali ikatoa kwa nia njema tu wala sio nia mbaya. Baada ya kuja kushtuka visiwa vyetu vya Zanzibar hivi sasa vinatangazwa na vizuri sana na wageni wanaokuja kutembelea hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Spika, kitu kikubwa Mwenyezi Mungu alichotujaalia katika nchi yetu ni kwamba hatuna wanyama wa pori kama Bara, hatuna wanyama wa kuvutia ukiwacha hapa kwetu ukiacha Kimapunju. Lakini Mwenyezi Mungu ametujaalia rasilimali katika Afrika ya Mashariki na Kati, naweza kusema kwamba Zanzibar ni sehemu nzuri ya utalii na tukiangalia mandhari yake inapendeza. Bahari yetu na fukwe zetu Mhe. Spika, ni sababu tosha ya wageni kuja kwa wingi katika nchi yetu na kuitangaza kwamba Zanzibar nendeni mkatembeeni, kuna kila mandhari nzuri katika fukwe zetu na bahari yetu.

Mhe. Spika, katika bahari kuna wazungu ambao wanakwenda ku-*dive*, hawa *diving* wakifika kule wao wanaangalia ile hali halisi iliyokuwepo, samaki ya kuvutia, matumbawe mazuri na mambo mengineyo Mhe. Spika. Pia ukitaka ufurahi zaidi kama ni kipindi cha shwari, basi mgeni yeyote anayekuja kule anajiona kama kalala kwenye bahari, kumbe bahari ile ikichafuka ni hatari. Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, kwamba Zanzibar tuna bahati kubwa ya visiwa vyetu kuwa na mandhari nzuri ya utalii.

Mhe. Spika, jambo kubwa la kukuza utalii ni kutoa taaluma nje ya nchi na jambo kubwa la kukuza utalii ni kuwaelimisha wananchi. Mimi naamini mambo mawili hayo yakienda sambamba, kama wanavyojitahidi wenzetu wa kamisheni, basi uwezo wa serikali yetu na uwezo wa wizara yetu ya utalii na kamisheni yenyewe basi ongezeko kubwa litapatikana, ninaamini kuwa mapato yatapatikana zaidi katika kuhakikisha kwamba utalii ni sehemu moja wapo ya kuhakikisha kwamba fedha za kigeni zinapatikana ili kuendesha nchi yetu na kuleta kila faraja katika maendeleo ya kila siku.

Mhe. Spika, kama tutatembelea nchi za wenzetu wana vyombo vingi sana vya utalii. Kuna haya majahazi ya asili ya zamani ambayo ni ya kisomali, yana kama nakshinakshi ya Washihiri. Yale majahazi Mhe. Spika, Dubai ni mengi sana, nafikiri wenzetu majahazi yale huwa ni kivutio kwa wageni na huwa ni

changamoto la kupata faida kwa wale vijana wao wanaofanyakazi katika sehemu zile. Kwa hivyo, niseme tu kwamba na sisi kwetu hapa Zanzibar tumebahatika tuna vyombo vyetu vya asili, ukiacha boti zetu zinazosafirisha wageni na mambo mengineyo. Pia ngarawa zetu nazo ni faraja kubwa sana kwa vijana wetu wanapata ajira zao za kuweza kuwasaidia katika kupata ajira na kusaidia maendeleo ya sekta hii ya utalii.

Mhe. Spika, fedha ndio msingi wa maendeleo na bila fedha Mhe. Spika, huna maendeleo. Kwa hivyo, niseme tu kwamba wenzetu kwa kuangalia hoja hiyo ndio wakasema kwamba ni vyema tukaanzisha mfuko wa fedha kwa ajili ya Kamisheni ya Utalii. Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri, naipongeza serikali kwa kuhakikisha kwamba suala hili ni muhimu na litawasaidia sana wenzetu hawa kufanyakazi zao na kuhakikisha kwamba wanakwenda wanakotaka kwa maslahi ya kutafuta masoko na kuielekeza Zanzibar katika kuitangaza vizuri juu ya kukuza utalii katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mfuko huu naamini utachangiwa vizuri na wenyewe watakuwa na sehemu zao wanazopata kodi zao. Kwa hivyo, mimi nakubali moja kwa moja kwamba mfuko huu uwalenge wenye kamisheni ya utalii na usimamiwe vizuri, ninaamini kwa watu waliokuwepo ni watu wa kuchacharika katika maisha, basi utakwenda vizuri na utasaidia sana katika kuleta maendeleo kwenye shughuli zetu mbali mbali za kuitangaza nchi yetu na mambo mengineyo.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hii ya serikali ya kuhakikisha kwamba inatafuta kila sehemu ambazo zinamuelekeo wa kupata utalii katika nchi yetu. Pia kuna mambo mengine ambayo yatatusaidia sana katika sehemu hizi. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kupitia Kamisheni ya Utalii na asaidiwe na watu wanaohusika na mambo ya historia ya nchi yetu. Kuna mapango mengi sana katika nchi yetu Mhe. Spika, kama yatahifadhiwa vizuri, naamini serikali inajitahidi na yataendelezwa vizuri kwa faida ya wageni wetu wanaokuja kutembelea katika nchi hii, basi Mhe. Spika, faida itapatikana na ongezeko zaidi la watalii wataongezeka.

Namuomba Mhe. Waziri kwa kupitia kwako Mhe. Spika, wenzetu wageni wanaokuja hapa hasa hawa wazungu waliopita huko nyuma au wanaokuja sasa hivi na wengineo basi wana kumbukumbu zetu nyingi sana za nchi za Afrika ya Mashariki au katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mimi nitowe mfano mmoja Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba wenzetu hawa wanajitahidi kuwa na kumbukumbu nyingi za nchi yetu, lakini sisi wenyewe hatuzijui. Mara baada ya kujenga hoteli hizi za Kiwengwa, kuna hii hoteli ya sasa hivi wanaita *Going*. Zamani *Sea Club, Franco Roso* lakini siku hizi wanaita *Going*. Mhe. Spika, nakuhakikishia zamani lilikuwa ni pori kubwa,

ukenda mpaka juu huko karibu ya Kituo cha Polisi kilichokuwepo pale Kiwengwa. Wakati huo sisi tuliokuwa tukiishi kule tulikuwa tunakunywa maji ya visima tu, kumbe huku juu kuna chemchem kubwa sana, yaani kuna pango lina maji mazuri na ni matamu na ni mengi sana tulikuwa hatujui. Wazungu baada ya kujenga hoteli yao walikuja na ramani zao twende hapa pana hichi na kweli walikigundua.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri maji yale yanafaida kwa wananchi wote bila ya matatizo. Naipongeza serikali yanapotokea matatizo madogo madogo mbio wameshafika ili kuhakikisha faida ile inapatikana kwa wananchi bila ya matatizo. Lakini nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba kwa kuwa wazungu wamegundua mambo mengi na wanazidi kuyagundua mengi zaidi, au wageni wanagudua mambo mengi. Tusiseme wazungu tu, pengine hata waswahili. Mhe. Spika, naamini kama tutawatumia vyema kwa kuwaambia tutafutieni mambo mbali mbali ya historia basi tunaweza kufanikiwa zaidi katika kukuza utalii wetu.

Mhe. Spika, kuna wenzetu Tanzania Bara wamebahatika wana mambo makubwa matatu, kwanza wana mlima Kilimanjaro, pili wana mbuga za wanyama kubwa na tatu wana mapango ya ajabu. Mapango ya ajabu yako kule kwetu Tanga Mhe. Spika, tulifika na mwenzangu Mhe. Haji Omar Kheir, nilimchukua akenda kutembea kidogo Mhe. Spika.*(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Spika, mimi ningeomba sana Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii kwa kupitia kwa watendaji wake mbali mbali waliokuwa nao, basi waende kuangalia hili pango moja la ajabu linaloitwa pango la amboni. Mhe. Spika, kila miujiza ya Mwenyezi Mungu aliyokuwanayo mwenyewe anayoweza kuifanya basi imo humo. Ndani unaingia kwa tochi, maana ukienda hivi hivi basi huoni. Kwa bahati mbaya Mhe. Spika, unaweza kupotea bila ya kujua ulipoingilia na ulikotokea kama huna mwenyeji. Mule ndani maajabu yake muna baridi ambayo ni kama muna AC, yaani ni kama hapa ukumbini tulipo.

Pia kuna vitu Mhe. Spika, vya ajabu katika mapango yale, kuna alama za meli, kuna alama za sijui niseme ndovu au tembo, kuna alama za mtoto mchanga yaani mtoto kama anazaliwa anachukuliwa, kuna alama za simba, sio yule simba sport club lakini ni simba huyu mla watu. Kuna alama nyengine nyingi za ajabu. Mimi nakuomba Mhe. Spika, kama tutapata nafasi baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, au kama Mwenyezi Mungu atatujaalia siku ya kuzindua ule umeme wetu wa kutoka Tanga kwenda Pemba, basi kama utakuwa uwezo upo basi na wajumbe wako wangeshiriki.

Mhe. Spika, nakuomba sana siku hiyo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuungana na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tuhudhurie kwenye kitu kikubwa cha historia ambapo Pemba kwa muda wote huo wamekosa umeme. Kwa hivyo, utakapozinduliwa basi Baraza lako sio vibaya kwenda kule tukashuhudia pamoja na yeye Mhe. Rais.

Mhe. Spika, naiomba serikali suala hili liangaliwe kwa sababu ya historia ya nchi yetu na manufaa ya vizazi vyetu.

Mhe. Spika: Ili baadae twende Amboni.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ehee. Twende Amboni. *(Kicheko)*.

Mhe. Spika, baadae tupate kwenda Amboni tukaangalie maajabu haya. Huko Mhe. Spika, kuna watalii wengi sana. Kwa hivyo, nasema tu kwamba vianzio vyote vile vinavyoendelezwa katika maeneo yetu ni kukuza utalii na kuhakikisha kwamba mapato yanayopatikana yanasaidia nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hapa kwetu kuna baadhi ya mapango mbali mbali katika maeneo yetu. Ukenda kule Bumbwini Mangapwani kuna sehemu mbali mbali zimejitokeza katika maeneo, lakini hawajapewa kipaumbele watu wale kusaidiwa na kuyahifadhi maeneo yale na kuyaweka katika mazingira mazuri, ili utalii utangazwe vizuri na wageni wanaokuja katika maeneo yale wapate kuingia katika mazingira ambayo yanafaa.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri mule mote mwenye vianzio vya watalii wanamotembelea basi mazingira yake yawekwe vizuri, ili wageni wakienda pale waweze kukaa na kuweza kuuliza maswali katika sehemu yenye kuridhisha, ili wageni waweze kuambizana na kuja kwa wingi.

Jengine Mhe. Spika, tuna bahati nzuri katika nchi yetu kule Dunga jumba la mawe. Mhe. Spika, pale pahala watalii wengi wanakwenda sasa hivi, mimi nafurahi sana, lakini hadhi hapana. Najua Mhe. Waziri suala lile litakuwa haliko upande wake, lakini kwa kuwa watalii wamo katika wizara yake basi nipake. Kwa hivyo, sio vibaya kuungana na watu wa kumbukumbu za historia ya nchi yetu ili kuhakikisha kwamba wale wageni wanaokwenda pale basi pawe na kitu cha kuvutia, japokuwa sio kikubwa. Kwa sababu mzungu hataki nyumba ya mawe wala hataki nyumba ya ghorofa. Anataka pawe na panda japo la makuti limewekwa vizuri tu, basi anaweza kukaa akauliza maswali au akanywa madafu pale na mambo mengine basi masuala yamekwisha kwa wao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba kukuza utalii kuna nyanja nyingi na kuna njia nyingi na tunataka tuongeze mapato katika sekta hii, basi ni vyema tukahakikisha kwamba maeneo yote yanayokidhi haja na yale yanayoangaliwa kwamba watafaa, basi namshauri Mhe. Waziri kama hayako katika wizara yake yeye, yako katika wizara nyengine, lakini tija inapatikana basi atilie mkazo sehemu hiyo au aongeze bidii ya mazungumzo, ili ufanisi upatikane kwenye sehemu hizo na lengo la utalii wetu ni kwamba utangazike pamoja na kwenda vizuri.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo kwa wenzetu nimeligundua kwa ajili ya kubana au kupata matumizi sahihi katika maeneo mbali mbali. Kwa mfano, hapa kwetu kuna wageni ambao huwa wanakuja kwenye fukwe zetu kama vile hutembelea Pwani Mchangani, Kiwengwa, Matemwe, Nungwi pamoja na sehemu nyengine, yaani wao huwa wanatoka mjini moja kwa moja na kwenda kule.

Kwa hivyo, wanapofika kule mtalii au watalii wale huwa wanazubaa au wanaweza kuuliza, yaani kabla ya kufika kule Pwani anaweza kukuuliza kwenda Pwani ni kiasi gani. Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri anifahami vizuri swali langu. Kwa mfano, anapouliza mtalii kule Pwani kwenda kuogelea ni kiasi gani anaambiwa huku kwenda kuogelea ni bure, yaani wanashanga au wanatushangaa sana.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo tuhakikishe kwamba mtalii kila atakachokifanya kwenye nchi yetu basi anatakiwa alipe na hilo ndilo lengo letu. Lakini napenda kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika hili likasimamiwa vizuri na kutafutiwa nafasi nzuri ya kuwekwa, yaani mtalii anayekwenda kuogelea basi angalau Kamisheni ipate kiasi fulani na wala si vibaya.

Kwa sababu mtalii anatoka kwao na fedha zake au mamilioni ya fedha anayo na kutakiwa atoe dola kumi kwa ajili ya kuogelea b
asi haoni chochote labda kama fedha ndogo sana au fedha ya kununulia peremende tu. Mhe. Spika, naomba mambo yote madogo madogo tusiyadharau.

Nikiendelea na mchango wangu kuhusiana na mswada huu nitoe mfano mwengine, sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tulipofanya ziara ya kwenda kutembelea Arusha katika masuala ya michezo na wenzetu walitupeleka kwenye mbuga za wanyama.

Kwa kweli tulishuhudia Mhe. Spika, kwamba mkakati pamoja na njia gani kuanzia kwenye mlango mkubwa wa kuingia mpaka kuingia ndani, namna unavyoshughulikiwa mtu mmoja katika masuala ya kusajiliwa kwa madhumuni

ya lile linalohitajika kupatikana basi lipatikane.

Kwa hivyo, nawapongeza sana wale.Na wala si vibaya na sisi kwenda kusoma kwa wenzetu Mhe. Spika kwa ajili ya kujifunza kila chenye manufaa kwa nchi yetu, kwa lengo la kuongeza tija katika nchi yetu pamoja na kuukuza utalii wetu kwa maslahi ya watu wetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu ni mzuri na ninaamini wenzangu wote waliomo humu sijui kwa mtazamo mwengine walionao, lakini mimi kwa kuwa napenda utalii tena najua kwamba ndio roho yetu ya mapato ya nchi yetu.

Napenda kusema mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Vile vile namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kama nilivyompa ushauri na nimempongeza sana pamoja na watendaji wake, basi tuelekeze nguvu zetu katika kupanga mipango mizuri ya uadilifu kabisa, ili pato la nchi liongezeke kupitia sekta ya utalii pamoja na kuendeleza wananchi wetu kwa faida ya kuleta mambo mengi ya kimaendeleo.

Kwa mfano, masuala ya barabara, maji, umeme, hospitali, skuli na mengineyo, yaani huduma zote tunazitegemea kutokana na fedha nyingi kwenye sekta ya utalii.

Mhe. Spika, baada ya kuunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu, basi narudia tena kusema mimi mwenyewe binafasi na kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Kwahani hasa nikizingatia wengi hivi sasa wako Kiwengwa, Nungwi, Bwejuu, Paje, Michamvi katika masuala ya kutafuta riziki, pia namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie salama hii tuliyonayo. Kwa sababu bila ya wao kwenda kuwatengenezea mazingira wanayotaka wale watalii basi watakuwa hawana faida.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika na kipindi hiki watu wetu wako kimya na wala hawana zogo, vile vile wanamuomba Mhe. Waziri waongezewe njia za kuhakikisha kwamba vipato vyao vinaongezeka wao pamoja na familia zao, ili maendeleo yakue , zaidi na kupunguza umasikini. *(Makofi)*

Baada ya hayo nakushukuru Mhe. Spika na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja na ahsante sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka katika hali ya uzima na utulivu, ili kujadili biashara ya utalii.

Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kwa ajili ya kutoa mchango wangu hasa unaohusiana na Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam.9 ya 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, hivi sasa katika masuala ya utalii ni muda mrefu na sote tunaujua utalii, yaani athari pamoja na faida zake. Hivi sasa utalii si jambo geni kwa hapa kwetu Zanzibar.

Kwanza sote tunajua kwenye ufafanuzi katika mambo ambayo ni mazuri sana kwa utalii ni usalama wa watalii na mali zao. Mhe. Spika, mpaka leo tuko kwenye hali nzuri ya suala hili, yaani watalii wanatembea na kulala salama pamoja na mali zao. Kwa kweli hili ni jambo la kushukuru sana kwa Zanzibar *(Makofi)*.

Lakini hili lingeongezeka zaidi kama tungeweka mazingira mazuri ya utalii. Ninaposema hivyo nakusudia kusema kwamba mazingira ya utalii Zanzibar bado hayajawekwa vizuri, kwa sababu uzuri wa mazingira ya mtalii ni mashirikiano baina ya mtalii na zile sehemu anazokwenda kutalii. Kwa hivyo, katika masuala haya tunatakiwa tuwe makini sana, kwa sababu kwenye maeneo ya utalii, yaani wale walioko katika maeneo yale wanaathirika sana lakini hawana mtetezi wala muombezi.

Mhe. Spika, maeneo yenye utalii maji yanatumika sana, mazingira yanaharibika, lakini yote hayo Kamisheni ya Utalii haishughulikii isipokuwa inashughulikia faida tu. Kwa hivyo, hili ni tatizo ambalo bado hatujaweka mazingira mazuri ya utalii. Kwa kweli bado fukwe zetu ni bikira na wala hazizeeki, kwa sababu za maumbile *(Kicheko/Makofi)*.

Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuona kwamba tunawasaidia vipi wale watu ambao wametoa maeneo yao kwa utalii, kwa sababu wanakula hasara sana Mhe. Spika, kama vile wanakuwa na migogoro ya maji. Kwa kuwa utalii hauzingatii kutengeneza miundombinu kwa yale maeneo ambayo watalii wanakwenda.

Kwa mfano, barabara ya Kijini kuna hoteli nzuri ya Mnemba ya Utalii tena ya asili, lakini bado mazingira yake yote yanategemea yawekwe na mwekezaji.

Vile vile kuna eneo kubwa la zaidi ya *Five Stars* liko Muyuni na wawekezaji wanasubiri Kamisheni ya Utalii itengeneze eneo, ili wawekezaji wajenge na wenyewe wa kule wapate ajira, lakini bado kimya na maeneo yamezuiwa na wala hakuna kuendeleza miundombinu. Kwa hivyo, kinachobakia pale ni

migogoro, maana yake eneo likikaa zaidi ya miaka miwili basi kila mtu anajua kisheria kwamba eneo hilo hurudi serikalini.

Kwa maana hiyo, likeshajulikana limerudi serikalini basi huwa linazaa migogoro. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, tunapokusudia kufanya biashara hii ya utalii, basi lazima tuone kwamba tunapeleka vipaumbele vya miundombinu katika maeneo ya utalii.

Mhe. Spika, suala jengine kwenye ukusara wa 36 kifungu cha 2 katika tafsiri hasa kwenye ufafanuzi wa askari wa utalii. Kwa kweli sifahamu askari wa utalii ni nani, kwa sababu haiwezekani tunao watu wa aina nyingi wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, raia wa kawaida wa kujiunga na kuwa askari.

Kwa hivyo, hawa sijui taratibu za matangazo ya tenda yanakwenda vipi kwamba wapate wenzetu wa nje ya Tanzania na Wazanzibari bado wapo na wala hawapati hii nafasi ya kuwa wao ni askari wa utalii.

Kutokana na hali hiyo, bado mazingira ya utalii hayapendezi na tunaomba yaimarishwe. Vile vile siku zote tunasema kwamba Wazanzibari wapewe kipaumbele kwa masuala ya utalii kwa sababu wao ndio wenyewe na wala hawa wasichokiweza Wazanzibari, isipokuwa wengine wavivu lakini wengine hodari *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, tuweke mikakati maalum ambayo itawasaidia Wazanzibari, kwa sababu Wazanzibari wanashida sana ya ajira, lakini ajira zipo na maeneo ya ajira yanafanywa kwao na wao hawana ajira. Kwa mfano, *Tours* wanazo kampuni za gari kubwa, lakini wale Wazanzibari wenyewe hawapati zile nafasi za kuwa wao ndio wenye kutembeza wageni, sasa sijui tatizo nini.

Vile vile kama hilo halitoshi wako Wazanzibari wenye gari zao za kawaida ambazo huwa zinachukuwa wageni kutoka eneo moja na kupeleka eneo jengine hawa hawapati nasafi ya kutoa huduma, kwa sababu hakuna msimamizi wala muangalizi katika hali hiyo ya kuona Wazanzibari na wao hasa yale maeneo wanayotoka wanapata zile ajira. Kutokana na hali hiyo, inakuwa chuki baina ya hoteli za kitalii na wao na wala si hayo tu.

Kwa upande wa huduma za maji kwa mfano kule kwetu kuna gari kama tano za maji, lakini jambo la kushangaza zitatoka gari mjini sijui za mkubwa gani na kupeleka huduma ya maji, tena maji yale yatoke kule na watu wanaohudumiwa wako kule na wao wakose nafasi.

Mhe. Spika, mambo haya yataleta nongwa baina ya Wazanzibari na wageni au wenyewe kwa wenyewe, yaani Wazanzibari.

Suala jengine katika nafasi za kutembeza watalii mimi hushangaa sana na wala sijui kama ndio utaratibu wa utalii kwamba mtembezaji wa watalii lazima kichwa chake kiwe kizito kuliko yeye mwenyewe, maana huona hapa mjini. Kwa mfano, wale wanaotembeza watalii wote hawana hali ya mazingira ya kawaida ya Mzanzibari, yaani utamuona mtu amechoka anapepesuka basi huyo ndiye mtembezaji wa watalii.

Kwa hivyo, nadhani ni vyema tuweke taratibu na tuone kwamba Mzanzibari hayuko kwenye hali ile ambaye amekamilika. Kwa maana hiyo, unapomuona Mzanzibari ambaye anatembeza wageni kichwa chake hakiwezi, basi huyo analo tatizo na halafu watu kama hawa ndio wanaosababisha matatizo kwa wageni, maana anachokieleza hakijui. Kwa mfano, anakusudia mtu anayechuma embe anaweza kusema kwamba *that man ironing mango*, kwa sababu lugha haifahamu *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, tuone kwamba tunaposhajihisha watu kama hawa basi tunawapa mafunzo ya kutosha na wala tusiwape kwa udugu tu. Kwa hivyo, ni vyema tufahamu kwamba tunapozungumza utalii basi tunazungumza hali halisi ilivyo.

Suala jengine kwenye ukusara wa 44 kifungu cha 18 hiki kinazungumzia zaidi hali ya daftari katika maeneo ya wamiliki wa hoteli. Mhe. Spika, hapa ndipo yanapopotea mapato, kwa kweli wamiliki wa mahoteli bado hawajawa wakweli hasa orodha inayooneshwa kwa maafisa inatofauti na orodha ya kulala wageni.

Kwa sababu wengine wanaweza kuwa wanalala lakini hawapewi risiti kwa wakati ule, yaani hawajisajili. Kwa kweli, msajili au mmiliki anafanya kidogo kama hana habari nao ambapo tayari ameshawaweka chumbani kama itafika mpaka asubuhi kama hajapita afisa basi haiwezi kujulikana idadi ya wageni waliolala na hali hii ni tofauti sana na kule Tanzania Bara.

Mhe. Spika, Tanzania Bara wakati tunapokwenda kwa shughuli zetu basi kitu cha mwanzo lazima mgeni aorodheshwe kwenye daftari kwa ajili ya kulipa. Kwa hivyo, ukweli unakuwepo tena kwa uaminifu wao wenyewe tofauti na kwetu mpaka usimamiwe, sijui haya anawafundisha nani. Kwa sababu hoteli zilizopo Zanzibar hasa kwenye maeneo ya vijijini huko wengi wamiliki ni wageni kwa hiyo hawajui mbinu.

Nadhani hawa *Local Managers* hawa wanaakili kuliko hawa wawekezaji wenyewe. Kwa hiyo, bado hili tuendelee kulisimamia vizuri, kwa sababu kutoa maeneo bila ya faida tunakula hasara kubwa ni sawa kuwa hatujaweka utalii na

eneo lipo tu inakuwa hakuna tofauti, basi ni vyema tukajitahidi.

Katika kusimamia suala hili tusiwaachie Kamisheni ya Utalii peke yake, nafikiri ni vizuri kuwe na kitengo ambacho kinafuatilia na tena ziwekwe adhabu ambazo zitakuwa zikionesha kwamba mmiliki atayekwenda kinyume na haya ni mkosa na adhabu yake iwe ya kileo na wala isiwe ya kizamani. Kwa sababu adhabu za kizamani zote zimeshapitwa na wakati na wala hazina muda wa kutengenezea mazingira ya kudhibiti.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kuchangia hapa ni kuandaa kwa mpango wa kazi. Kwa kweli sijui katika kazi za utalii mpango wa kazi unaandaliwa vipi, kwa sababu naijua ile moja tu ya kujiweka tayari kwenda kuutangaza utalii wa Zanzibar.

Suala hili linalalamikiwa sana kwamba viongozi wa juu wa Kamisheni ya Utalii peke yao ndio wenye fursa za kwenda na kutangaza utalii, sasa wanapofanikiwa na wasipofanikiwa ni wao tu.

Kutokana na hali hiyo, ninaomba au ninapendekeza katika hili basi wapande maafisa wa utalii kuona kwamba kila mmoja anakwenda na kuja kutueleza kipi amekiona na jinsi gani amefanikiwa.

Vile vile ipo haja ya kuongeza vipeperushi vya kukuza utalii, kwa sababu kama hakuna vipeperushi vinavyoweza kuvisifu visiwa hivi kwa uwekezaji basi bado tutakuwa na kazi kubwa katika kutanga utalii. Kwa hivyo, naomba tuongeze juhudi, ili utalii uwe unafanyakazi vizuri.

Mhe. Spika, pia tungeomba tupate tofauti baina ya miaka ya nyuma na hii tunayoendelea nayo na jinsi gani tunaendelea katika masuala ya utalii, kwa sababu kimatayarisho tumeondoka kwenye watalii wale tunaowaita vishuka na hivi sasa tunashajihisha utalii wa daraja la kwanza.

Kwa hivyo, kila mwaka tuona tunapata tathmini kwamba tunaongeza kiasi gani, maana isiwe tunaongeza au tunakaribisha watalii wengi na mapato yenyewe hayalingani na wageni ambao wapo wanaoingia.

Vile vile tuangalie zile ambazo zina watalii hasa na tuziache zile nchi ambazo zenye watembezi tu, kwa sababu wengine wanapoingia kwenye maeneo hawatumii fedha au taratibu zote za huduma wametengeneza kwao na wanapokuja hapa wanatembea tu, kwa kweli hii ni kasoro kubwa sana na wala tusiikubali. Kwa sababu sisi tumekaribisha watalii kwa ajili ya kupata faida ya kutalii Zanzibar.

Mhe. Spika, sijui kama hawa Wataliana watalii wazuri, lakini kwa upande mmoja hawa wamekuza soko sana na kukuza soko kwao kwamba hawa hawana hiyana katika kufundisha lugha yao wanapotembea. Kwa hivyo, ukitembea ukanda wa mashariki Kiwengwa pamoja na sehemu nyengine watoto wengi wanajua Kitaliana, tena wanakisema vizuri sana na sijui lugha yao haina utata, lakini bado Wataliana wana faida kubwa.

Kwa hiyo, labda atakapokuja Mhe. Waziri anieleze tukitoa Italy kuna nchi gani nyengine ambayo watalii wake wanakuja kutalii na kuacha faida hapa nchini, kwa sababu wanaotembeza watalii wengi tayari wameshakuwa matajiri.

Suala jengine nikiacha sehemu hiyo ambayo nimeichangia ni kutaka kuona kwamba hizi biashara ambazo wanazotolewa huduma watalii, imebainika kuwa kuna baadhi ya biashara hawawaachii Wazanzibari wenyewe. Kwa mfano, matunda, mboga mboga pamoja na mambo mengine, yaani hizi zinamilikiwa na makampuni makubwa na wengi katika watu ambao wanazo tenda basi mara nyingi amekosekana kama hatoki nje anatoka mjini.

Kwa hivyo, kinachofanyika ni kwamba kule vijijini wasipate nafasi ni wale managers kama anatoka mjini basi tenda hizo zitakuwa mpelekaji wake anatoka mjini, kwa hiyo kila kitu kitakuwa kinatoka mjini na wale wenyewe hawapati. Pamoja na kwamba Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto imeshajihisha sana kwamba watu wajiunge kwa lengo la kuzalisha kwa wingi, ili wafaidike.

Matokeo yake wanajiunga na kuzalisha bila ya kufaidika. Kwa mfano, kama utapita Mkwajuni basi utaona kwamba wananchi wa kule wameshajihika kwa kulima mboga mboga nyingi kama vile mchicha na kadhalika, lakini inafika kuharibika kondeni bila ya kupata *order* ya kupeleka mboga kwenye maeneo ya utalii.

Vile vile wengine wamefuga kuku wengi tena mayai yapo kwa wingi na hata Mfurumatonga yapo, lakini *order* ya kupata kupeleka kwenye mahoteli imekuwa ndogo mno. Kwa hivyo, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto vizuri sana, kwa kweli ile dhana hasa ya kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo bado haijafika pahala pa kuwakwamua kibiashara.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache maana nilikuwa sijajiandaa vizuri tokea asubuhi tuko na kamati ukumbi wa juu. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Matemwe kwenye mapendekezo niliyoyataja wameyasikia wenyewe na wamefurahi.

Kwa maana hiyo, mimi pamoja na wananchi wangu tunaunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu *(Makofi)*.

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii Zanzibar Nam.9 ya 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, Katibu Mkuu wake, Wanasheria wake pamoja na watendaji wake wote kwa jumla kwa kuona mswada huu, ili utambulikane kwa mujibu wa sheria na watu wafahamu ni hasa dhana ya utalii.

Mhe. Spika, katika jimbo langu kuna eneo kubwa sana la utalii, ambalo kwa mujibu wa sheria hii itaweza kutusaidia sana. Kwa sababu kuna wananchi ambao hawafahamu nini maana ya utalii wa uwekezaji, isipokuwa wao wameona tu kwamba Serikali basi wameleta kwa mujibu wa kuona serikali itakuwa inapata mapato tu na wao hawanufaiki na kitu chochote.

Lakini hizi ni dhana ambazo wanazo wale wananchi wasiokuwa na taaluma na hali hii ni kweli. Mhe. Spika, hivi karibuni nilipata ugeni wa Mhe. Waziri Kiongozi na tulikuwa naye kwenye Hoteli moja ya *Go Inn* ambayo zamani ilikuwa ni *Sea Club*. Kwa kweli Mhe. Waziri Kiongozi alishangaa sana kutokana na ule utaratibu wa mahoteli wa kuwasaidia jamii.

Mhe. Spika, kilichomshangaza Mhe. Waziri Kiongozi baada ya wahusika kuwauliza maswali na kujibu maswali yale na kuona kwamba kwa kweli yule ambaye yupo karibu na utalii wenyewe amegundua kumbe hakunufaika, walionufaika ni wale walionje tena kwa asilimia kubwa kabisa.

Kwa mfano, Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Mhe. Ame Mati Wadi alitoa mifano hiyo, yaani kuna mambo ambayo wananchi wale wa vijijini wao uwezo wa kupata manufaa ya ule utalii ulioopo kwenye maeneo yao.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna vitu ambavyo wao wanaweza kuvimiliki, lakini utaona nafasi zile hawapewi wao na kupewa watu wa nje kabisa. Kwa hivyo, hili ni moja miongoni mwa kasoro na kuona kuwa utalii una manufaa gani kwa wananchi?

Vile vile kuna hizi kazi ambazo hazihitaji taaluma kubwa isipokuwa ni vifaa au nyenzo za kufanyia kazi. Kwa mfano, kama hizi gari za taka badala

mwanakijiji yeye sehemu ile aweze kupewa na kufanya shughuli ile, basi anatokea mtu mwenye fedha zake kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi na wala sisemi kama kuna mkubwa nadhani hawezi kuingia kwenye gari la kuzolea taka.

Kwa hivyo, analeta gari kwa ajili ya kupata manufaa yake na wale wananchi wanaendelea kulala hoi pale, yaani wanasinzia. Sasa hali hiyo kwa kweli wananchi wetu wanashindwa kuifahamu hii mantiki ya kusema utalii unafaida gani kwao wao.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba alifanyakazi kubwa sana Mhe. Waziri Kiongozi baada ya kugundua kasoro zile, basi alitutaka baadhi ya viongozi wa Kamisheni ya Utalii, Mkuu wa Mkoa pamoja na mimi Mwakilishi wao kwa ajili ya kukaa pamoja na kujadili hali ile kwa lengo la kunusuru hatari ile iliopo pale.

Kwa sababu hata ile kazi na mfano ukatolewa aliulizwa yule mhusika na kuambiwa wewe familia yako ndugu wa baba na mama mmoja na ndugu wa shangazi na mjomba yupi utakayempa kazi, basi alisema huyu ndugu yangu wa baba na mama mmoja.

Lakini kwa maana hiyo ni kwamba yule mtu wa karibu anakosa kazi wa pale kijijini, ambaye yeye wakati linapotokea janga lolote basi anao uwezo wa kwenda kusaidia na yule ndiye anayekosa kazi, matokeo yake anakuja kutoka mjini au kutoka sehemu nyengine kama vile Kenya na kupewa nafasi ile.

Kwa kweli suala hili linaudhi sana pamoja na kuwavunja imani wananchi wetu, lakini kwa bahati nzuri *alhamdulillah* unapotoa taaluma nzuri na watu wakafahamu, basi suala hili linaweza kurudisha imani kwa wale wananchi wetu.

Mhe. Spika, hivi sasa tayari gari la taka wananchi wameshaanza kupata manufaa madogo madogo na wamerejeshwa na wanaendelea kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo, ile imani inarudi baada ya kufahamu kwamba hivi sasa utalii utatusaidia katika kuondoa umasikini na kutupeleka kwenye utajiri.

Nikiendelea na mchango kwenye kifungu kinachosema askari wa utalii. Mhe. Spika, ninavyofahamu ni kwamba afisa mhusika, lakini kwa dhana nyengine au wenzetu katika nchi nyengine wanakuwa na sare maalum, yaani utamjua kama huyu ni askari huyu kwa sare aliyovaa ni wa sehemu fulani. Lakini tukisema askari wa kawaida kama ni *Officer* tu, basi tutakuwa hatujamfahamu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, anisaidie maarifa hayo, kweli hawa ndugu zetu wanatusaidia kwa ajili ya kuweka

usalama wa utalii na mpaka hivi sasa *alhamdulillah*. Kwa sababu wanapotoka huko kwenye maeneo yao na kuja Zanzibar hatujawahi kusikia na masuala madogo madogo yamo, lakini hasa kwa asilimia kubwa hayajatokezea yale matukio yaliomakubwa sana kama nchi za wenzetu.

Mhe. Spika, labda niseme hapa kidogo kuwa ulinzi huu au askari wa aina hiyo tuweze kuelimishwa vizuri na kuoneshwa zile sare zenyewe zinazohusika, hasa ikiwa kama kitengo hiki kinataka kuanzishwa au kipo, basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, azidi kukitanua vizuri na tuwaone hawa maaskari ambao ni walala hoi ndugu zetu hapa kwa ajili ya kuweza kutusaidia.

Mhe. Spika, napenda kumuomba Mhe. Waziri awape taaluma nzuri, kwa sababu ni kweli kuna watalii wengine wanapenda watu wa aina ile. wenye rasta, walevi, wavutaji wa bangi, wavaaji wa herine, lakini pamoja na hayo tuangalie na sisi *culture* yetu ilivyo hapa.

Kwa hivyo, na hilo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa makusudi ili hawa waweze kuwasaidia pamoja na kufanyabiashara nzuri kwa lengo la kuitangaza Zanzibar kutokana na zile tabia zetu tulizokuwa nazo. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri awaite hawa na kuwaelimisha ili waweze kupata taaluma nzuri, waweze kuielezea Zanzibar halisi ilivyo na wao wapate ajira kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, kule katika ukanda wetu wa pwani Kiwengwa kuna hawa watu wanaoitwa mapapasi. Kwa kweli hawa ndugu zetu wamefika pahali sasa hivi wanakera sana watalii. Lakini kuna watalii wengine ni wakaidi kusema kweli, ukaidi wao haridhiki kama hakumpata fulani, sijui wenzetu wana siri gani. Kuna watu kama kule ukanda wa Kiwengwa wamefuata sheria, wana kijiji wamejikusanya vizuri kabisa kwa mujibu wa taratibu zao na wanazo sare zao unajua kama hawa ni watu wa usalama na wamefuata sheria na wako tayari kuonana na wazungu na kuweza kuwafahamisha zile sehemu zinazotakiwa za kiutalii. Lakini utakuta kuna watu wengine wanakwenda kuwakera wakati anajua muda fulani amelala yeye ndio anakwenda kumkera.

Mhe. Spika, vile vile huyu mtalii anakwenda kumtafuta mtu huyo huyo anakiuka ile sheria iliyowekwa katika kijiji. Mhe. Spika, watu kama hawa tungeomba watafutiwe taaluma na waelimishwe vizuri, pia wafahamishwe hawa waliokubalika kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar wawe na usalama wa aina gani. Mhe. Spika, tukifanya hivyo basi nafikiri tutakuwa katika ile dhana ya utalii itakuwa katika sehemu nzuri sana.

Mhe. Spika, sasa hivi huko kuna kero kubwa sana kwani nimeshakwenda mimi mwenyewe na nimeshuhudia vizuri, tumeshazungumza na wale askari na

wenye mahoteli tumejaribu kuzungumza nao, lakini hilo suala bado mpaka sasa hivi halijawezwa kuondoshwa kwa asilimia kubwa sana. Kwa hivyo, ningeomba wale wanaohusika tuko tayari kutoa msaada kwa nguvu zetu zote ili tufike pahali lile kero la wale wazungu liondoke na wakae katika sehemu ambayo inastahiki na wao wajiskie kama wanafanya mambo yao kwa raha kabisa.

Mhe. Spika, hili ni suala ambalo la biashara ya utalii. Unajua watu wengi sana suala hili linakuwa gumu kwetu kulifahamu, lakini kama nilivyosema watu wengine hawajui kama utalii uko wa aina gani. Utalii ni kuondoka sehemu moja na kwenda sehemu nyengine hiyo ni moja katika utalii. Hilo nalo pia inawajibika sisi tulifahamu nini maana ya utalii, ili tujue dhana ya utalii.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kuchangia katika mswada huu ni kuhusu suala la leseni. Mheshimiwa Kamisheni na wao wanatoa leseni, Halmashauri nao wanatoa leseni, lakini hili suala la utalii lina upana mkubwa katika biashara hizi. Kwa kweli mimi ningeomba Mhe. Waziri awasaidie sana hawa watu wa Halmashauri kwa sababu na wao wanatusaidia sana katika maeneo yetu. Sasa kila siku zikienda kila mtu akiwa anaanza kuchukua sheria kwa lile lake alililoliona basi utakuta pahali hiyo Halmashauri haitoweza kufanya kazi ya aina yoyote na hatoweza kutusaidia katika maeneo yetu. Mhe. Spika, Halmshauri kila wakifanya kazi nzuri basi na wao wanaweza kusaidia kutoa mchango mkubwa katika serikali yetu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nichangie kidogo tu mimi sina tatizo na mswada huu nimeukubali mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa hayo machache nasema ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuhusiana na mswada huu wa kurekebisha sheria ya utalii.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima tukaweza kuweko mbele ya Baraza lako tukufu kuzungumza yale ambayo Mwenyezi Mungu mwenyewe ametujaalia tuyazungumze.

Pili kwa kuwa nilikuwa nimo ndani ya Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya kujadili mswada huu nina vipengele vichache ambavyo ningependa nivitolee maoni yangu ndani ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kwa kuanzia mimi natizama madhumuni ya mswada huu. Kwa sababu Kamisheni yenyewe ipo ambayo inaitwa idara na sasa inataka kufanywa vyenginevyo, basi madhumuni makubwa yaliyotajwa ni kuongeza ufanisi na kujenga mazingira mazuri ya kukuza biashara ya utalii. Kwa kutizama mantiki

kauli hii ni lazima Mhe. Spika jambo hili lihusishe shughuli zote za utaratibu wa uendeshaji wa nchi, kwa sababu watalii ni watu ambao tunawategemea kuleta tija huwa wanatoka katika mataifa mbali mbali.

Kwa kuwa wanatoka katika mataifa mbali mbali na tamaduni zao, uendeshaji wao wa mambo unatofautiana. Watalii ambao tunawategemea waingie ni watu wenye fedha zao ambazo kwa kiwango fulani wameweza kuweka na wanataka kuja kutimia kwa kujiridhisha nafsi zao. Ikiwa sisi tunataka waingie watalii haiwezekani kuwaita watalii wa kuunda vyombo vya kubadilisha majina kila siku, lakini tuwaite watalii kwa mazingira yaliyo mazuri na ya kiusalama katika nchi yetu. Bila ya kutengeneza mazingira ambayo sio ya kiusalama, biashara hii itakuwa ni ngumu na sisi.

Mhe. Spika, mjumbe mmoja hapa alitangulia kusema kwamba Kenya ilipoingia katika mtafaruki baada ya uchaguzi mkuu idadi ya watalii ilipungua kwa kasi kubwa na ilibidi watumie mamilioni ya shilingi zao za Kenya kwa kuirudisha hali ile pamoja na marekebisho ya ndani ya nchi kufanyika ya kurudisha imani ya wale watalii. Ni bahati mbaya sana Mhe. Waziri anauleta mswada huu wakati nchi yetu inaingia katika utata mkubwa wa kukosa utulivu katika nchi. Mimi ni mtetezi mkubwa wa shughuli za maendeleo, Waheshimiwa Mawaziri watatu tunaofanya kazi nao katika wizara hizi wananielewa.

Vile vile sipendi kuuficha ukweli ikiwa kuna haja ya kuusema, kwa sababu kuna msemo mmoja wa wataalamu wanasema “Haifai kuweka kitu kinachotakiwa kusemwa wakati wa ikitokea haja”. Wako viongozi ndani ya redio zetu na televisheni zetu waliotangaza kuwa wanakuja Pemba kupambana na ugaidi, wanastaajabu nini Balozi wa Marekani na wenzake kusema kwamba tunawatahadharisha Zanzibar kwamba hakwendeki.

Mhe. Spika, siku ya tarehe 17-8-2009 nikiwa mimi ni shahidi wa macho si wa kuelezwa, kuna vijana waliohudhuria kwa usalama bila ya bakora hata ile ya Kipemba, walikwenda katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya kwa madhumuni ya kupatiwa vitambulisho, waliambiwa basi nendeni haya tutayatengeneza. Kwa hivyo, viongozi pamoja na Wakuu wa Polisi walikuwa wanayatengeneza yale mambo ghafla zikateremka *defender* mbili na gari moja kubwa la jeshi likaanza kuzunguka mji mzima wa Chake-Chake.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atajua kwamba karibu na Benki ya Watu wa Zanzibar Chake-Chake kuna hoteli nyingi zimefunguliwa ziko eneo lile, hoteli zote hizo zina wageni wa rika mbali mbali na wa maeneo mbali mbali wanayaona mambo haya, jeshi lile linazunguka na hawakuweza kubaki katika gari zao wakashuka kuwatimua watu na hali ya kuwa wageni wapo wanayaona. Mimi ndio nasema kwamba tusikatae maneno yanayosemwa na baadhi ya vyombo

vya habari wakati mambo haya sisi tunayashuhudia. Tukisema watalii sasa hivi hawaji na hali ya kuwa mazingira haya tumeyatengeneza sisi wenyewe, kwa hivyo tusijialumu tuangalie wapi tulipokosea. Ikiwa tunaona hatukukosea basi tuendelee hivi hivi, lakini mtalii ni mtu ambaye anaona yanayotekezea wala hategemei kuambiwa.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kujenga mazingira ya biashara ya utalii ni kuweka miundombinu bila ya kubagua maeneo. Watalii wengi wanaokuja huwa tunawaona sisi wale wanaokuja na kuijua hii nchi au kusikia mbali ya hao wanaokuja kwa shughuli nyengine. Ikiwa wanazo *map* zetu tokea huko wanakotoka wao wanaijua Zanzibar ilivyokuwa inatangaza biashara ya utalii lazima huwa wameshatengeneza miundombinu yao. Anakuja anataka kwenda pahali gari iliyotegemewa kumpeleka hawezi kumpeleka, watalii wanaotumia Hoteli ya Fundo Lagon kule Wambaa mpaka leo wanatumia boti hakuna anayetumia gari, huu ni mwaka wa kumi tokea kufunguliwa ile hoteli. Mhe. Spika, utasemaje wewe unatanua biashara ya utalii wakati miundombinu hupeleki au unapeleka kwa njia unayoitaka mwenyewe.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ni mazingira mazuri ya kutengeneza hii Kamisheni ya Utalii ni kuwa na chombo ambacho kitakuwa na wataalamu wa kutosha. Nchi yetu imegawika katika visiwa viwili, sisi haya hatukuyataka kama vile mtu anavyokuwa hachagui pa kuzaliwa, wala hachagui pahali pa kufa. Wewe hata ukasema kwamba mimi nataka nife hapa petu, unaweza ukapata safari na ukaitengeneza mwenyewe vizuri sana na malipo ukalipwa lakini ukifika tu kule ziraili anakusubiri huko huko. Je, ulichagua kwa kwendea kufa kule.

Kwa hivyo hakuna ambaye alichagua mimi nizaliwe hapa, sasa kwa mtindo huo tunaoendelea nao sisi hatuwezi kupata maendeleo kwa sababu wako watu ambao wana uwezo mzuri tena ndani ya wizara hii. Lakini kwa sababu wamezaliwa pahala fulani basi yeye hapewi nafasi ile kwa sababu anatiliwa wasi wasi kwamba huyu ni mtu wa fulani, huyu ni mtu wa aina hii. Pengine hata jambo hilo siku moja tu katoa rai yake ikaonekana rai hii haiwezi kuwa ni yake lazima itakuwa inatoka pahali fulani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuunda hii Kamisheni kwa kuanzia na Mkurugenzi Mkuu basi wizara iweze kuamua kwamba kipaji cha mtu, uwezo wake na utandaji wake ndio kiwe kigezo cha kuchukua. Sio kazaliwa wapi, ana chama gani la kapitia *GSO* basi tuendelee lakini tusione kama tunarekebisha vitu kwa kubadilisha majina halafu tukaona vitafanya kazi kwa kumtizama alipozaliwa au kwa kumtizama anapoelekea. Wewe mtizame uaminifu wake huyu kama ni CUF umempa milioni kumi amezifuja basi ashitakiwe, lakini akiwa ni CCM asije akalindwa nae. Akiwa ni CUF umempa milioni kumi kazitunza basi na

wewe mtunze na umzawadie. Lakini tukianza kuchukua mwenendo huo basi hatufiki pahala.

Mhe. Spika, jambo hili linasikitisha sana na hivyo ndivyo tunavyokwenda sisi tunapata maelezo mbali mbali kutoka kwa watu tofauti kwamba kitengo hiki hakiendi kwa sababu hii na hii, na ukitizama mambo hayo yamo. Ikiwa Mhe. Waziri au mtu mwengine anataka mimi nimpe ushahidi kama tuko peke yetu basi nitampa. Kwa kweli tukiwa kama hivi hatwendi mbele kabisa.

Mhe. Spika, humu limetajwa neno Mzanzibari, mimi nafurahi sana kwa mujibu wa maelezo yalivyoandikwa, hivyo ndivyo itakavyotumika neno Mzanzibari. Lakini huyu Mzanzibari anatakiwa awe na kielelezo, kielelezo cha sasa ni kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi lakini kama mtu hakupewa je? Kwa hivyo, imefika wakati lazima tujitizame kweli huu mwendo tunaokwenda ndio halisi unaotakiwa, ndivyo hasa tunavyotaka twende. Sisi wengine kwa mfano mimi binafsi napenda sana kusikiliza habari za televisheni tofauti kabisa, lakini ukitizama TVZ basi utaifunga hapo hapo kutokana na hayo mambo yanayotajwa.

Kwa hivyo, na sisi tunataka kusikia katika nchi yetu habari ambazo zina ukweli ndani yake na zilizofanyiwa uchambuzi. Kwa nini televisheni zote za wenzetu zina habari zilizofanyiwa uchambuzi na zinakwenda vizuri. Mimi sidhani kwamba nikisikiliza televisheni ya Marekani hatopenyeza propaganda yake ya Marekani lazima ataipenyeza propaganda yake na akipenyeza basi wewe utaijua. Leo mimi nazungumza hapa mambo yote haya basi hutolisikia hata moja kuzungumzwa katika televisheni, lakini ikiwa Sheha mmoja siku moja kasema jambo basi litatoka kuliko mimi niliyechaguliwa na watu 10,000. Kwa hivyo, kuna uwiano gani hapo, mwakilishi niliyechaguliwa na watu 10,000 nazungumza kwa muda wa mwezi nzima hapatoki jambo, Sheha ambaye Mkuu wa Mkoa siku moja tu amemtaja jina kwamba wewe utakuwa Sheha basi mambo yake yote yamo ndani ya televisheni.

Mhe. Spika, sasa kwenye biashara ya utalii kunatakiwa kuwe na ukweli ndani yake ili yale maneno ambayo watu ambao wanashiriki katika biashara ile na wale wageni wanapokuja waone kwamba mtiririko ndio ule ule. Kwa sababu watalii moja katika jambo ambalo mimi nalifuatilia katika biashara ya utalii kila ukitoa tangazo ya biashara ya utalii wanatolewa wale watu wenyewe. Kuna kipindi katika televisheni moja kinaitwa *travel* hata Zanzibar kimeshawahi kuoneshwa siku moja. Ile *travel* wanaonesha kwamba ili upate nafasi ya kwenda kule huwa wanachukua ile jamii namna inavyoishi, wakija hapa huwa wanatia watu vurugu tu.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu utata wa leseni limeshazungumzwa hapa kwa kirefu hivyo bado tunawaomba wizara hii iweze kukaa kitako na vyombo vyengine vya leseni waweze kukubaliana kimsingi kwani karibu tunaingia mwaka mpya. Kwa hivyo, kabla hatujaingia mwaka mpya iwe hii Kamisheni imeshakaa kitako au ikiwa ni wizara na vyombo vyengine vya leseni wakubaliane bila ya hivyo kwani fedha ikishakulipwa serikali sio rahisi yule mtu kwenda kudai. Kwa hivyo, kabla ya vile vyombo vyengine havijatoa nafasi ya kulipa mara mbili au tatu iweze kutizamwa.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka kulizungumzia hapa ni kwamba katika Bodi ya Wakurugenzi kumetajwa daktari, inawezekana asiwe daktari peke yake lakini kuna watu muhimu sana wanaoitwa watu wa afya ya jamii. Mhe. Spika, wataalamu hawa ni muhimu sana kuweza kuingia katika vyombo kama hivyo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ili nchi yetu iweze kukwamuka katika mkwamo huu kwa sababu kuiendeleza biashara hii ya utalii kinachotakiwa hasa ni kuzidisha pato la taifa. Kwa sababu ikiwa ni kuwakaribisha tu wageni halafu wakenda zao sidhani kama ndio madhumuni wenyewe. Pamoja na kwamba tunajenga mazingira mazuri lakini lengo ni kuzidisha pato la nchi. Katika kuzidisha pato la nchi hoteli zinazojengwa hazitoi nafasi kwa wananchi kutimia au kupeleka fursa zao.

Kwa hivyo, serikali inapaswa ifanye mambo matatu. Kwanza iwe karibu na kila mwananchi wake bila ya kubagua, ukimbagua mwananchi unajenga mazingira ya kwamba yule mwananchi hawezi wewe akakusaidia katika jambo lako na serikali inahitaji wananchi wake waisaidie ile serikali katika mambo yao.

Jambo la pili ni kujenga mazingira ya ukweli kile tunachokisema kiwe ni kweli kwa sababu hata hizi picha zinazopelekwa huko nje, mwisho tutasema tutazipeleka sizo kwa hivyo watalii watakapokuja hapa watakuwa wanaona mambo ni tofauti na vile tulivyoambiwa. Ikiwa hapa hapana utulivu basi mseme kweli kweli kwamba sasa na sisi tunakubali kwamba hapana utulivu isiwe *statement* inatoka kwamba hapana utulivu nyinyi mkasema njooni, wakija wakaona hapana kwa hivyo hata mkatoa kauli gani watakuwa hawaamini tena.

Jambo la tatu *transition* ya nchi kutoka kila miaka mitano ni yenye kutatanisha. Sasa tukubali jambo moja hawa watalii hawatembelei nchi ya chama kimoja wala nchi ya vyama vingi, wala nchi yenye ufalme, wao huchagua mazingira mazuri wakenda. Ikiwa vyama vingi havitufai sisi tunawapenda sana watalii waje ili tupate mapato yao, ikiwa vyama vingi havitufai basi bora turudie chama kimoja ili watalii wetu wetu waje, na ikiwa chama kimoja pia hakitufai

kwa sababu ya makundi turudie kwenye ufalme. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Utalii ya Zanzibar 2009 na mambo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, kwa kweli mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa kama nilivyotarajia, lakini hata hivyo, nitajitahidi kadiri inavyowezekana niweze kuchangia yale ambayo nahisi kwa mawazo yangu yanahitaji kuchangiwa.

Nianze na madhumuni ya mswada huu kama yalivyoelezwa katika ukurasa wa 48 kwamba,

> "Mswada huu wa Sheria unalenga kuweka mfumo bora wa kisheria ili kujenga mazingira mazuri ya kukuza biashara ya Utalii, ambapo sekta ya umma na binafsi zitahamasishwa kuendesha shughuli zinazojali mazingira, shughuli za kitalii katika baharini na katika anga ndani ya Zanzibar".

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu nadhani yako wazi, kama ilivyoelezwa hapa ni kuweka mfumo bora wa kisheria ili kujenga mazingira mazuri ya kukuza biashara ya utalii. Kwa mujibu nilivyofahamu mimi katika kipengele hiki ni kwamba, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji inakusudia kuweka mfumo bora wa kisheria, ambao ndani yake utajenga mazingira mazuri ya kukuza utalii.

Mhe. Spika, bila ya sheria lazima tukubali kwamba hakutakuwa na mfumo bora au mazingira mazuri ya jambo lolote, lakini pale ambapo tutakuwa tumeanzia na sheria naamini kabisa kwamba mazingira mazuri ambayo tumeyakusudia basi yatakuwepo. Kwa sababu mazingira mazuri yanajengwa na misingi ya kisheria ni lazima kwanza tutengeneze sheria na baadae ndipo mazingira mazuri ambayo tunayatarajia yatajitokeza.

Inawezekana kwamba madhumuni ya mswada huu pengine wenzangu wamefahamu kama walivyofahamu, lakini nilivyofahamu mimi ni kwamba lazima kuwepo na sheria kwanza na ndipo mazingira mazuri yaweze kuwepo. Kwa maana hiyo basi, mswada huu unakusudia kuweka sheria ambayo itakuwa ndio muongozo katika kujenga mazingira mazuri haya ya kuendesha au kukuza biashara ya utalii ambayo inawezekana kwa upande mmoja sekta binafsi au ya umma itakuwa ndio ambayo inaongoza.

Nataka nikiri kwamba mswada huu umekuja kwa wakati mwafaka, wakati ambapo nchi yetu inakusudia kuendeleza sekta ya utalii na kama inavyoeleweka kwamba sekta ya utalii ni moja ya nguzo muhimu ya uchumi

wa taifa letu. Pia tutakapokuwa tumeweka mazingira mazuri ya kisheria maana yake ni kwamba tunaweka wazi wajibu wa kila mtu. Lakini wajibu wa kila taasisi na wajibu wa kila mfanyabiashara ambaye anaingiza katika biashara hii.

Mhe. Spika, leo mchana nilibahatika kwenda Fumba, lakini nilipofika njiani nikawa najiuliza maswali mengi tu na moja ikawa ni ile barabara ambayo sasa hivi inajengwa kuelekea Fumba ambayo hivi karibuni itamalizika. Kwa kweli nilipofika Fumba nilijaribu kudadisi wenyeji wa Fumba jinsi ya mazingira ya Fumba na uwezekano wa kupata kiwanja katika maeneo yale. Lakini kila ambaye nimemdadisi aliniambia katika mazingira ya sasa hivi si rahisi kuweza kupata kiwanja katika eneo la ufukwe. Nikawa najiuliza kwa nini? Lakini mwenyewe nikawa nimejipatia jibu ni kwamba moja ya sababu ambayo imepelekea kwa nini viwanja sasa hivi maeneo ya Fumba imekuwa ni shida, ni ile barabara ambayo hivi sasa inakaribia kumalizika.

Mhe. Spika, hapa nakusudia kusema kwamba, serikali inajitahidi kadiri inavyowezekana kuweka mazingira mazuri ambayo yatawezesha sekta hii ya utalii kuweza kwenda vizuri. Wakati nilipofika kule pia niliiona njia moja ambayo imeteremka pwani nikauliza huku kuna nini? Nikaambiwa huko kuna hoteli. Hapa nilichojifunza ni kwamba mazingira ya utalii yanategemea sana kuwepo kwa miundo mbinu ikiwemo barabara. Katika visiwa vyetu hivi sasa kwa kweli tunajivunia kwa kiasi kikubwa sana. Maendeleo makubwa ambayo yamefikiwa ya barabara ambazo hasa katika maeneo ya utalii kwa kweli ni moja ya mambo muhimu sana ambayo nchi yetu tujivunie kwamba imefanikiwa.

Mhe. Spika, nakusudia kusema kwamba mazingira ya utalii yanategemea miundombinu na moja ni hii barabara ambapo kwa kiasi kikubwa nchi yetu imefanikiwa. Pamoja na kwamba bado yapo maeneo ambayo hadi hivi sasa inawezekana bado hayajakuwa na miundo mbinu hiyo mizuri ya barabara, lakini mwelekeo, nguvu na jitihada ya serikali ni kuona kwamba maeneo yote yanapata miundombinu hiyo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilijifunza katika mswada huu ni sehemu ya pili ya kazi za kamisheni. Moja ya kazi ambayo kamisheni itapangiwa ni kuhusu kuziendeleza na kuziratibu sekta za binafsi na za umma zinahusisha biashara ya utalii. Mhe. Spika, huwezi kuendeleza, kuratibu au kuweka utaratibu mzuri bila ya kuwa na sheria ambayo imetengenezwa vizuri.

Napenda niwashukuru watu wa Wizara ya Utalii wakiongozwa na Mhe. Waziri kwa kuona umuhimu wa kuwa na mswada huu ambao kwa kweli utakuwa ndio muongozo katika kuratibu na kuendeleza sekta hii ya utalii. Kama nilivyosema mwanzo sheria ndio muongozo na sheria ndio itakayoweza kutufanikisha kutoa

muongozo wa kuratibu au kuendeleza.

Jambo jengine ambalo ni muhimu sana kulizingatia katika sheria ni jinsi gani sekta hii itaweza kuchangia ama kufanikisha au kuharibu mazingira. Sasa hivi ulimwengu umekuwa unalia na mazingira. Hapa nimejifunza tu kwamba, sababu kubwa ni kutokuwepo na sheria ambazo zinaongoza mazingira na sheria ambazo ziko makini katika kuongoza mazingira.

Mhe. Spika, sisi kama visiwa ni lazima tuwe na sheria ambayo itakuwa ni muhimili wa kuongoza katika kudhibiti mazingira. Nawashukuru kwamba katika mswada huu wamegusia kabisa kipengele cha mazingira ambayo ni muhimu kwa taifa letu.

Sisi tunaishi katika mazingira ya visiwa. kwa hivyo, kama hatutakuwa makini katika kudhibiti mazingira yetu basi visiwa hivi vitakuwa hatarini kuweza ama kutoweka ama kuwa hatarini katika kupata majanga mbali mbali. Tunajifunza na nchi mbali mbali za Asia hivi sasa zinavyoathirika na mazingira au uharibifu wa mazingira. Mara nyingi nchi hizo zimekuwa zikikumbwa na vimbunga ama mafuriko au majanga mengine ya maradhi. Kwa kweli hapa nimpongeze Mhe. Waziri wa Biashara kwa kuja na sheria hii ambayo pia imezingatia mazingira kama ni jambo muhimu katika dunia ya leo.

Mhe. Spika, tunapozungumzia mazingira hatuzungumzii misitu peke yake bali tunazungumzia mambo mbali mbali ambayo yataathiri mazingira yakiwemo na mambo ambayo yatatokana na matumizi ya hiyo hoteli. Hivi sasa dunia kama nilivyosema kwamba imekuwa ikikutana na kuzingatia kwa kiasi gani mazingira yanaweza yakatunzwa. Mazingira yanaweza kuharibika hata maji yale ambayo yanatumiwa katika mahoteli haya. Maji haya kama hayatatunzwa vizuri au kudhibitiwa yanaweza yakapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira katika visiwa vyetu hivi. Lakini pia mabaki mbali mbali ambayo yanatumika katika mahoteli, kama hatutakuwa na sheria nzuri za kuweza kudhibiti basi bila shaka tutakuwa wenye kuathirika kwa kiasi kikubwa sana.

Utalii una mambo mengi na moja ni hili la mazingira. Hapa nimegusia sana mazingira kwa sababu naliona ni jambo muhimu sana katika visiwa vyetu hivi. Kukua kwa utalii ni lazima tukubali kwamba kutatuathiri kwa namna moja au nyengine kama hatutakuwa na muongozo na utaratibu au mfumo bora wa kisheria. Lazima tukiri kwamba tangu utalii uingia katika visiwa vyetu hivi kumekuwa na athari kubwa sana ya kupotea kwa misitu, kuharibika fukwe zetu na athari kubwa sana za utamaduni wetu.

Mhe. Spika, napenda nimalizie kwa hiki kipengele cha mazingira ni kwamba, sheria hii itatoa muongozo wa kudhibiti mambo yote ambayo yataathiri au

yatatuathiri kwa namna moja au nyengine katika uharibifu wa mazingira. Kwa sababu tayari kamisheni itakuwa na kazi na jukumu la kuweza kudhibiti uharibifu wa mazingira naamini kabisa sheria hii itaweza kutusaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kudhibiti suala zima la mazingira ambayo yanatokana na athari za utalii.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni muhimu na ambalo limeelezwa katika kipengele cha pili kwamba, katika kazi za kamisheni moja wapo ni kuelimisha umma juu ya umuhimu wa utalii kwa Zanzibar na jukumu lake katika maendeleo ya utalii. Lazima tukubali kwamba tunahitaji kuwaelimisha wananchi umuhimu wa utalii na athari zake katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, sheria hii kama ilivyoelezwa kwamba Kamisheni ya Utalii itakuwa na jukumu hili. Bila shaka kwamba itaandaa mipango mizuri ya kuwaelimisha wananchi kuona kwa kiasi gani waweze kusaidia Sekta hii ya Utalii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu.

Tunapozungumzia utalii inawezekana ni moja ya uwekezaji ambao umetoka moja kwa moja kutoka nje ya nchi ama inawezekana ni wawekezaji ambao wa ndani waliowekeza katika visiwa vyetu kwa lengo la kukuza uchumi wetu. Utalii ama utasaidia katika kukuza ajira, lakini vile vile utasaidia katika kukuza taaluma ya watu wetu. Watu wetu wakielewa umuhimu wa utalii bila shaka ndipo mafanikio yatakapojitokeza, lakini kama hawataelewa umuhimu wa utalii naamini kwamba mafanikio nayo hayataweza kufanikiwa. Kwa maana hii nakusudia kusema kwamba, Kamisheni ya Utalii ina jukumu kubwa sana ama kufanikisha Sekta hii ya Utalii ama kurudisha nyuma itategemea kwa kiasi gani wataweza kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, ajira katika Sekta ya Utalii sasa hivi imechukua sehemu kubwa ya ajira katika visiwa hivi vya Zanzibar. Bila ya utaratibu mzuri wa ajira naamini kabisa watu wetu hawataweza kunufaika, lakini kwa sababu sheria hii tayari itakuwa inatoa miongozi kwa wawekezaji jinsi gani waweze kutekeleza suala zima la ajira basi naamini kabisa baada ya kuelimishwa wananchi wetu basi wananchi hao wataweza kufaidia na Sekta hii ya Utalii.

Jengine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu suala zima la majukumu ya wawekezaji. Majukumu ya wawekezaji katika uwekezaji wao, lakini pia katika majukumu ya kijamii. Kama walivyotangulia kusema wenzangu ni kwamba, uwekezaji ni moja ya chachu ya kuweza kusaidia jamii yetu pale ambapo wawekezaji wapo.

Tumejifunza mengi wakati watalii wapo hapa nchini, wameweza kusaidia katika nyanja mbali mbali. Lakini ni wajibu wa kamisheni kuwaelimisha pia

hawa wawekezaji, kwamba wana wajibu wa kuona kuwa majukumu haya ya kijamii na wao wanahusika katika kuweza kusaidia majukumu hayo. Hapa nadhani ni lazima tuchukue jitihada ya kuweza kuwafahamisha vizuri wawekezaji kuona kwamba wana jukumu gani katika jamii ambayo imewazunguka, mbali ya kwamba wao wanaweza kutengeneza pesa, vile vile wana jukumu la kuhakikisha kwamba jamii iliyowazunguka inawategemea na ndio ambayo itaweza kufanikisha sekta hiyo. Kuwa mbali na jamii ni dhahiri kwamba mafanikio ya utalii nayo pia hayatafanikiwa. Lakini wakiwa karibu, wakitekeleza majukumu yao basi bila shaka sekta hii ya utalii itaweza kufanikiwa na kuweza kusaidia mchango wa pato la taifa letu.

Mhe. Spika, kuna uzoefu wa wawekezaji hasa katika sekta hii ya utalii. Mara nyingi wawekezaji wamekuwa wakija hapa nchini wakipewa ardhi lakini baadaye wakipata fursa mbali mbali kwa mfano hiyo fursa ya kodi ambayo mara nyingi huwa wanatoa kwa muda fulani wasilpe kodi. Lakini baadaye wanageuza. Mhe. Spika, wengine wamekuwa wajanja kugeuza ile fursa ambayo wameipata baadaye kuweza kufanya ujanja na kuwapa watu wengine.

Mhe. Spika, ni lazima tuwe makini, Sekta ya Utalii au Kamisheni ya Utalii ni lazima iwe makini na suala hili. Kwa sababu yale manufaa ambayo imekusudia kuyapata hayataweza kufanikiwa ikiwa kutakuwa na mtindo huu. Ni lazima sheria hii iweke vipengele ambavyo vitawabana wawekezaji kuhusu msingi mzima na zana nzima ya kodi ambayo wanasamehewa.

Mhe. Spika, ni mtindo sasa hivi kuona kwamba pengine mwekezaji alipokuja katika Sekta ya Utalii alikuwa na jina fulani. Lakini baada ya miaka mitano mwekezaji pengine amekusudia anageuza jina. Vile vile inawezekana pengine mwekezaji amekuja kapewa ardhi baada ya miaka mitano ardhi ilke akampasia mtu mwengine na kuweza kuendesha biashara. Kwa hivyo, ninachokusudia kusema hapa Kamisheni ya Utalii iwe makini na mazingira haya ambayo yamekuwa ni mtindo sasa hivi katika dunia, na sio hapa kwetu tu Zanzibar, lakini ni mtindo katika dunia.

Mhe. Spika, hivi karibuni nilibahatika kwenda Burundi na nilipoondoka hapa nikawa nimetajiwa jina la hoteli ambayo nitafikia, lakini kufika uwanja wa ndege tu naambiwa sasa hivi tunakwenda *Source DUNIL* nikashangaa! Nikasema mbona hoteli imeandikwa jina hili? Nilipofika kule hoteli nikaonesha kwamba hoteli niliyopangiwa mimi ni hoteli hii hapa, sasa mbona nimewekwa hapa? Nikaambiwa ndio hii hii, ilikuwa jina fulani lakini sasa hivi limebadilishwa limekuwa jina fulani. Sasa ninachokusudia kusema kwamba mazingira haya ni ya ulimwengu si mazingira ya Zanzibar tu, ni mazingira ambayo yapo ulimwenguni hivi sasa kwa wawekezaji wote.

Kwa hivyo, Kamisheni ya Utalii ni lazima iwe makini na sheria ichukue mkondo wake kwa hili, kwa sababu vyenginevyo tutakuwa tunawapa watu fursa za kujiendeleza lakini fursa zile hawazitumii kama tulivyokusudia.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ninapenda kuchangia katika mswada huu, wenzangu walijaribu kulizungumza kuhusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, mchangiaji mmoja alizungumza kwamba vyuo vyetu au skuli ziwe na utaratibu wa kusomesha mafunzo ya utalii. Napenda nimuarifu kwamba hivi sasa Wizara ya Elimu tayari imeshaliona hili na tayari ina utaratibu mzima wa kuweza kufundisha mafunzo ya utalii katika vyuo vyetu vya amali vilioko Mkokotoni pamoja na Vitongoji. Kutakuwa na mafunzo maalum ambayo yataweza kuwafundisha vijana ambao watabahatika kuingia katika vyuo hivi na kuweza kujifunza mambo ya utalii na baadaye waweze kupata fursa ya kuweza kujiendeleza au kupata ajira katika Sekta ya Utalii.

Kwa hivyo, napenda nimhakikishie kwamba, serikali kupitia Wizara ya Elimu tayari imeshaliona hilo na imeona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuweza kujenga mazingira mazuri kwa vijana wetu hasa katika Sekta hii ya Utalii.

Katika ukurasa wa 41 mimi kidogo inawezekana ikawa sijafahamu hapa, napenda nifahamishwe vizuri kwa sababu sijapaelewa.

Mhe. Spika, katika kipengele cha 7(3) panaposema kwamba, “bodi inaweza wakati wowote kutengua jukumu ililoipa kamati, bila kujali kama kamati imekamilisha au haijakamilisha jukumu au majukumu ambayo imepewa na bodi hiyo”. Hapa naomba Mhe. Waziri kidogo anipe ufafanuzi wa mazingira gani ambayo yatapelekea pengine bodi isijali majukumu ambayo tayari imeshawapa kamati na iweze kutambua wakati wowote bila ya kujali. Naomba Mhe. Waziri hapa aniwekee wazi kwa sababu sijafahamu.

Vile vile katika ukurasa wa 42 kuna kipengele sijakifahamu vizuri naomba Mhe. Waziri pengine atoe ufafanuzi na wajumbe wapate fursa au kuweza kuelewa vizuri. Mhe. Spika, katika kipengele cha 9(6) nacho kidogo kinanipa utata.

Kifungu 9(6) kinasema:

> “Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 4 cha kifungu hiki, iwapo kikao hakitafanyika kutokana na kutopatikana akidi. Bodi itafanya kikao hiki tarehe inayofuata na wajumbe waliohudhuria itakuwa ndio akidi ya kikao na watakuwa na uwezo wa kuendesha shughuli za kikao hicho”.

Mhe. Spika, kipengele cha 4 kinasema akidi ya kikao ni nusu ya wajumbe walioteuliwa kwa wakati huu. Mhe. Spika, hapa nadhani anakusudia kwamba kama kikao kimeitishwa mara moja na siku ile pengine wajumbe hawakuhudhuria wengi kiasi ya kupitisha idadi ya kikao ambayo inatakiwa. Kwa hivyo, siku ya pili hata kama hawakuja maana yake hata kama wamekuja wajumbe wawili maana yake ni kwamba wajumbe hao watakuwa na majukumu ya kupitisha kikao hiki. Sijui kama hivyo nilivyofahamu ndivyo au vipi, kama ndivyo nilivyofahamu mimi kidogo inanipa wasi wasi, kwamba wajumbe wawili tu ndio waliohudhuria siku ile waweze kupitisha maamuzi kidogo, mimi inanipa wasi wasi. Naomba Mhe. Waziri aje atupe ufafanuzi ili tuweze kufahamu vizuri zaidi.

Mhe. Spika, nadhani kama nilivyosema kwamba sina mchango mkubwa kwa sababu matayarishao yangu pia hayakuwa mazuri. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtoni naomba niunge mkono Mswada huu wa Sheria ya Utalii na utakapopitishwa basi nadhani inawezekana ukatekelezwa vizuri na Sekta hii ya Utalii ikatupa manufaa makubwa zaidi. Mhe. Spika, naunga mkono ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuzungumza machache katika kuchangia mswada huu ambao Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji ametuletea ili kuboresha mazingira ya utalii hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia nataka niseme kwamba, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mimi kidogo nataka nijaribu kuzungumzia suala zima la nini maana ya mazingira mazuri ya utalii? Mhe. Spika, mswada huu tumeupata na tumejaribu kuuangalia kuna baadhi ya marekebisho yaliyofanywa, kwa sababu tulikuwa tuna Kamisheni ya Utalii ambayo ilikuwa ikiongozwa na mwenyekiti. Kama serikali yetu ilivyoamua kwa makusudi kuona umuhimu wa utalii katika nchi yetu ndio maana hata jina la wizara likabadilishwa na likaanza kwa jina la utalii. Kwa hivyo, hii ni serikali yetu kuona umuhimu gani wa kuweza kuupa nguvu utalii katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, tukiangalia kwenye madhumuni, kwa sababu madhumuni ndio zaidi inayotoa *summary* ya yale madhumuni mazima ya ule mswada, kwa ruhusa yako nitaomba ninukuu kidogo ili baadaye nikitoa yale maelezo yangu yawe yanaowana na yale ambayo ninayazungumza.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria unalenga kuweka mfumo bora wa kisheria ili kujenga mazingira mazuri ya kukuza biashara ya utalii ambapo sekta ya umma na binafsi zitahamasishwa kuendesha shughuli zinazojali mazingira shughuli za kiutalii baharini na ardhini katika anga ya Zanzibar.

Vile vile imeendelea, utakapopitishwa mdawa huu utatoa sura ya utekelezaji wa dira ya malengo na majukumu, sera mpango ambayo inafafanua uhusiano wa dira 2020 pamoja na mpango wa kupunguza umasikini Zanzibar. Sasa hapa Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri ametumia umakini mkubwa sana kwa kuweka hii *summary* ambayo haya yote tutakayoyazungumza humu madhumuni yake makubwa yalikuwa katika maeneo haya.

Mhe. Spika, tunapozungumzia mazingira mazuri ya utalii, kwanza visiwa vyetu vya Zanzibar vyenyewe vinajiuza katika suala zima la utalii. Mhe. Spika, kwa wenzetu wanaobahatika kusafiri sana nchi za nje wanaona jinsi nchi za Ulaya zilivyokuwa si nzuri kimaumbile. Lakini kwa bahati Mwenyezi Mungu amewajaalia uwezo na uwezo wao wakautumia vizuri, sasa hivi mtu akitaka kujisifia basi anajifananisha na nchi za Ulaya.

Mhe. Spika, Zanzibar kwa bahati nzuri sana Mwenyezi Mungu ametujaalia pamoja na umaskini wetu tuliokuwa nao na tukijitahidi huu utaondoka. Lakini visiwa vyetu Mwenyezi Mungu amevijaalia viko katika mazingira mazuri sana ya utalii. Kwa hivyo, sisi kazi yetu inapungua katika kutengeneza huu utalii lakini katika kuvutia watalii au uwekezaji katika hii sekta ya utalii.

Mhe. Spika, ukiangalia fukwe zetu ni nchi chache sana duniani zenye fukwe zilizokuwa maridadi, nzuri tena zenye mchanga mweupe ambao mtu anaweza akagaragara na baadaye wala asione kwamba ameingia vumbi. Kwa hivyo, hii ni moja katika kivutio kikubwa cha uwekezaji katika utalii.

Sasa je, sisi wenyewe tumejitayarisha vipi katika kulinda hizi fukwe zetu, lakini katika kulinda taswira ya visiwa vyetu, ili huu uzuri ambao tuliojaaliwa na Mwenyezi Mungu tusiuharibu.

Kuna wenzangu waliotangulia wao walianza kuzungumza hata ujenzi wetu wa mahoteli yetu haya ya kitalii unakwenda kinyume na maelekezo hata ya mswada. Kwa sababu unapozungumza mazingira mazuri ya utalii, kwa hiyo yale mazingira yenyewe kwanza ya kuweka kile kinachomvutia mtalii kinatakiwa kiwe vizuri.

Sahibu wangu Mhe. Abass Juma Muhunzi alitoa mfano mzuri sana ambao unaeleza ni namna gani mimong'onyoko ya ardhi inapokuja zaidi katika yale maeneo ambayo yaliyojengwa haya mahoteli. Sasa kitu ninachokiomba

kwamba kuna yale ambayo yaliyokwisha kujengwa itabidi sasa tujirekebishe ili tufuate sheria na mazingira yanavyotaka ya uwekezaji.

Kwa sababu katika Sheria ya Mazingira inaeleza kuna mita maalum ambazo kutoka katika fukwe ya bahari mtu haruhusiwi kujenga, lakini hayo makosa tayari kuna baadhi ya maeneo yameshafanyika.

Sasa hivi ukiangalia hata bahari kwa sababu bahari ina njia zake, unapoilazimisha isipite katika njia ile itatafuta sehemu nyengine ya kupita. Sasa hiyo utakuta kuna kuta zinajengwa ambazo zinazuia hata ile *flow* ya maji. Mhe. Spika, mimi nafikiri kuna baadhi ya mambo itabidi lazima tukae tuangalie upya ili tuweze kwenda vizuri na huu utalii wetu tusiuharibu.

Mhe. Spika, kwa upande wa serikali sisi kazi yetu kutengeneza sheria na baadaye tukaleta Barazani kwa ajili ya kupata maoni ya Waheshimiwa Wajumbe na kuzipitisha na kwa ajili ya kuzifanyia kazi. Kwa hivyo, kwanza kitu ambacho ninachokiomba zaidi kwa watendaji wetu ambao tuliwapa dhamana katika kusimamia hizi sheria tunazozipitisha hapa. Kwa sababu sheria yoyote inataja watendaji. Ukiangalia kwenye mazingira kuna Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira.

Mhe. Spika, kwa kuwa sisi tumeshatunga sheria umeshapewa meno sasa hakuna sababu ya kwenda kumuuliza mtu je, sasa hivi nitekeleze au nisitekeleze. Watendaji wetu wakati mwengine tunapokuwa na mwahali mwingi na matokeo yake mambo yanaanza kuharibika. Katika mazingira yetu mtu anafanya makosa na sio kama hajui anafanya makosa, anajua kwamba mimi hapa sasa hivi ninafanya makosa. Lakini makosa yenyewe inakuwa kama ile hadithi ya ngamia anajaribu anapenyeza kichwa kidogo anasikiliza je, mwenye nyumba atashtuka. Kama mwenye nyumba hajashtuka anapenyeza na shingo kibanda chenyewe cha mgongo ngamia akisimama tu basi anakiondoa. Umeanza kumruhusu sitaki nirejee, kaingiza na shingo, sasa hivi umemuachia kaingia mwenyewe. Kwa hivyo, matokeo yake unakuta yule ngamia uliyemkaribisha amekubomolea nyumba.

Mhe. Spika, sisi tunaopewa dhamana basi nadhani tutekeleze wajibu wetu vizuri. Kwa sababu ukimuachia huyu kajenga hapa hujamchukulia hatua na mwengine ataiga kama yule hujamchukulia hatua, ndio ule mfano wa ngamia niliosema na mwengine atafanya. Sasa mwengine akishaona mmoja, wawili, watatu wamevunja sheria wameachiwa, basi sasa yeye ndio anaingia mzima mzima anakibomoa mpaka kibanda chenyewe na kibanda chenyewe ndio huu utalii wetu.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba kwamba watendaji wetu ambao tuliwapa dhamana na katika sheria mbali mbali wametajwa, basi tukishatunga hizi sheria wao ndio wanaotakiwa wazisimamie katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Spika, tukizungumzia mazingira mazuri ya utalii serikali imeshajitahidi kufanya mambo mengi sana katika kuboresha mazingira ya utalii Zanzibar. Nakumbuka kwenye miaka ya 2001/2002 siku hizo sisi ndio kwanza wabichi hapa, mimi kwa bahati nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kipindi hicho Mwenyekiti wangu alikuwa Mhe. Rufeya Juma Mbarouk, alikuwa akikamata *mike* hapa basi nyumba inakaribia kupasuka. Tulitembelea katika maeneo ya utalii, ilikuwa tukishakwenda kwenye kamati basi siku ya pili mwenyekiti wetu inabidi mpaka saa 4 tumsubiri hajaamka. Mhe. Spika, Mhe. Rufeya sote tulikuwa tunamjua mtu mzima lakini kashiba kidogo. Kwa hivyo, ile mikiki mikiki ya barabara kwenda katika hayo maeneo ya utalii, kwa sababu mwenyekiti wangu pamoja na kwamba alikuwa mtu mzima na mwili wake mzito, lakini hakubali lazima anataka ashiriki.

Kazi kubwa tulikuwa tunaifanya katika *field*, tulikuwa tunakwenda katika ukanda ule wa Kiwengwa, tunakwenda katika maeneo ya Paje, yaani tunapasua huko kwa huko. Tunachukua karibu masaa 4 mazima hatujafika katika safari yetu kwenda na kurudi hadi tunarudi jioni. Kwa hivyo, tuliporudi hapa kwenye kamati taarifa zetu tukiangalia kwenye *hansard* zitakutikana. Tulikuwa wakali kweli kweli, tunasema serikali yetu imeanzisha utalii na kipindi kile ilikuwa bado haijapewa moja kwa moja kwamba utalii ndio uti wa mgongo, ilikuwa bado tunazungumzia karafuu ndio uti wa mgongo, utalii pale ndio ulikuwa unazidi kukuzwa ili ushike nafasi. Tulikuwa tunasema kweli kweli.

Lakini kutokana na usikivu wa serikali yetu inayoongozwa na Mhe. Rais wetu mpendwa Mhe. Amani Abeid Karume na Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali anayesimamia utekelezaji wa ilani na utekelezaji wa majukumu ya serikali Mhe. Waziri Kiongozi Shamsi Vuai Nahodha ambaye sasa hivi na yeye ananisikia. Walikuwa yale tunayoyasema na kama hivi tukisema yeye utamkuta ameinama anaandika. Sasa sio kama yalikuwa yanaishia hapa hapa, yalikuwa yanapangwa na utekelezaji wake sasa hivi hayataki tochi kila mtu anayaona. Kwa hivyo, hata wale wananchi ambao waliotuleta hapa sasa hivi wanajua faida na matunda ya kuwaleta waheshimiwa wao hapa Barazani. Kwa sababu mambo mengi ambayo yalikuwa hayajafanywa na serikali, serikali imejitahidi kwa nguvu zote kuweza kuyatekeleza.

Nadhani Mhe. Spika, kabla hatujamaliza bajeti ya mwaka 2010 mwezi Julai, basi ungelimualika siku moja mwenyekiti wangu mstaafu Mhe. Rufeya Juma Mbarouk, ukaja siku moja ukamkabidhi Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na

Kamati ya Fedha na Uchumi. Halafu umwambie yale uliyokuwa ukiyapigia kelele kwenye mwaka 2001/2002 sasa hivi twende ukashuhudie wewe mwenyewe serikali imetekeleza katika kiwango gani, nadhani atatoa saluti. Sasa kama angelikuwemo humu yeye nafikiri angekuwa ndio msemaji mkuu wa mwanzo. Lakini kwa bahati kutokana na umri wake tumemwambia pumzika sasa hivi sisi wanafunzi wako tumeshakolea tuachie tuendeleze hili jahazi.

Kwa kweli Mhe. Spika, Waswahili wanasema kwamba ukisubiri kusifiwa basi pale umeshafunikwa shuka watu wanakupepea juu pale sifa zote zitatajwa. Lakini kama bado unatwina utaelekezewa zaidi lawama.

Kwa hivyo, kwa kweli Mhe. Spika, serikali kwa upande wake haya mazingira yaliyoelezwa katika mswada kuweka mazingira mazuri, basi kwa asilimia kubwa serikali imeshatekeleza tena kwa vitendo na sisi wenyewe tunaridhika.

Mhe. Spika, ilikuwa watalii wanapotoka *Airport* basi ile mizigo yao kulikuwa kuna magari yale ya mbavu za mbwa, maana yake mtu mwenye *hiace* yake kipindi hicho alikuwa haipeleki hata siku moja. Kuna magari yale mengi yalikuwa ya vikundi vya ushirika yalikodishwa kodishwa kwenye mahoteli yakawa yanatumika. Kwa sababu yale ndio yanayohimili vishindo vya mashimo panda shuka, panda shuka, mabegi yanapakiwa kwenye gari yake mbali na wageni wanapakiwa kwenye magari yao mbali.

Mhe. Spika, hata hizo hoteli zenyewe zilikuwa vibanda vya makuti. Walikuwa wanakuja wale wanatuambia uwekezaji mtu anaweka makuti yake ukija kupiga hesabu kumbe hata wewe unaweza. Lakini sasa hivi hasa kwa maelekezo ya serikali kwamba tunataka mtujengee mahoteli yanayoitwa ya utalii.

Maana yake walikuwa wanatudanganya wanasema watalii huku wakija wanapenda makuti kwa sababu kwao nyumba zao za bati. Sasa huku ndio wanataka ile *eco-tourism* (utalii wa mazingira), basi utalii wa mazingira vibanda vya makuti. Kumbe vile walikuwa wakitudanganya danganya. Lakini kutokana na maelekezo na usimamizi wa serikali sasa hivi kuna mahoteli ya kisasa yamejengwa, kama utakwenda kuchukua *moving camera* ufanye kama una-*act* uko katika ziara basi mtu ukimwambia hapa nilikuwa Ufaransa kumbe ulikuwa Lagema. Utamwambia nilikuwa Italy au Ujerumani kumbe ulikuwa Kempinski. Sasa Mhe. Spika, hii ni hatua kubwa kweli kweli. Hii yote imekuja kutokana na yale mazingira mazuri.

Mhe. Spika, nitazungumzia suala dogo ambalo sahibu wangu Mhe. Rashid Seif Suleiman alilizungumza. Kwa kuwa tuko Barazani lazima tuzungumze, ajira ya waheshimiwa ni kusema, kama huwezi kusema basi wananchi hawakuleti tena.

Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa kila mtu aseme, sio aseme tu lakini aseme kwa niaba ya wananchi wake zaidi wale waliomtuma.

Mhe. Spika, moja ya mazingira mazuri unaweza ukawa na nchi nzuri, fukwe nzuri, mahoteli mazuri lakini hali nzuri ya kuishi kwa amani, utulivu, kupendana hicho ni kigezo cha mwanzo kabisa.

Nashukuru wageni wengi unapokutana nao katika nchi mbali mbali wanakwambia kabisa, Zanzibar ni sehemu ambayo ni tofauti na sehemu nyingi duniani. Sababu yenyewe nini? Kwanza ukarimu.

Mhe. Spika, wewe umeshakwenda Ulaya, Ulaya unaweza ukaanza tokea asubuhi mpaka jioni wewe unaranda kutwa nzima hakuna hata mtu mmoja atakayekuuliza hali. Watu wanapishana kama ng'ombe, huyu kampiga kibega huyu, lakini wanapokuja kwetu wanashangaa sawa sawa na sisi tunavyoshangaa.

Unajua Mhe. Spika, mimi siku za mwanzo nilipokuwa nakwenda kwenda huko nchi za watu, ile mtu kupishana naye tu basi utataka umtolee asalam alaykum japo mkono tu kama mjomba Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) hayupo. Maana yake mjomba anakusalimia kama anataka kukupiga kibega hivi.

Mhe. Spika, wakati mwengine mtu ile hali umeshamuuliza basi anakutazama hivi, nikaona eeh! nisije nikaonekana huku wakuja, maana yake Waafrika wapo huko wenzetu lakini nisije nikaonekana wakuja, mwisho na mimi nikawa napishana nao tu kama ng'ombe. Kwa sababu wao ukiwauliza hali wanakushangaa, lakini hapa kwetu utashangaa mpaka vitoto vidogo *hallo*! *hallo*! Kwa hivyo, ule ukarimu wetu kwa kweli umetupelekea salamu nyingi sana duniani, sasa hiki ni kitu ambacho tunahitaji sisi hasa tuliokuwemo ndani. Sisi ndio viongozi humu, tukisema suu! basi wale tunaowalea watatupita kwa sababu wao wana kasi kuliko sisi. Kwa hivyo, sisi suu! yetu tuizungumze katika hali ya amani na utulivu.

Zanzibar mara nyingi na ndio asili yetu tuko wakarimu mtu hata kama humjui. Mimi siku moja nilitoa mfano watu wakaniona labda nimedanganya, lakini mfano huu nitaendelea kuutoa. Zamani makwetu huko shamba kama anakuja mgeni anapishwa tena anapishwa ndaniii. Nazungumza mila na utamaduni, maana yake hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere siku zote anazungumzia kwamba mtu aliyekuwa haithamini mila yake basi atachukua mila ya mwenzake. Kwa hivyo, ule ulikuwa ni ukarimu, wewe leo mtu chumbani akiba zako zote ndio unaficha huko, maana watu wa zamani hata pesa hawaweki benki, basi zile akiba zote zinawekwa chumbani chini ya mchango, anapishwa mgeni ndani wenyewe wanakaa sehemu nyengine.

Kwa hivyo, ule ni utamaduni wetu yaani tuko na amani na utulivu mzuri, mara nyingi tunaishi katika hali nzuri. Lakini inapokaribia masuala haya ya uchaguzi *Allah Akbar* hatari, mama hamjui mtoto, mtoto hamjui mjukuu, wala bibi hamjui babu, watu wanapishana kama wazungu. Sasa mimi naomba tusiwe hivyo.

Mhe. Spika, kama hatuwezi, maana yake kuna kabila moja kule wenzetu Bara kama ukioa hujampiga ngumi yule mke basi anasema kwao kwamba yule mwanamme hafai. Sasa kwa mazingira ya Zanzibar akija kwenu mtu akisema hafai watu watashtuka, lakini kwa kule Bara watu hawashtuki hivyo. Sasa Mhe. Spika, sio ile ya Tumbatu, maana yake Tumbatu watu wakienda kushtaki kama mume wangu hafai, *Allah Akbar* watu itabidi wawekane hapo atafutwe bibi.

Wenzetu kule Bara kuna kabila moja kama mtu hujamtia mangumi na mateke ukamtoa tezi basi hajisikii kama mume wangu hasa ananipenda. Mhe. Spika, nazungumzia ile ile ya sahibu wangu, sisi kama hatuwezi kitu kidogo tu kwa sababu hakuna asiyependa maendeleo, hakuna *CUF*, hakuna CCM, hakuna CHADEMA, hakuna NCCR, sote tunayapenda maendeleo . Lakini kama tunahisi ikishafika kipindi kama hiki lazima tujikunjue kidogo na yale mambo yetu mimi nafikiri Mhe. Spika, sisi si ndio tunaotunga sheria, hebu turekebisheni hapa sheria. Katiba tunatunga sisi, sheria tunarekebisha sisi, tuwekeni sasa.

Kwa sababu kwanza ukiangalia miaka mitano ni kidogo, hebu tuweke uchaguzi kila baada ya miaka kumi. Sisi si ndio tunaotunga sheria, sasa kila baada ya miaka kumi ndio uchaguzi, miaka minane tutakuwa tunajenga nchi, mwaka mmoja kampeni, mwaka mmoja ule kuondoa yale machungu kupunguza chuki na uhasama. Kwa sababu hata kama ulipata ngeo basi ule mwaka baada ya uchaguzi unapata kujichua chua pale ukanyooshwa ukarudi katika hali ya utulivu.

Sasa miaka minane Mhe. Spika, kama tunajenga nchi hasa tumeshikana wallahi tunafika mbali kweli kweli. Lakini tunawafuata hawa wazungu sasa hivi kila baada ya miaka mitano uchaguzi watu hawaelewani. Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk sasa hivi hayupo lakini angesema kweli. Tulikuwa tukienda Pemba kule anatuandalia na wenzangu wapo Mhe. Ame Mati Wadi, Mhe. Tafana Kassim Mzee msije mkasema alikuwa anapewa chakula na *CUF*, aaa si peke yangu. Tunakwenda kwa Mhe. Said Ali Mbarouk anatupiga mpunga halafu anawaambia wale watu wake, mnawajua nani hawa, anawaambia Wawakilishi wa CCM, wanashtuka hivi ah! Lakini tumeshakula wameshatuletea kila kitu, tunasahau yote. Lakini sasa hivi sijui kama Mhe. Said Ali Mbarouk akinikaribisha kwake kama nitakwenda kula.

Mhe. Spika, huu mfano nilikuwa nautoa yale mazingira, hii miaka kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi inatupa tabu kweli kweli. Lakini sisi Mhe. Spika, ni maskini, nchi maskini zinatakiwa zijenge uchumi imara halafu baadaye wafanye mambo mengine.

Mhe. Spika, nitakutolea mfano mmoja. Nchi zote za Ulaya walijitawala kwanza wakaongoza nchi zao si chini ya miaka 100 ndio wakaanzisha demokrasia ya mfumo wa vyama vingi. Lakini kwanza walizisimamia nchi zao wakajenga uchumi imara. Kwa sababu Mhe. Spika, demokrasia wakati mwengine inaharibu mambo mengi, mtu anaweza akafanya utumbo, basi mwachieni maana yake kura ile unailea, mwachieni msalieni Mtume.

Lakini kama mfano mko mnaendesha serikali mnasimamia shughuli zenu maelekezo ya serikali yanafuatwa, basi nchi zinapiga hatua kubwa sana za maendeleo. Sasa tatizo letu sisi hapa demokrasia hii inatupa tabu kidogo.

Mhe. Spika, Mzee Abeid Amani Karume alitoa wasia, unajua hawa viongozi wakati mwengine wanakuwa wanaona mbali. Mzee Karume alisema kwamba Zanzibar hakuna uchaguzi mpaka baada ya miaka 50. Sio kama alikuwa anataka aendelee kukaa yeye kwenye madaraka, alijua sisi binadamu kuna vitu vina hisia, kuna mambo watu wanakumbuka, sasa watu wakae mpaka wayasahau. Lakini sasa sisi kwa wazungu demokrasia, utawala bora, tunataka kusaidiwa tumeingia miaka 50 haikutimia ile matokeo yake ndio haya hapa.

Mhe. Spika, hili nilikuwa natoa tu mfano kwamba kama sote tumeshahisi kwamba haya masuala ya usalama yanaharibika katika uchaguzi turekebishe, kama miaka 10 mingi basi tufanye 7, miaka 2 ile ya kampeni, mmoja wa kampeni kabla ya uchaguzi, mmoja kuweka sawa mambo na wale ulioshindana nao, miaka mitano tunajenga nchi tungefika mbali.

Mhe. Spika, kama utakuja huo mswada sijui nani atakataa. Nadhani Mhe. Zahra Ali Hamad ndie atakayepiga vigelegele, mswada huu najua haupingi miaka 7 humu ndani, maana yake unajua tunapata muda wa kuendesha nchi, tunapanga mipango yetu ya maendeleo. Kwa hivyo, waamuzi wa mazingira mazuri zaidi ndio sisi humu tuliokuwemo Barazani.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mswada kuna mambo mengi yamezungumzwa humu. Huu utalii upo katika maeneo mengi na utalii unaleta faida kubwa sana kwa watu wetu. Mhe. Spika, utalii umetekeleza ile sera yetu ya *vision* 2020 ya kupunguza umaskini. Hii sera ya *vision* 2020 kupitia utalii kuna wengine sio umewapunguzia umaskini umewaondolea kabisa umaskini. Mhe. Spika, sasa hivi vijana wetu wengi baada ya kuja kutupigia hodi serikalini tunataka ajira

basi moja kwa moja wanakwenda zao katika sekta za utalii na wengi wao wanajiajiri wenyewe.

Mhe. Spika, sasa hivi wenye vituo vya petroli, zamani Unguja nzima vilikuwepo vituo kama vitatu, sasa hivi kila siku vinaanza vituo vipya. Sasa utalii huu ukiondoka vituo vile itabidi vitaanza kufungwa kimoja baada ya kingine, haya mafuta atamuuzia nani. Zanzibar hii hizo gari zinakwenda wapi hata vituo vyote hivyo viuze mafuta. Lakini harakati za utalii wanaopeleka mazao huko kwenye mahoteli kwa sababu watalii wanakula wale. Kwa hivyo, utakuta kuna wakulima wa mboga mboga wamepata ajira, wenye magari yao wengine mtu akishastaafu ananunua kijibasi chake anampa mwanawe anabeba watalii. Ajira nyingi imejitokeza kupitia katika sekta ya utalii na ndio maana nikasema kuna wengine kutokana na hii sera ya utalii na *vision* 2020 sio kama imepunguza umaskini imeuondoa kabisa.

Sasa hivi kuna watu kuna watu wamefungua tour *operators* wameajiri vijana wengi kweli kweli, yeye mwenyewe alikuwa maskini lakini kupitia sera ya utalii na *vision* 2020 amewaajiri vijana wengi sasa hivi kila mmoja anajitegemea na yeye anatengeneza faida.

Mhe. Spika, wakulima wetu zamani mapapai yote yalikuwa anapelekewa Mhe. Tafana Kassim Mzee, sio anapelekewa yeye wapiga kura wake. Katika watu wanaojua kuyatumia mapapai vizuri hakuna kama Jimbo la Uzini. Ukienda yanarowekwa kwenye mapipa yale *time* kama hizi ukienda watu wanagongana wanasinzia wana kiwanda kule. Viwanda vidogo vidogo kule Wilaya ya Kati vipo vingi lakini sasa hivi watu wengi wanakimbilia mjini maana yake mapapai hayapatikani, siku hizi watu wengi wanakunywa bia. Lakini mapapai yote sasa hivi yanakwenda hotelini. Kwa hivyo, utakuta hata wale wakulima wetu, hata wale wakulima wa Mhe. Haji Mkema Haji, wengi wakulima wa mapapai sasa hivi mapapai yananyang'anyiwa. Ukiangalia ndimu Mhe. Spika, zamani sisi tulikuwa tunakwenda tunagaiwa. Sasa hivi nani akakugaie ndimu, ndimu ina thamani kubwa sana. Hii ni kwa kuwa soko la utalii.

Kwa hivyo, tunaposema utalii ni uti wa mgongo, basi tunatakiwa tuuenzi kweli kweli. Mhe. Spika, tukisema kwamba utalii tunauvuruga au unaharibika hawaji hawa ndugu zetu, basi itabidi sasa tuanze kuingiana maungoni kwa sababu chakula huna itabidi uende kwa jirani, jirani hana itabidi uende kwa mjomba, mwisho utawamaliza maana yake unapanga jana nilikwenda kwa mjomba nani, kesho nitakwenda kwa baba mdogo na kesho kwa nani, mwisho mtaanza kukimbia mkisikia hodi mnatoka kwa mlango wa nyuma. Sasa hivi hii sekta ya utalii imeajiri watu wengi tena kweli kweli.

Mhe. Spika, mazingira ya utalii yana mambo mengi. Kuna baadhi ya masuala hasa katika mambo ya *license* yamezungumzwa hapa, nafikiri Mhe. Waziri atakuja kuelezea vizuri. Kuna baadhi ya wananchi wetu na hili nilikuwa naomba sana niliseme Mhe. Spika, kwa sababu tunatengeneza sheria nzuri wakati mwengine wananchi wetu wanaposhindwa kuzifahamu, matokeo yake baadae tunakuja kulaumiana.

Kuna biashara hawaruhusiwi kufanya wageni, lakini kutokana na upeo mdogo wa watu wetu anaweza akaja mtu kutoka nje, keshaiona hii fursa mimi naweza nikaitumia lakini nitafute mgongo wa huyu Mzanzibari ambayo ndio katika sheria yetu nafasi kubwa imempa Mzanzibari, akaatumia mgongo wa Mzanzibari yule ili yule kuweka uwekezaji wake. Matokeo yake yule atakayekuja atakuja na *capital* kubwa, kwa hivyo anaweza aka- *invest* pale, akatumia mgongo wa Mzanzibari huyo au mswahili huyo, kumbe sekta ile inaweza kuchukua watu wengi wakaifanya wao. Lakini anakuja mtu mmoja akamkamata Mzanzibari anafanya kama yeye ndio yake.

Kwa mfano mtu anaweza akafungua kampuni ya *tour operator*, unajiuliza mswahili huyu mabasi yote kayapata wapi, tangu lini, benki gani iliyomkopesha yeye na ikamuamini mabasi yote hayo, pengine kuna mtu kaingia ubavuni pale. ukiangalia hata ile *share* yake. Ndio maana katika sheria imeeleza kwamba kutakuwa na utafiti sasa, mpaka ile miradi ambayo inaambiwa ina *share holder,* je huyu mswahili kweli ana hisa zake pale na kama ana hisa ngapi.

Kwa sababu wakati mwengine tunaweza tukatumiwa, watu wanasema tutapigwa kwa bakora yetu, ndio kama hii. Mtu anakuja anatuchapa kwa bakora yetu wenyewe. Kwa hivyo, kuna mambo hapa vijana wetu au watu wetu inabidi tuwape maelekezo ya kutosha. Kama fursa ile unaweza kuitumia basi itumieni ili waweze kuitumia wengi.

Kwa mfano, biashara yako unaweza kuifanya lakini mtaji wako mdogo, shirikianeni na wenzenu, kwa sababu mkishirikiana watu kama wanne au watano mkifungua kampuni pale kila mmoja anaandika *share* zake basi ile kazi inakua yenu halafu nyinyi mawazo yenu yanazidi kutanuka baadae mtakuja kutanua biashara zaidi. Lakini unaposema unajificha katika mgongo wa mgeni kwa kukutumia wewe, kwa hivyo asilimia yako ndogo ya faida ndio sasa unatengeneza mrorongo wa watu wengi kuja kukuomba, kwa sababu wale watakuwa hawana kazi ya kufanya.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tutakuwa tunakazi kubwa na zaidi katika kamisheni yetu hii ambayo tunaijenga upya na itakuwa na majukumu mengi ambayo yametajwa. Vile vile na kazi zake za bodi itaweza kutusaidia katika yale

mapungufu ambayo tuliyoyakosea, basi watajaribu kuwaeleza wananchi wetu ili turudi katika ile nia na dhamira ya uwekezaji katika nchi yetu. Uwekezaji huu faida kubwa inatakiwa waweze kufaidika wananchi.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie kidogo suala la mazingira. Suala la mazingira Mhe. Spika, katika utalii linagusa sana. Tunashukuru kuna baadhi ya mahoteli vile walivyojenga mahoteli yao basi hawakutaka kuchonga chonga, ile ndio hasa *echo tourism*, hawakutaka kuchonga mfano jiwe ulitowe uweke sijui vitu vyengine, wameboresha tu kidogo, yale mawe wameyazungushia mbolea na wamepanda miti kule imeota vizuri sana.

Mhe. Spika, lakini tujiulize kabla ya kuanzishwa sekta ya utalii katika mahoteli kwenye mawe yale kulikuwa kunaota nini baada ya nguruwe tu, walikuwa wanaota nguruwe tu kule, ndio walikuwa wanakaa. Sasa ndio maana tukasema walikuwa wanaota nguruwe tu.

Mhe. Spika, baada ya kuanza uwekezaji wa mahoteli ya kitalii wametuonesha ni namna gani uzuri wa kisiwa hiki, ndio lile nililolizungumza mwanzo na kama tutaweza kutumia akili zetu tukaboresha vizuri, basi hiki kisiwa Mhe. Spika, kitakuwa mali kweli kweli, kwa sababu kila mtu atataka kuja kuishi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa katika maisha yangu sikufikiria kama mnazi unaweza ukaung'oa pahala ukaenda kuupanda sehemu nyengine ukaota, na wengi wetu humu walikuwa hawajui sio mimi tu, kwa sababu mara nyingi kitu ukikifikiria wewe basi mwenzako alikuwa anataka kukisema wewe umetangulia tu.

Mhe. Spika, nitatoa mfano katika hoteli ya *Kempiski* wenzetu wale, maarufu ilikuwa inaitwa kwa Mchina mwanzo, tulikuwa tunaona watu wanakwenda kubeba minazi, tukawa tunasema hawa wendawazimu. Maana kitu chochote kama hujakijua kama hujapata dozi ile ya elimu huwezi ukajua hasa maana yake, tukasema hii minazi sasa wanaipeleka wapi, wengine tena jamaa zangu wa kule pwani wakasema hawa wazungu kweli hawana akili, kwanza wanakwenda uchi halafu wanachukua minazi wanakuja kuipanda kweli itaota hii. Kumbe inaota bwana. Mhe Spika, minazi imeng'olewa mizima mizima imekwenda kupandwa. Tena imekwenda kupandwa maweni, lakini kumetiwa mbolea na mambo mengine huwezi ukaamini kama pale palikuwa mawe matupu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ndio tunapozungumzia suala la mazingira, kweli wazungu watoke kwao waje watufundishe sisi mazingira, waje watufundishe kujenga nchi yetu. Sasa hii inakuwa kinyume kinyume. Viongozi wetu

walikuwa wanatupa wasia wanatuambia nchi tunatakiwa tuijenge sisi wenyewe tusisubiri mgeni atoke kwao aje ajenge nchi yetu. Sasa wakati mwengine watu wetu kutokana na akili zao finyu, sasa hivi hao wazungu wametoka kwao wamekuja kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, ukanda wa mawe sasa hivi unaota misheli sheli na masheli sheli yanaota, minazi inapandwa na inaota tena katika maeneo ambayo yalikuwa ni mawe matupu. Sasa hii ni elimu tujifundishe. Leo watu wetu wanakaa katika ardhi ambayo ina mbolea mtu hata huna haja ya kupanda mnazi, ile nazi tu imeanguka imekaa siku nyingi unakuja kuukuta mche umeota, wewe baada ya kuushughulikia kuuwenga enga ukaota ukawa mkubwa ukaja kukusaidia baadae, basi sasa hivi sisi ndio tumeinunua misumeno ya moto tunaikata minazi.

Wazungu wameng'oa minazi wamekwenda kupanda maweni. Waswahili minazi imeota katika ardhi ya mbolea wanaikata kwa misumeno, anakuambia anatengeneza vitu na vitu vyengine. Jamani eeh, halafu hata hiyo minazi tumesema pamoja na umri. Wewe umeshafika miaka 60 umeshazeeka, leo mnazi haujabalehe umeshakatwa.

Mhe. Spika, kwa kweli hapa tujifunze, huu utalii wa mazingira sio kwamba watalii wasikanyage ile miti, hapana wao tayari wenzetu wameshatuonesha mfano, kwa hivyo hili ilikuwa tunatakiwa sisi tuliige. Mhe. Burhan Saadat Haji mzee wetu, mimi nafikiri siku hizi duniani kila tarehe imeandaliwa utaratibu wake. Nadhani mwaka huu katika ile siku ya mazingira duniani, basi mheshimiwa japo mwakani ungetafuta fedha nyingi kwanza ukaja ukatufanyia semina, ndio kwa sababu hapa Mhe. Spika, ndio *center*. Ndio maana pale mwanzo nilisema kwamba sisi ndio wenye jukumu kubwa la hii nchi, ukisema 'suu' basi wale wananchi wako ile *speed* yao watakupita wewe.

Mhe. Spika, Mhe. Burhan Saadat Haji, Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira ambapo mazingira ipo chini ya wizara yako mwakani tutafute fedha, tutafute fedha kwanza unakuja kutupiga dozi hapa ya mazingira, halafu na sisi tunakuwa walimu wa kwenda kuwaelimisha watu wetu. Vile vile tufanye makongamano hasa vijijini katika yale maeneo ambayo miti inakatwa ovyo, twende tukawaelimishe na tuwachukuwe hasa wale wenye misumeno ile ya mbao tuwachukuwe tuwapeleke Kiwengwa tukawaoneshe kwamba huku kulikuwa kuna mawe matupu, sasa hivi angalia hii minazi unayokata wewe basi wenzetu wameiotesha huku. Kwa hivyo, hebu tubadilishe badala ya kwamba wewe una msumeno wa moto basi tukutafutie mbolea sasa uipande wewe hii minazi.

Mhe. Spika, wananchi wetu zaidi wanataka elimu, sasa hivi kuna mikutano mingi na inazungumzia sana suala la mazingira. Wakubwa wameshaharibu hewa huko duniani, joto jingi wakati mwengine. Mhe. Spika, samahani nitatoa mfano mdogo. Kuna kipindi sisi tulikuwa Geneva kule Msumbiji na Angola ilikuwa ni wakati wa kiangazi, mheshimiwa kulikuwa kuna mafuriko. Wakati wa kiangazi Angola na Msumbiji kulikuwa kuna mafuriko. Walikuja wale wenzetu wanaoshughulika na masuala ya maafa, wametoka kule wanakuja roho zinawatapa wanasema jamani tuwasaidie vipi wenzetu wanakufa. Kuna nini, aah maana yake kule *River Mpopo* sijui imeshafurika. Watu wanajiuliza, jamani kiangazi hiki, ndio. Kwa sababu mvua hazina mpango sasa hivi.

Kwa hivyo, haya mambo wakati mwengine wewe unakwenda na shoka yako unakata mti, ule mti ndio unaoita mvua. Vile vile ule mti ndio unaosaidia hata hizi hewa, kwa hivyo wewe kama utakuwa unajikatia tu hii miti na hii miti sio Mwenyezi Mungu kaiumba tu, kaiumba kwa maana yake. Tukila mboga mboga ndio dawa ya maradhi tunapata afya na mambo mengine. Vile vile tunapokuwa hatuutumii kwa utaratibu tunaharibu mazingira.

Mhe. Spika, siku hizi hata wakati wa masika pia joto. Sasa wewe jiulize wakati wa masika mvua tupu joto linatokea wapi, kwa sababu Mhe. Spika, tunaharibu mazingira. Kwa hivyo, utalii na suala la mazingira unachukua nafasi kubwa sana tena sana.

Mhe. Spika, juzi tarehe 14 ilikuwa ni siku ya kimataifa ya maafa, leo tuna tarehe 15. Mhe. Spika, katika nchi ambazo ziko katika hatari ya kukabiliwa na maafa makubwa na Zanzibar tumo, kwa sababu Zanzibar ni visiwa tena vidogo kweli kweli.

Mhe. Spika, sasa hivi kwenye Bara la Atantika kama sikosei kule kuna mabarafu makubwa sana, nadhani sijalikosea hilo Bara. Mhe. Spika, mabarafu yale inasemekana kwa muda wa miaka zaidi ya milioni kadhaa iliyopita, kila siku yalikuwa ni mabarafu matupu. Mhe. Spika, sasa hivi mabarafu yale yanayayuka. Inasemekana ile *regularity* ya bahari iko katika Bara lile, yaani ujaaji wa maji na ukupwaji wa maji uko katika Bara lile. Kwa hivyo, ina maana ile ndio ilikuwa ina-*balance* maji ya bahari, sasa hivi imeshayayuka. Kwa hivyo, katika nchi ambazo ni za visiwa, Mwenyezi Mungu atuepishie mbali, usije ukasikia siku moja unaamka hupo, kwa sababu unapoamka hupo, wewe si ulilala na unategemea utaamka asubuhi kuna bahari. Sasa haya Mhe. Spika, katika mazingira yetu ya kawaida watu wetu hawajui.

Mhe. Spika, tunakwenda katika mikutano kule wenzetu wanakuja wanalia namna vile visiwa vyao vinavyoliwa. Mhe. Spika, ndio maana nikasema wakati wa kiangazi *River Mpopo* ilijaa na ilifurika, kwa hivyo na hapa kwetu tusije

tukashangaa. Mhe. Spika, masika tu hapa Kwahani, Mhe. Ali Suleiman yuko wapi hapa hayupo. Kwahani pale tunapeleka boti tunaokoa watu. Hii Mhe. Spika, inatokana na mazingira kubadilika.

Kwa hivyo, suala la maafa Mhe. Spika, katika visiwa vyetu tukitumia rasilimali zetu vibaya, ardhi tukiitumia vibaya basi kuna hatari kubwa ya maafa, hata tunapojenga katika vianzio vya maji tunakaribisha maji kupotea, kwa sababu maji yanakimbia miguu, pale kuna mitope tope unakwenda unaikata unajenga nyumba chini ya vianzio vya maji, utegemee nini Mhe. Spika, maafa. Maji hakuna siku zote mtamlaumu Mhe. Tafana Kassim Mzee, lakini wewe umejenga chini ya kianzio cha maji, maji yatakuja wapi.

Mhe. Spika, kwenye mabonde ya mpunga, bado ni utalii huo. Kwenye mabonde ya mpunga Mhe. Spika, tukijenga mule tutakula nini. Kwa hivyo, utalii una mambo mengi. Kwanza utalii uwakute watu wameshiba.

Mhe. Spika, tunapozungumzia suala la utalii hasa kutengeneza mazingira mazuri ya utalii, kwanza unatakiwa uipende nchi yako. Vile vile ukubali yale yaliyokuwepo uyaendeleze ili wale wapate kuvutiwa kuja katika nchi yako.

Mhe. Spika: Nafikiri umalizie sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nilitaka kueleza kazi za bodi, lakini wataeleza wenzangu. Kuna wenzangu nadhani hawajachangia, kesho tukijaaliwa wataelezea kazi za bodi, kuna Mkurugenzi baada ya Mwenyekiti kuna Mkurugenzi, bodi kazi yake nini, hawatakiwi wafanyekazi ziku zote. Kuna vitu vyengine watakuja kueleza wenzangu.

Sasa mimi kwa kuwa mswada huu tulipata nafasi tukauzungumza sana, ndio maana tukasema haya tuliyoyaleta hapa zaidi wenzetu watie nyama. Mimi nilikuwa najaribu kuzungumzia mazingira mazuri ya utalii na mazingira mazuri ya utalii serikali imeshajitahidi kwa upande wake, kazi iliyobakia ni sisi kwetu tufanye marekebisho haya aliyoyaleta Mhe. Waziri tuunge mkono mswada huu, ili Mhe. Waziri tumpe nafasi kubwa ya kuweza kufanyakazi.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru tena, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Spika: Tunashukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi kwa mchango huo ambao si mfupi sana. Dalili ilionekana mapema kwamba Mhe. Waziri ni mchangiaji wa mwisho, kwa sababu kwa muda mrefu nilikuwa naomba kwamba majadiliano yanaendelea.

Kwa hivyo, kesho tukijaaliwa baada ya kipindi cha maswali tunategemea kwamba Mhe. Waziri afanye majumuisho moja kwa moja. Baada ya maneno hayo basi naahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 16/10/2009 saa tatu za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi kesho tarehe 16/10/2009 saa 3:00 za asubuhi)